Nipashe
Jumanne Novemba 19, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580079
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Mchungaji aanzisha 'tuisheni' ya sekondari bure kanisani

UKURASA 3




UKURASA 13


**YALIYOMO**

UKURASA WA 2

**ANYONGWA KWA KAMBA YA VIATU**
MTOTO Andrea Sekei mwenye umri wa miaka saba, ameuawa kwa kunyongwa na kamba ya viatu na watu wasiojulikana...

UKURASA WA 4

**MCHAKATO UCHAGUZI CHADEMA WAANZA**
CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimetangaza ratiba...

UKURASA WA 8

**BOSI BODI YA KOROSHO AWEKWA KIKAANGONI**
WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amemwagiza Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Julius Mtatiro, ahakikishe anaondoka na Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho hadi ...

**VIGOGO CHADEMA WAJIPELEKA MAHAKAMANI**
UKURASA 3


# Pengo amtabiria makubwa Makonda

**ASEMA** utendaji wake unambeba kurithi mikoba ya Magufuli, atamani wawapo vijana wengi kama yeye... *Endelea ukurasa wa 2*

Distributed via ippmedia


Pengo


Makonda



Scan Hapa
Google Play App Store

# Mkapa ashtushwa na kasi ongezeko la watu

UKURASA 2

**MICHEZO** MSUVA AIKATAA VAR IKIINGIA MOROCCO UK. 31

**MAONI, KATUNI UK.6**

# Pengo amtabiria makubwa Makonda

**Na Mary Geofrey**

ASKOFU Mkuu mstaafu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Polycarp Kardinali Pengo, amesema anafurahishwa na utendaji wa Paul Makonda na anaona Mkuu huyo wa Mkoa wa Dar es Salaam anafaa kurithi mikoba ya Rais John Magufuli.

Pengo (75), aliyasema hayo jana katika mkutano uliowakutanisha viongozi wa dini na Makonda kuzungumzia mafanikio ya miaka minne ya uongozi wa Rais Magufuli katika jiji hilo.

Alisema kama wakiwapo vijana wengi wanaomsaidia kazi Rais Magufuli mfano wa Makonda, ni wazi kuwa hakutakuwa na haja ya kufikiria nani ataendeleza kazi nzuri zinazofanywa na Rais huyo.

"Tunajiuliza baada ya Magufuli atakuwapo nani, mkiwapo kama wa aina yako (Makonda) wengi, mimi nisingekuwa na shaka kwamba tungekuwa na watu gani wa kuendeleza kazi za Magufuli," alisema Kardinali Pengo.

Kiongozi huyo wa kiroho pia alisifu kazi aliyodai ni nzuri ya Makonda kueleza miradi inayotekelezwa na serikali, akifafanua kuwa Mkuu wa Mkoa huyo ameonyesha ni aina gani ya kiongozi anayemsaidia Rais Magufuli.

"Makonda asante kwa kuniita, katika uzee niliyonao, ningekuwa nimechoka kukaa saa mbili ulizokuwa unaeleza kazi zinazofanywa na serikali, lakini sikuchoka hata katika hali yangu ya uzee. Na hata ongeongeza saa nyingine moja ningekuwapo bila kukuomba ruhusa ya kutoka nje," alisema.

Kardinali Pengo alidai Makonda ni moja kati ya wasaidizi bora walio pembeni ya Rais Magufuli na wanapomwombea aendelee, wanaombea na vijana wa aina yake waendelee.

"Na tunamwomba Mwenyezi Mungu atujalie viongozi wa aina yako wengi zaidi. Kwa maana hii Rais ni mtendaji kazi, lakini hawezi kufanya yote peke yake, anahitaji watu chini, juu na pembeni yake ambao wapo naye kwa ajili ya kumsaidia," alisema.

Kardinali Pengo pia alimpongeza Rais Magufuli kwa kazi anazozifanya tangu aingie madarakani na kuwashangaa watu aliodai wanamwita dikteta.

"Katika mitandao kumezuka maneno kwamba Rais wetu ni dikteta. Yale anayoyafanya anashughulikia kuendeleza vitu kuliko kuendeleza watu.

"Wanaongelea juu ya kushughulikia vitu kuliko watu ni watu gani hao hawajashughulikiwa wakati mambo mengi yanafanyika kwa ajili ya watu?

"Ni lugha ambayo kwa akili zangu za kizee, siwezi kuelewa, utakuwa unamshughulikia mtu kiasi gani kama unamfanya mtoto wake na mjukuu wake waende shule?" alihoji Pengo.

Awali, Makonda alisema kasi ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo inayofanywa na Rais Magufuli, inazidi maelekezo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Kawafanya hata viongozi wa serikali wanaotumia hirizi kumtaja Mungu kwanza. Mara nyingi ameweka wazi kuwa mambo yanavyokwenda kasi hata yeye mwenyewe anamshangaa Mungu," alisema.

Makonda alisema katika kukabiliana na tatizo la utiririshaji wa majitaka, Mkoa wa Dar es Salaam, yuko kwenye mpango wa kuanzisha vituo maalum kwa ajili ya kuchakata maji taka na kuyarudisha kwenye matumizi.

Alikumbusha mpango wa kujenga kituo eneo la Jangwani na kitagharimu Sh. bilioni 800.

INAENDELEA UK 8

# Mkapa ashtushwa na kasi ongezeko la watu

**Na Sanula Athanas**

RAIS mstaafu Benjamin Mkapa amesema ongezeko la watu ni tishio kwa maendeleo ya nchi, akishauri kuwe na sera madhubuti ili kulikabili.

Katika kitabu chake cha 'My Life, My Purpose' (Maisha Yangu, Kusudio Langu), kilichozinduliwa na Rais John Magufuli jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, Mkapa anagusia hoja hiyo akieleza shaka yake kuhusiana na kasi ya ongezeko la watu nchini.

Anasema anasikitika kuona suala hilo ni tatizo kubwa si tu Tanzania, bali bara la Afrika kwa ujumla huku kukikosekana mjadala wa kutafuta ufumbuzi wake.

Mkapa aliyeiongoza Tanzania kwa miaka 10 kuanzia mwaka 1995, anasema katika kitabu hicho kuwa haoni sera na mwongozo sahihi wa kuikabili ishara hiyo mbaya kwa maendeleo ya umma.

"Ongezeko la watu katika nchi siyo kipimo cha maendeleo bali ni kikwazo kwa maendeleo. Shida kubwa ya nchi nyingi za Kiafrika hatuna mjadala madhubuti kuhusu sera ya idadi ya watu katika nchi zetu," Mkapa analalamika.

Kiongozi huyo mstaafu anaeleza ubashiri wa kisayansi wa mwelekeo wa sensa zijazo, kwamba ifikapo mwaka 2025, ambao ndiyo ukomo wa Dira ya Maendeleo ya Taifa, nchi inatarajiwa kuwa na wakazi milioni 67. Tanzania ina eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 947,300.

Juni 1999, Tanzania ilizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambayo pamoja na mambo mengine, inalenga kupunguza nusu ya watu wanaoishi katika umaskini na kuwafanya wawe katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Mkapa anabainisha kuwa wakati wa uhuru mwaka 1961, kulikadiriwa kuwapo Watanganyika milioni 10.4 na idadi iliongezeka hadi milioni 27.4 alipoanza kukalia kiti cha urais mwaka 1995 na iliongezeka hadi milioni 36.1 wakati anaondoka mwaka 2005.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Tanzania mwaka huu, inakadiriwa kuwa na watu 55,890,747 (milioni 55.89). Kati yao, wanaume ni 27,356,189 na wanawake 28,534,558.

Kwa makadirio hayo, idadi imeongezeka kwa watu milioni 43.59 katika kipindi cha miaka 42 kwa kuwa takwimu za NBS zinaonyesha mwaka 1967, Tanzania ilikuwa na watu milioni 12.3, Tanzania Bara ikiwa na watu milioni 11.9 na Zanzibar watu 354,815.

Vilevile, Ripoti ya Juni 21, 2017 ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu (UNFPA), ilibainisha kuwa Tanzania imo katika nchi tisa zinazochangia kasi ya ongezeko la watu duniani. Tanzania ilitangazwa kuwa ni ya nne barani Afrika.

Ripoti hiyo inaitaja India, taifa linalokadiriwa kuwa na watu bilioni 1.3, ndiyo ya kwanza kwa kasi kubwa ya ongezeko la watu na katika mataifa nane yanayofuata, matano ni ya barani Afrika na matatu ni ya kusini mwa Jangwa

INAENDELEA UK 8

Distributed via ippmedia



Mtumishi wa Mahakama ya Wilaya ya Temeke, Lezilie Koini, akiwa chini ya ulinzi wa askari Polisi baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Anyongwa kwa kamba ya viatu

**Na Elizabeth Faustine, MWANZA**

MTOTO Andrea Sekei mwenye umri wa miaka saba, ameuawa kwa kunyongwa na kamba ya viatu na watu wasiojulikana wakati akichunga mbuzi, kondoo na ndama eneo la Mahiringa wilayani Magu mkoani Mwanza.

Baba mzazi wa mtoto huyo, Sekei Andrea, mkazi wa kitongoji cha Mahiringa, kijiji cha Isangijo, alisema Jumamosi asubuhi, Andrea alipeleka wanyama hao malishoni na ilipofika saa tano kama ilivyo kawaida yake kuwarudisha nyumbani kwa ajili ya kunywa maji, hawakurudi.

"Nilianza kushtuka saa 5:00 nikasema vipi mbona huyu leo haleti mapema mifugo, kwanini? Nilipofika nikaja kwangu hapa kuna mkubwa wake nikamwambia aende akamwangalie kule anakochungia. Akaenda akaanza kuzungukazunguka lakini hakumuona.

Muda kidogo nikasema nenda sasa hivi au mama yako ukamwambie na huyo Vero wapitie njia nyingine nami nipitie hapa twende tukamtafute. Tukaanza kutafuta mpaka huko nikapata kondoo mmoja.

Nikakutana na wachungaji wengine nikaanza kuwaeleza wakasema muda wa saa tatu saa nne alikuwa anachungia pale mbugani, lakini walimkosa na walimkuta huyo kondoo tu," alisema.

Sekei alisema kuwa baada ya kumtafuta kwa muda bila mafanikio, walishauriana kuwa wengine waende mnadani Igoma kumtafuta na ilipofika saa 12:00 jioni wakiwa kule mnadani, walipigiwa simu kuwa mtoto ameshaonekana lakini amefariki dunia.

"Ninaomba serikali ifanye mchakato wapatikane hao watu waliofanya hili tukio la kumnyonga mtu mpaka kufa," alisema Sekei.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mahiringa, Balekele Balele, alisema watuhumiwa waliotenda kosa hilo la kinyama waliondoka na mbuzi na kondoo zaidi ya 50 aliokuwa akiwachunga mtoto huyo.

"Taarifa za kutoonekana mtoto nilipokea nikiwa msibani Kisesa, nikasema kitu cha kwanza baba

INAENDELEA UK 8

HABARI KITAIFA

# Mchungaji aanzisha 'tuisheni' ya sekondari bure kanisani

Na Beatrice Moses

MCHUNGAJI Kiongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Kimara, Dar es Salaam, ametangaza mkakati wa kutoa mafunzo ya ziada ya bure kwa wanafunzi wa sekondari kwa kuwatumia walimu ambao ni waumini wake.

Lengo la mpango huo ni kuinua kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa sekondari sambamba na ushauri nasaha.

Mchungaji huyo, Willibrod Mastai, ambaye pia ni Kaimu Naibu Katibu Mkuu wa KKKT Dayosisi ya Mashariki na Pwani (Utawala, Utumishi na Milki), alitangaza hatua hiyo kwenye ibada ya Jumapili iliyopita usharikani hapo.

Katika kile kinachoonekana kupata mwitikio kwa waumini, walimu zaidi ya 30 walijitokeza, huku mchungaji huyo akieleza kuwa anaamini kutakuwa na matokeo mazuri.

Aliwataka wazazi na walezi washarika wa kanisa hilo wenye watoto wanaosoma kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne kuwaandikisha kwa ajili ya masomo ya muda wa ziada yatakayotolewa bure kila Jumamosi.

"Tumekuwa tunawaombea wanafunzi wetu kila inapofika kipindi cha mitihani ya taifa, lakini nimeona kwamba kuna haja ya kutathmini na kusaidia maandalizi yao kwa kuwatumia walimu wetu ambao ni washirika hapa," alisema mchungaji huyo.

"Pia kuna wataalamu wa masuala ya ushauri nasaha watakuwapo, ili kuwasaidia vijana kujitambua na kuendelea kuwa na maadili mazuri kwa manufaa ya kanisa na taifa kwa ujumla," alisema.

Mchungaji Matsai alianzisha hatua za kufanikisha mkakati huo wiki mbili zilizopita kwa kuwaita walimu ili kubaini idadi yao na masomo wanayoofundisha.

Baada ya hapo walijitokeza walimu 25 kabla ya kuongezeka idadi hiyo juzi na kufikia 32.

Alisema atashughulikia mahitaji ya walimu hao ikiwamo nyenzo za kufundishia.

"Nasisitiza ni vyema kushughulikia sababu za wanafunzi kushindwa kufanya vizuri kwenye mitihani kuliko kuwaombea pekee," alisema, huku waumini wakishangilia kwa kupiga makofi.

# Hatimaye wabunge Chadema wajisalimisha

Hellen Mwango

HATIMAYE wabunge wawili cha Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), akiwamo Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa na Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche, wamejisalimisha jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Mbunge mwingine aliyejisalimisha ni wa Kawe, Halima Mdee ambaye alijisalimisha Kituo cha Polisi Oysterbay baada ya mahakama hiyo kutoa hati ya kukamatwa kwa kukiuka masharti ya dhamana katika kesi ya uchochezi inayowakabili.

Hata hivyo, baada ya kufika mahakamani waliwekwa chini ya ulinzi wa askari polisi, na wote waliunganishwa na kupelekwa Kituo cha Polisi Oysterbay.

Kesi hiyo imepangwa kuendelea kusikilizwa leo ushahidi wa utetezi mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Mshtakiwa mwingine aliyeandikiwa hati ya kukamatwa ni Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya, anayedaiwa kuwa mgonjwa na kulazwa.

Mapema Ijumaa ya wiki iliyopita mahakama hiyo ilitoa hati ya kuwakamata washtakiwa hao wanne kwa kukiuka masharti ya dhamana pamoja na wadhamini wao kwenda kujieleza kwanini hawakutimiza wajibu wao kuwapeleka washtakiwa mahakamani.

Washtakiwa hao walikiuka masharti hayo kwa kushindwa kufika mahakamani hapo bila kutoa taarifa.

Awali kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa ushahidi wa mshtakiwa wa kwanza, Mwenyekiti wa Taifa Chadema, Freeman Mbowe, ikiwamo kuhojiwa na mawakili wa Jamhuri.

Wakili wa Serikali Mkuu, Faraja Nchimbi, alidai kuwa washtakiwa wanne hawapo mahakamani na kwamba Jamhuri haina taarifa, aliiomba mahakama kutoa hati ya kukamatwa kwa kukiuka masharti ya dhamana.

Hakimu Simba alisema Novemba 15, mwaka huu kesi hiyo ilipangwa kuendelea kusikilizwa ushahidi wa utetezi leo (jana) saa 3:00 asubuhi.

Alisema mahakama yake inatoa hati ya kukamatwa washtakiwa hao wanne kwa kukiuka masharti ya dhamana pia inatoa hati ya wito kwa wadhamini wao kwenda kuieleza kwanini hawakuwapeleka washtakiwa kusikiliza kesi yao kama masharti ya dhamana yanavyowaelekeza.

Wakili wa utetezi, Faraji Mangula, alidai ameshika mikoba ya mawakili wa utetezi, Profesa Abdallah Safari, Peter Kibatala na Jeremiah Mtobesya kwamba ana taarifa za Bulaya.

Hata hivyo, hakimu alimwelekeza Wakili Mangula kwamba mwenye jukumu la kutoa taarifa za mshtakiwa ni mdhamini na siyo kazi ya wakili.

Wakili Nchimbi aliiomba mahakama itoe hati ya kuwakamata washtakiwa hao na wito kwa wadhamini wao ili wajieleze kwa nini hawakuwapeleka washtakiwa mahakamani kama masharti ya dhamana yanavyotaka.

Mahakama hiyo iliridhia na kutoa amri ya kukamatwa washtakiwa na wito kwa wadhamini. Kesi hiyo itaendelea kusikilizwa ushahidi wa utetezi Novemba 19, 20 mpaka 21, mwaka huu.

Washtakiwa waliofika mahakamani jana ni, Mbowe, Naibu Katibu Mkuu Chadema, upande wa Zanzibar, Salum Mwalimu, Naibu Katibu Mkuu Bara na Mbunge wa Kibamba, John Mnyika, Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Vincent Mashinji na Mbunge wa Tarime Mjini, Ester Matiko.

Katika kesi hiyo Mbowe na wenzake wanakabiliwa na mashtaka 13, ikiwamo kula njama, kufanya mkusanyiko wenye ghasia na kuhamasisha hisia za chuki kwa Watanzania dhidi ya serikali.

Distributed via ippmedia



# Jaji Mkuu awaonya majaji wapya

Na Hellen Mwango

JAJI Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, amewaonya majaji wapya kuacha kupokea maelekezo ya namna ya kusikiliza kesi mahakamani na kutoa uamuzi badala yake wafuate kanuni za utumishi wa umma na kutoa haki kwa wananchi.

Kadhalika, aliwaasa kuzingatia mafunzo yaliyoandaliwa na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) ya siku 21 kwa kuwa watatokea katika mazingira tofauti na yanawaleta kwa pamoja katika kutekeleza kazi ya utoaji haki kwa mahakama.

"Kila mmoja alikuwa na maisha yake kabla, miunganiko yenu ya zamani ikiwamo marafiki, ndugu, majaji wazoefu au wasaidizi wenu wa sheria msiruhusu kuwaingilia kwenye uhuru wa kutoa maamuzi ya mahakama," alisema.

Akifafanua alisema wakati wa kazi zao za ujaji watakumbana na majaribu mbalimbali ya kuingilia uhuru wao, lakini watapambana na majaribu hayo iwapo watasimamia na kufuata viapo vyao. "Nawataka msome kanuni zinazotoa mwongozo ambazo zinaelekeza kuwa ofisa wa Mahakama ya Tanzania, analindwa na misingi ya usawa, haki na maadili katika kazi zao kwa kufuata kanuni," alisema Jaji Mkuu, huku akizitaja kanuni hizo.

Kati ya kanuni hizo inamtaka kila mmoja kujikinga kuingiliwa katika kazi zao hasa kutoka kwa ndugu, marafiki na hata wenza weo.

Pia, inawakumbusha wasiruhusu watumishi wengine kuonyesha kwamba wako katika nafasi muhimu ya kuathiri kazi zao.

Aliwakumbusha kanuni zinazohusu uhuru katika kufanya kazi zinaweza kuathiri wakati mwingine zikasababisha kujitoa kwenye shauri lililopo mbele yao ili aonekane yuko huru.

"Kwa mfano kanuni nyingine inakutaka ujiondoe kwenye kesi inayoweza kuhoji uhuru wako, muyasome maamuzi mbalimbali ya Mahakama Kuu na Rufani mjiridhishe muone umuhimu wa kujitoa," alisema na kuongeza:

"Mfano kesi ya Mwita Chacha na wenzake iliyoamriwa 2007 na Mahakama ya Rufani kwamba jaji anaweza kujitoa pale anapoona kwamba anaweza kuegemea upande mmoja katika maamuzi yake, lakini unapaswa kutoa sababu kwanini unajitoa."

Alisema utayari wa kujitoa bila sababu za kutosha ni ubakaji wa kazi za kimahakama na utachochea maombi yasiyo ya msingi kwa maofisa wa mahakama kujitoa katika kesi mbalimbali pale wanapoombwa na walalamikaji na walalamikiwa kufanya hivyo.

Alitoa mfano katika kesi maarufu ya Chavda iliyoamriwa mwaka 2016, jaji aliwasikiliza wadaiwa, maombi ya kuongezewa muda akaahirisha kutoa uamuzi kwa miezi 18, wadaiwa walipofika mbele yake alijitoa kwenye kesi hiyo kwa sababu mmoja wa wahusika alikuwa mteja wake kwenye kampuni yake ya uwakili kabla hajapata ujaji.

Kesi hiyo ilienda kwa marejeo mahakamani ya rufaa, mahakama hiyo ilieleza kuwa ofisa anaweza kujitoa wakati wowote kesi inapotokea kama akibaini ana maslahi binafsi, lakini isiwe kwa sababu zisizo za msingi.

"Majaji wanapaswa mara moja wanapopangiwa majalada kesi kuyasoma kwa makini ili kugundua kama kuna maslahi yoyote binafsi, sababu nyingine binafsi zisiingilie majukumu ya kukwamisha uhuru, imani ya dini na mazoea yasiruhusiwe kuingizwa kwenye mwenendo wa kesi hizo na baadaye kwenye uamuzi watakaoutoa kama majaji.

Distributed via ippmedia



Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Baroda, India, Shanti Lal Jain, ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Benki hiyo, nchini, akimkabidhi Nathumal Sajnanai, cheti cha makabidhiano ya kituo cha watoto yatima wasioona cha Sri Satya Sai, Kariakoo, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mchakato uchaguzi Chadema waanza

Na Enock Charles

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimetangaza ratiba yake ya uchaguzi wa ngazi mbalimbali za viongozi wake wa Kitaifa na Mabaraza ya chama hicho unaotarajiwa kuanza Disemba mwaka huu.

Akizungumza na vyombo vya habari Jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Vincent Mashinji, alisema Mkutano Mkuu wa kuchagua viongozi wakuu wa chama ikiwamo Mwenyekiti wa chama hicho unatarajiwa kufanyika Disemba 18, mwaka huu.

"Baada ya uchaguzi katika mabaraza Disemba 16 kutakuwa na Kikao cha Kamati Kuu kwa ajili ya uteuzi wa awali na Disemba 17 kutakuwa na Mkutano Mkuu na kufiatiwa na Baraza Kuu kwa ajili ya kupitisha majina ya wagombea kabla ya Mkutano Mkuu kwa ajili ya uchaguzi wa viongozi wa Kitaifa " alisema Dk. Mashinji.

Akizungumzia kuhusu uchukuaji wa fomu za kugombea nafasi mbalimbali, alisema ulianza jana, na mwisho itakuwa ni Novemba 31, mwaka huu na Disemba 7 Kamati Kuu ya chama hicho itakutana kwa ajili ya majina ya wagombea walioomba nafasi katika chama hicho ili kufanya uteuzi wa awali wa wagombea wenye sifa.

Akitaja nafasi zinazotakiwa kugombewa katika ngazi ya kitaifa, alisema ni Mwenyekiti wa Chama Taifa,Makamu Mwenyekiti mmoja kutoka Tanzania Bara na mwingine kutoka Zanzibar, wajumbe 8 wa Kamati Kuu, katibu mkuu, naibu katibu mkuu Bara na naibu katibu mkuu kwa upande wa Zanzibar, mweka hazina wa chama,wawakikishi watano wa mkutano mkuu na wawakilishi 20 wa baraza kuu.

Kuhusu upatikanaji wa fomu za kugombea nafasi hizo, Dk. Mashinji alisema zinapatikana Makao Makuu ya chama hicho, ofisi za kanda, ofisi za mabaraza na katika tovuti ya chama hicho, na kuonya vitendo vya upendeleo katika uchaguzi huo.

# Akiri kupokea rushwa 200,000/-

Na Hellen Mwango

MTUMISHI wa Mahakama ya Wilaya ya Temeke, Lezilie Koini, amekiri mahakamani kutenda kosa la kupokea rushwa ya Sh. 200,000 baada ya kusomewa shtaka la kupokea fedha hizo.

Mbali na Kooni, mshtakiwa mwingine ambaye imetolewa hati ya kukamatwa ni, askari polisi Itialy Omary.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustina Mmbando.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Odessa Horombe, alidai kuwa Mei 8, 2018, mshtakiwa Omary na Koini kwa pamoja walipokea rushwa ya Sh. 200,000 kutoka kwa Mussa Abdallah, ikiwa kama kishawishi asipatwe na hatia katika kesi namba 211/2018 dhidi ya kosa la usalama barabarani.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo mshtakiwa alikiri kutenda kosa hilo, upande wa Jamhuri ulidai bado haujaandaa maelezo ya awali, uliomba tarehe nyingine.

Pia upande wa Jamhuri ulidai kuwa hauna pingamizi la dhamana dhidi ya mshtakiwa.

Hakimu Mmbando alimtaka mshtakiwa kutimiza masharti ya kuwa na mdhamini mmoja mwenye barua na vitambulisho halali atakayesaini hati ya dhamana ya Sh. 500,000.

Mshtakiwa huyo ametimiza masharti ya dhamana yupo nje kwa dhamana, kesi itatajwa Novemba 21, mwaka huu.




## HABARI KITAIFA



Wafanyakazi wa kampuni ya usafi wakisaidiana kupakia mafurushi ya takataka kwenye gari, katika eneo la Kimara, jijini Dar es Salaam wikiendi. **PICHA: JOHN BADI**

# ‘Watu 4,000,000 kufariki kwa kisukari mwaka huu’

**Na Romana Mallya**

WAKATI ugonjwa wa kisukari ukitajwa kuongezeka mara tatu zaidi kama ilivyokuwa miaka 20 iliyopita, inakadiriwa watu milioni nne wanaoumwa duniani wanatarajiwa kufariki dunia mwaka huu.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Aga Khan, Dk. Ahmed Jusabani, aliyasema hayo juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kisukari Duniani.

Katika maadhimisho hayo, hospitali hiyo iliweka kambi maalum ambayo wananchi walijitokeza kupima afya zao na kupewa elimu namna ya kujikinga wasikipate.

Dk. Jusabani alisema jumla ya watu milioni 4.2 duniani wanategemewa kufariki dunia kwa ugonjwa huo mwaka huu, na kwamba ugonjwa huo umeongezeka mara tatu zaidi ya miaka 20 iliyopita, huku asilimia 75 walioupata ni watu wenye kipato cha chini na kati.

“Theluthi mbili ya wagonjwa wa kisukari wapo mjini. Hili ni janga la kimataifa, tunapenda tuifanyie kazi ili kulipunguza janga hili Tanzania,” alisema na kuongeza:

“Hii inania ya kuongeza ufahamu kwenye familia kutambua dalili, hatari za kisukari, kuwatunza wagonjwa, kuboresha kinga na kuelimisha.”

Pia alisema endapo kisukari kikiachwa bila kutibiwa kinaleta madhara hatarishi makubwa ikiwa ni pamoja na kumsababishia mtu upofu, kukatwa miguu, figo kushindwa kufanya kazi, mshtuko wa moyo na kiharusi.

“Kisukari kimesababisha watu milioni nne kupoteza maisha yao katika miaka miwili iliyopita, Aga Khan imechukua hatua ya kuboresha ufahamu wa watu kuhusu vyanzo vya ugonjwa huu na kinga zake na kuanzisha kliniki ya sukari yenye wataalamu kwa ajili ya kuchunguza, kutibu na kuelimisha,” alisema.

Dk. Jusabani alisema takwimu za kidunia zinaonyesha wanaoishi na kisukari ni watu 463 ambapo kati yao watoto ni milioni 1.1.

Naye Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani wa hospitalini hapo, Samina Somji, ambaye ndiye mwanzilishi wa kambi na kliniki ya kisukari alisema wameanzisha hilo lengo ili watu waangalie afya zao mapema na kuchukua hatua za kujilinda wasikipate.

**“Kisukari kimesababisha watu milioni nne kupoteza maisha yao katika miaka miwili iliyopita, Aga Khan imechukua hatua ya kuboresha ufahamu wa watu kuhusu vyanzo vya ugonjwa huu na kinga zake na kuanzisha kliniki ya sukari yenye wataalamu kwa ajili ya kuchunguza, kutibu na kuelimisha,” alisema.**

Distributed via ippmedia

# Majaliwa asimamisha vigogo watatu TBA

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemtaka Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Daud Kondoro, ajitathmini kuhusu utendaji kazi wake, huku akiwasimamisha kazi wakurugenzi watatu wa wakala huo.

“TBA tunaihitaji, lakini watu wake wana shida. Hatuwezi kuwaacha, TBA wasipewe miradi kwa sababu hawawajibiki na wanadhani kwa kuwa ni taasisi ya serikali ndio wataachwa wafanye mambo ya ovyo.”

Waziri Mkuu akiwasimamisha kazi wakurugenzi hao, jana, alipotembelea mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) eneo la Njedengwa jijini Dodoma.

Wakurugenzi walioasimamishwa kazi ni Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Ujenzi, Humphrey Killo, Kaimu Meneja wa Miradi, Abdallah Awadh na Kaimu Mkurugenzi Idara ya Ushauri, Hamis Kileo.

Waziri Mkuu alichukua hatua hiyo baada ya kutoridhishwa na utendaji kazi wa TBA katika miradi mbalimbali waliyopewa na serikali ukiwamo ujenzi wa jengo la NEC ambalo ujenzi wake ulianza Julai, 2017 na ulitakiwa ukamilike Juni 2018 kwa gharama ya Sh. bilioni 13. Hata hivyo, mradi huo haujakamilika na ujenzi wake umesimama.

Akiwa katika eneo la mradi wa ujenzi wa ofisi ya NEC, Waziri Mkuu alihoji sababu za mradi huo kutokamilika kwa wakati, ambapo kaimu mkurugenzi wa ujenzi alisema jengo hilo limeshindwa kukamilika kwa sababu wakati walipokuwa wanaanza kazi walibaini kuwa kuna vitu vilisahaulika wakati wa uandaaji wa Bill of Quantities (BOQ). TBA ndio waandaaji wa ramani ya jengo hilo na ndio wajenzi.

“Bajeti ya awali ilikuwa Sh. bilioni 10 wakati wa uandaaji wa michoro ya ujenzi gharama zilizongezeka na kufikia Sh. bilioni 13 ambazo ndizo tulikubaliana katika mkataba. Wakati tunaendelea na kazi tuligundua kuna vitu vimesahaulika kwenye BOQ jambo lililoongeza bajeti ya ujenzi na kufikia Sh. bilioni 32,” alisema Killo.

Waziri Mkuu akahoji tena: “Kutoka Sh. bilioni 13 hadi kufikia Sh. bilioni 32, je, unaona inakuja vizuri hiyo, Sh. bilioni 10 hadi Sh. bilioni 13 tena hadi Sh. bilioni 32 inazungumzikaje hii?”

Na je, mwenye jengo mlikubaliana naye? Awali mwenye mahitaji alisema ana Sh. bilioni 10 sasa imefikaje 32, je, mlimshauri muhusika kuhusu ongezeko hili?”

Killo alipotakiwa kueleza sababu za kuongezeka kwa gharama za ujenzi huo, alisema waligundua tofauti wakati wakiwa kwenye eneo la ujenzi kwamba kuna kazi zilitakiwa zifanyike, lakini katika mkataba hazipo, na hawakuwasiliana na muhusika.

Miongoni mwa vitu vilivyosahaulika katika BOQ ya mradi huo ni pamoja na kutokuwapo kwa ghorofa ya nne katika jengo moja wanalolijenga katika mradi huo ambalo ni la ghorofa nane, pia hapakuwa na paa la jengo la kuhifadhia vifaa mbalimbali vya NEC.

Waziri Mkuu alisema miradi mingi inayojengwa na TBA katika maeneo mbalimbali imeshindwa kukamilika kwa wakati, hivyo alimwagiza Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu), Jenista Mhagama asitishe mkataba huo wa ujenzi na atafutwe mkandarasi mwingine aje amalizie.

“Jengo la Tamisemi lililopo katika mji wa serikali limejengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 1.7, nyie wataalamu gani na kwa nini tuendelee kuwaacha ndani ya taasisi? TBA hamfanyi kazi vizuri wakuu wa mikoa na wilaya wanalalamika majengo hayakamiliki ni serikali gani itakayowavumilia, mmeshindwa kutambua majukumu yenu.”

Waziri Mkuu aliagiza mkandarasi atakayepatikana ahakikishe mradi wa ujenzi huo unakamilika katika kipindi cha miezi sita kuanzia sasa na lijengwe kwa kutumia mfumo wa ‘force account’.

TACECA | CATA | ACCT

COUNCIL OF CONTRACTOR ASSOCIATIONS

TAARIFA KWA UMMA

TAMKO LA BARAZA KUHUSU KUSIKITISHWAWA NA VITENDO VYA KUINGILIA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA UMMA NA KUWAWEKA NDANI KIJINAI MAKANDARASI BILA KUZINGATIA MIKATABA

Baraza la Vyama vya Makandarasi (The Council of Contractor Associations - CCA) linasikitishwa na ongezeko la matukio ya kuingilia utekelezaji wa miradi ya Umma na kuwaweka ndani kijinai makandarasi bila kuzingatia mikataba ya miradi hiyo. Tumesikia katika vyombo vya habari juu ya:

- Uamrishaji wa mabadiliko ya muda wa utekelezaji au mabadiliko mengine bila kuzingatia mikataba iliyoko;
- Utumiaji wa madaraka kutoa maagizo au kuwakamata wakandarasi na kuwaweka ndani kijinai, badala ya kutumia vifungu vya mikataba ya ukandarasi kutatua matatizo yanayojitokeza;
- Kutumia vitisho na kuwadhalilisha makandarasi.

Tunatambua shauku ya viongozi wa Umma kuona miradi inatekelezwa kwa ufanisi na kwa muda mfupi iwezekanavyo.

Hata hivyo tunatambua pia kwamba kazi za ujenzi haziendeshwi kijinai bali utekelezwa kwa kuzingatia mikataba ya kisheria ambayo ikivurugwa, huharibu utekelezaji wa miradi hiyo na pia huharibu mazingira ya kufanya biashara ya ujenzi na sekta ya Umma kwa ujumla.

Tunaiomba Serikali na taasisi zake kuwasihi viongozi wa Umma kuwatumia wasimamizi wataalam (consultants) kutekeleza mambo yote yanayohusu miradi kwakuzingatia mikataba husika.

Baraza na Wakandarasi wote kwa ujumla wataendelea kushirikiana na Serikali kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa ufanisi na kwa muda muafaka na mara zote, kutumia vipengele vya mikataba ya miradi husika kushughulikia migogoro yake.

Mwenyekiti – Tanzania Civil Engineering Contractors Association
Mwenyekiti – Association of Citizen Contractors
Mwenyekiti – Contractors Association of Tanzania

215521802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Wenye ualbino waondolewe hofu uchaguzi mkuu wa 2020

**LIMEKUWA** jambo la kawaida kuwasikia watu wenye ualbino wakielezea hofu ya usalama wao kila mwaka kinapokaribia kipindi cha uchaguzi mkuu.

Hali hiyo ya hofu inatokana na imani za kishirikina miongoni mwa watu katika jamii ambao huamini kuwa viungo vya watu wenye ualbino vinaweza kuwasaidia kupata nafasi za uongozi wa kikiasa ukiwamo udiwani na ubunge.

Imani hizo za kishenzi na zilizopitwa na wakati ndizo zinazowasukuma baadhi ya wanasiasa na wapambe wao kuona kuwa njia pekee ya kushinda uchaguzi ni kuvipata viungo vya watu hao kwa gharama zozote kupitia njia mbili; mosi, kuwaua kabisa na ya pili kuwakata viungo na kuondoka navyo.

Hakika, vitendo vya kuwaua au kuwatoa viungo watu hao licha ya kusababisha hofu wao na kwa jamii nzima, pia vimekuwa vikisababisha nchi yetu kupata sifa mbaya kwa jumuiya ya kimataifa, kwa kuonekana kuwa imekithiri katika ukiukaji wa haki za binadamu.

Sote tunakumbuka matukio mengi ya kuwaondoa viungo na mauaji ya watu wenye ualbino katika maeneo kadhaa nchini yakihusishwa na uchaguzi pamoja na mambo mengine ikiwamo kufanikisha biashara.

Jambo la kushukuru ni kuwa wakati wa uongozi wa serikali ya awamu ya nne, hatua kadhaa zilichukuliwa ikiwamo kuwasaka na kuwafikisha mahakamani watuhumiwa wote kisha mahakama kuwahukumu wote waliokutwa na hatia.

Kwa kiasi kikubwa mpango wa kuiwezesha mahakama kwa bajeti uliisaidia kupanga ratiba maalum kwa majaji kusikilizwa mashauri hayo katika mikoa mbalimbali na kuamuriwa ndani ya muda mfupi. Kwa kweli hatua hiyo ilisababisha kupungua kwa matukio hayo kwa kiwango kikubwa.

Hata hivyo, wakati uchaguzi mkuu ukitarajiwa kufanyika mwakani, baadhi ya watu wenye ualbino wameanza kudai kuwa wameingiwa na hofu ya kuuawa au kutolewa viungo kwa lengo la kukidhi matarajio ya wahusika husussan wanasiasa.

Hofu hiyo ilielezwa na watu hao mkoani Shinyanga kwenye mafunzo ya kuwajengea uwezo watu wenye ualbino pamoja na wazazi ambao wamezaa watoto wa aina hiyo, ili kwenda kutoa elimu kwa jamii kuondoa unyanyapaa dhidi yao.

Katika mafunzo ambayo yalitolewa na Shirika la Under The Same Sun ambalo linatetea haki za watu wenye ualbino nchini, baadhi yao walisema kinapofika kipindi kipindi cha uchaguzi hasa uchaguzi mkuu ndipo mauaji ya watu wenye ualbino huanza kutokea, na kuiomba Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani kuimarisha ulinzi wa usalama wao.

Kilio chao sio cha kupuuzwa kwa kuwa wana uzoefu wa matukio ya kuwadhulu, hivyo cha kufanya ni serikali kuweka utaratibu maalum wa kuwalinda ili wasidhurike.

Kuanzia sasa itakuwa vizuri kuwabana waganga wa kienyeji kuacha kuwadanganya wanasiasa na wapambe wao kuhusu mbinu za kishirikina za kushinda uchaguzi pamoja na kuwataka waache kupiga ramli chonganishi.

Hatua hizo pia ziende sambamba na kuwasaka watu wote ambao wanatuhumiwa kujihusisha na vitendo vya mauaji dhidi ya watu wenye ualbino pamoja na wapambe wao wakati wa uchaguzi.

Jukumu la kuwalinda watu wenye ualbino linapaswa kuwa la kila mmoja wetu badala ya kuiachia serikali pekee. Tunasema hivyo kwa kuwa sisi ndio tunaoishi na wanaofanya vitendo hivyo kwenye vijiji na mitaani. Ifike mahali sasa kuwapo hatua endelevu zitakazokomesha kabisa vitisho na mauaji ya watu wenye ualbino si wakati wa uchaguzi bali muda wote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Elimu kuhusu presha ya macho ni muhimu

Distributed via ippmedia

**TANZANIA** inakadiriwa kuwa na watu milioni 1.7 wenye matatizo ya uoni hafifu,unakosababishwa na changamoto mbalimbali ikiwamo mtoto wa jicho, upeo mdogo wa kuona na presha ya macho.

Takwimu hizo ni kwa mujibu wa Wizara ya Afya. Tena zikiongeza kuwa presha hiyo ni ugonjwa unaotajwa kuathiri zaidi watu wenye umri wa zaidi ya miaka 40 na kwamba asilimia 4.2 ya Watanzania ambao ni takribani watu 440,000 wana tatizo hilo.

Pamoja na kuwapo kwa idadi hiyo ya watu wenye ugonjwa huo, ambao kitaalam unaitwa 'glaucoma', inasemekana asilimia 70 hadi 90 ya watu wenye ugonjwa huo, hawajijui kama wanao, taarifa ya Wizara inaeleza.

Mwaka 2017 ni watu 13,240 tu walikwenda vituo vya tiba kwa tatizo la presha ya macho, idadi ambayo ni ndogo ikilinganishwa na walio katika hatari ya kuwa na ugonjwa huo, ambao hawajagunduliwa.

Ugonjwa huo inaelezwa kuwa ni kati ya kundi la magonjwa ya macho yanayoshambulia mshipa wa fahamu unaopeleka mawasiliano ya uoni katika ubongo ili kutafsiri kile kinachoonekana.

Presha ya macho huathiri mishipa ya fahamu inayohusika na kuona 'optic nerves', na kwamba mgonjwa asipopata matibabu kwa wakati anaweza kupata upofu.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Faustine Ndugulile, anayasema hayo mwaka jana kwenye wiki ya maadhimisho ya utoaji wa elimu kuhusu ugonjwa huo.

Anasema, 'glaucoma' ndiyo inayoongoza kwa idadi ya watu wasioona, na Tanzania inakadiriwa kuwa na watu milioni 1.7 wenye matatizo ya kutokuona vizuri.

Kutoona huko kunasababishwa na matatizo mbalimbali ikiwamo kuwa na mtoto wa jicho, na presha ya macho.

Anaeleza kwamba mtu anaweza kupata upofu taratibu siku hadi siku bila dalili yoyote katika hatua ya awali, na ili kuweza kugundua iwapo mtu anao kuna umuhimu wa kupima macho angalau mara moja kila mwaka.

> **Mwaka 2017 ni watu 13,240 tu walikwenda vituo vya tiba kwa tatizo la presha ya macho, idadi ambayo ni ndogo ikilinganishwa na walio katika hatari ya kuwa na ugonjwa huo, ambao hawajagunduliwa.**

Maelezo ya Naibu Waziri yanatosha kuhamasisha jamii kupata elimu na kujitokeza kwa wingi katika vituo vya afya wapime macho, kuona kama wana ugonjwa huo, ili wapate matibabu haraka kuepuka upofu.

Wito huo wa kupima macho ulirudiwa na mbobezi wa tiba ya macho wa hospitali ya CCBRT ya Dar es Salaam, Dk. Cyprian Ntomoka na kufafanua kuwa siyo kila ugonjwa wa macho ni lazima mtu avae miwani.

Anasema, wapo baadhi ya watu hawapendi kutumia miwani na wanapoumwa macho wanaamini kwamba wakienda hospitali kupima wataambiwa wavae miwani na kumbe sivyo. Ntomoka anasema, presha ya macho inatokana na majimaji yanayozalishwa kubakia zaidi jichoni ikilinganishwa na yale yanayotoka, hivyo wao hufanya kazi ya kuyapunguza kwa kutumia mashine maalum, ili yalingane.

Bingwa huyo anasema, kitaalam macho huwa yana presha ya kiwango kinachoitwa kitaalam 10mmhg hadi 21mmhg, lakini kinapozidi hapo, mtu hutambuliwa kuwa ni mgonjwa wa presha ya macho.

Msisitizo wake ni watu kupata elimu kuhusu ugonjwa huo na pia jamii kuwa na mazoea ya kupima macho, ili wale wenye umri wa miaka 30 wapime angalau mara moja kwa mwaka, lakini wa zaidi ya umri huo, upimaji wa macho ni wa lazima.

Hivyo ni muhimu watu kuchukua hatua mapema za kupima afya ya macho kuliko kusubiri kupata madhara wakati uwezekano wa kuyaepuka upo.

Wataalam wa afya wameshaweka wazi kwamba siyo kila tatizo la macho ni lazima mtu avae miwani, bali yapo mengine ambayo ni kutibiwa tu, kwa hiyo ni muhimu kupima ili kujua chanzo.

Macho ni miongoni mwa milango mitano ya fahamu inayowezesha kujua mazingira, kutambua mambo mbalimbali.

Milango ya fahamu yakiwamo macho, ni muhimu kwa binadamu, kutokana na kwamba yanaona na kufanya shughuli zake za kila siku kwa uhakika, hivyo ni vyema kuyapima kila inapowezekana.

## BARUA / MJADALA

# Chakula cha mifugo chini kuna sumukuvu?

**MHARIRI** *naomba maelezo ya mamlaka za afya na dawa kuhusu tatizo hili.*

*Mara nyingi tumekumbushwa kuanika vyakula kama mahindi na ulezi kwenye vichanja. Ili kujiepusha na sumu kuvu. Lakini mbona tunaanika pumba na vyakula vya mifugo chini?*

*Mamlaka za chakula zituambie na zihamasishe wananchi kujiepusha na kuanika vyakula vya mifugo kama pumba kwa kuwa kuku, ng'ombe wakila nasi tunapowala tunakula sumukuvu pia au ninakosea?*

*Lakini si hivyo tu, nadhani pia tunahitaji elimu zaidi kuhusu sumukuvu kwa vile hata wanyama wetu tunawapa chakula kwa kukirusha ardhini.*

*Hivi hili nalo litatunusuru na sumu kuvu? Ninauliza kwa sababu kuku wanakula chakula kinachowekwa ardhini na hata kama tumewawekea kwenye mabeseni kikidondoka chini wanakula bila kujua kuwa wanaathirika na sisi watatudhuru pia tutakapowala.*

***Muharami Kaju***
***Box 157***
***Kilimanjaro.***

# Tunaomba serikali ilete viuatilifu asilia

***Mhariri***

*MWAKA huu mvua za vuli zimewahi na wakulima wengi mijini na vijijini wamelima hasa mahindi na kunde kwa wakazi wa Dar es Salaam.*

*Lakini kinachonituma kuandika waraka huu kwa Mhariri ni wimbi la viuatilifu hasa wadudu jamii ya funza wanaotafuna mahindi.*

*Kila mahali tunapopita tunakutana na mahindi yaliyoshambuliwa na kuharibiwa sana na wadudu na kujiuliza hivi mbegu hizo zina matatizo gani mbona zinashambuliwa sana na wadudu?*

*Hali hiyo inatulazimisha kusaka viuatilifu ambayo ni sumu ya kuua, kuangamiza, kufukuza, au kuzuia visumbufu katika mimea.*

*Japo mvua imenyesha visumbufu vya mimea ni vingi kuna wadudu, kuvu au fungasi ambazo huharibu mahindi na mazao mengine mengi shambani.*

*Kinachojiri wakati huu ni kuona watu wakipulizia au kunyunyiza viatilifu mashambani na kwenye mboga . Unyunyiziaji wa viuatilifu unasababisha mchanganyiko wa sumu kusambaa sehemu kubwa na hata kuingia majini na hata chini ya ardhi na kusababisha athari kwa mazingira.*

***Tunaomba kuwe na viuatilifu asilia.***

***Manda Madeni***
***Dar es Salaam.***



Mazao ya bahari kama vikonyo hivi ni miongoni mwa samaki wanaolalamikiwa na wavuvi kuwa leseni zao zinatozwa pesa nyingi. **PICHA: MTANDAO.**

# Wavuvi hawa wanabeba kiroba cha tozo, leseni

**Na Mwandishi Wetu**

HIVI karibuni gazeti hili lilikutana na wavuvi wadogo wa kisiwa cha Mafia kilichoko mkoani Pwani, ambao bila kusita walipoiona Nipashe walituma ujumbe kwa serikali wakisema, wanaumizwa na kodi na tozo nyingi zinazowakwamisha kutoka kimaendeleo.

Wavuvi hao kutoka Ushirika wa Wavuvi wa Twendekazi , katika Kijiji cha Miburani, wanasema wanalipia leseni nyingi kuanzia ya kusajili na kumiliki chombo cha mvuvi hadi ya aina mbalimbali ya samaki wanazovua, wanazoomba zipunguzwe.

Wana Twendekazi, wanatoa kilio chao wakati wa ziara ya wanahabari katika kisiwa hicho iliyoandaliwa na Shirika la ActionAid, ambalo limewaunganisha na kuwapa mafunzo ya ujasiriamali, boti, injini na nyavu kwa ajili ya kuvua kisasa na kujiongezea mapato.

Katibu wa ushirika, Twaha Ismail, anataja baadhi ya leseni hizo kuwa ni ya mvuvi ambayo ni Sh. 25,000 (karibu dola 10).

"ActionAid imetupatia boti ya kisasa yenye thamani ya takribani milioni 24 na kutuwezesha kusafiri umbali mrefu kwa haraka kuvua pweza kwa wingi, lakini tozo na leseni ni nyingi , zinaturudisha nyuma tunaomba serikali itufikirie." Anaeleza Twaha.

Anapozungumza wakati wa mkutano huo uliofanyika kwenye kambi ya wavuvi ya Kitoni, kijijini Miburani, anawaambia wanahabari na maofisa wa ActionAid kuwa mvuvi hulipia leseni kila mwaka, lakini aina ya samaki anazovua nazo pia hulipiwa kila mwaka.

Anasema Twendekazi wanalipia leseni ya mvuvi kila mmoja 25,000 ya ngisi na pweza ambayo ni Sh.16,500, leseni ya chombo na zote hulipiwa kila mwaka, lakini pia mvuvi akivua samaki wengine wenye mapezi na wasio nayo kama vikonyo hulipia leseni zake.

Distributed via ipmedia

Aidha, anasema ukivua kamba na lobsta unalipia leseni ambayo ni takribani Shilingi 40,000 mambo yanayofanyika Mafia pekee na kwamba utitiri wa leseni hizo haupo Dar es Salaam, Tanga, Lindi au Mtwara.

Wanachama hao wanataka angalau kulipa kodi au leseni mbili si utitiri wanaousema. Wanadai , hawaoni kama kuna tija kwa vile halmashauri haiwaendelezi na kuwafanikisha kwenye ushirika wa kuwaletea maendeleo.

Wavuvi hao wanasema ActionAid imewawezesha kupata samaki zaidi kwani badala ya kuvua mtu mmoja mmoja, wana kikundi ambacho kinakusanya taribani kilo 70 za pweza kila siku.

Wamenunua kiwanja na kujenga ofisi na wanatarajia kuanza kuchakata na kuhifadhi samaki, lakini uwepo wa kodi nyingi unawafanya watembee mwendo wa kinyonga.

Mvuvi na mwanachama wa ushirika Selemani Masoud, anasema licha ya kwamba uvuvi ni uti wa mgongo wa kisiwa cha Mafia, halmashauri imewasahau na hawapati msaada hasa mafunzo kutoka kwake.

Anaeleza kuwa mara nyingi wanasaidiwa na asasi za kirai, lakini ushirika huo unaombwa mara kwa mara kuchangia fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo lakini Idara ya Uvuvi , Wilaya hawakumbuki kimafunzo wala kiuwezeshaji.

Wanalilia ukosefu wa kiwanda cha kuchakata samaki Mafia, wakituma ujumbe kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuwa ndani ya Ziwa Victoria kuna viwanda zaidi ya 40 vya kuchakata samaki vipi Mafia?

Wanalalamika kuwa kukosekana kwa wawekezaji kisiwani hapo kunadumaza sekta ya uvuvi kwani hakuna ushindani na upangaji wa bei za samaki huwaumiza wavuvi.

Ofisa Uvuvi wa Wilaya, Ayoub Sabu , anasema kuna wavuvi 5,133 na vyombo takribani 1,000 vya kisasa na vya kienyeji vinavyovua kwenye ukanda huo.

Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya ,Eric Mapunda , licha ya kukubali kuwa kuna mlolongo wa leseni, anapojibu malalamiko, anawaambia wavuvi hao kuwa leseni zote zimeandaliwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozi ya nchi.

Anakiri kuwa suala la leseni ya uvuvi ambayo ilikuwa inatolewa kila eneo la uvuvi mfano Dar , Mwanza na Tanga, limetatuliwa na kwamba kuanzia mwaka huu, leseni ya uvuvi ni ya kitaifa ukishaikata popote unaweza kuvua.

"Sheria za kupanga leseni kwa kila aina ya samaki ni utaratibu wa nchi, ukivua changu ana leseni, kamba , pweza na lobsta pia... lakini wanaweza kufikisha kilio chao serikalini . Kila jambo linazungumzika." Anashauri Mapunda.

Anasisitiza kuwa uvuvi ndicho chanzo kikuu cha mapato Mafia, hivyo tozo kwa aina za samaki, zana za uvuvi na leseni ni lazima zitumike kisheria, kuzifuatilia wanaovua, mapato na kulinda rasilimali bahari.

Hata hivyo, pamoja na maelezo hayo suala la kumaliza utitiri huo wa kodi ni lazima lijibiwe. Kama serikali iliondoa kodi sumbufu kwa wakulima iwakumbuke pia wavuvi wakiwamo wa Mafia. Iangalie na uwezekano wa kupata wawekezaji kwenye viwanda maana kilio chao pia ni kukosa mwekezaji wa kuongezea thamani samaki wanazovua.

**KABWELA** NA FADHILI MOHAMMED



# Pengo amtabiria makubwa Makonda

INATOKA UK 2

Kituo hicho kinatarajiwa kukusanya majitaka kutoka maeneo ya Kariakoo, Upanga, Posta na mitaa mingine ya katikati ya jiji hilo.

Katika mkutano huo, Makonda aliwaomba viongozi wa dini kuwakumbusha waumini wao kuwaheshimu watu walioapa kulinda nchi na usalama wao.

Alisema Jeshi la Polisi na majeshi mengine yanafanya kazi kubwa kuhakikisha mkoa unakuwa na amani huku ulinzi na usalama vikitawala.

"Kulikuwa na ujambazi zamani, watu walikuwa wanauawa ovyo, wakati mwingine hata polisi walikuwa wanashambuliwa, lakini sasa kazi kubwa imefanyika, kuna utulivu, hakuna panya roads wala wizi wa vifaa vya magari," alisema.

"Mikakati mingi iliwekwa na (Lazaro) Mambosasa (Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam) na wenzake na matokeo tunayaona jiji la Dar sasa ni shwari," Makonda alitamba.

# PM amweka kikaangoni bosi Bodi ya Korosho

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemwagiza Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Julius Mtatiro, ahakikishe anaondoka na Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho hadi Tunduru ili wakahakiki ni kwanini wakulima hawajalipwa.

"Nimefurahi kusikia minada ya korosho inakwenda vizuri. Lakini sijafurahia habari ya Tunduru. Mheshimiwa Rais aligiza Sh. milioni 40 zipelekwe kwa wakulima. Na ninajua kwamba zimeshalipwa. Sasa ni kwanini wakulima bado wanadai?" Alihoji.

"Ukitoka hapa kwenye mkutano nenda pale jengo la Bodi ya Korosho. Ondoka na Mtendaji Mkuu wake, mwende Tunduru akafuatilie ni kwanini malipo ya mwaka jana hayajalipwa hadi sasa." Mtatiro ni Mkuu wa Wilaya ya Tunduru.

"Nataka afuatilie fedha zimekwama kwa nani. Kaimu Mkuu wa Mkoa ukigundua wanaokwamisha ni viongozi wa ushirika, shughulika nao hukohuko kama ambavyo umekuwa ukifanya," alisisitiza.

Alitoa agizo hilo jana wakati akifungua kongamano la siku moja la makandarasi na wazabuni wa mikoa ya Kusini liloandaliwa na benki ya CRBD.

Akizungumzia kuhusu kongamano hilo ambalo kaulimbiu yake ni "Pamoja nawe kukuza uchumi," Waziri Mkuu aliwataka makandarasi hao baada ya kupata elimu kidogo kuhusu shughuli za benki hiyo, anatarajia kuwa wataenda kwenye halmashauri zao na kutafuta.

"Serikali inajenga miradi mikubwa kama vile bwawa la kuzalisha umeme kwa nguvu ya maji la Mwalimu Nyerere, bomba la mafuta la kutoka Hoima hadi Tanga na miradi ya maendeleo kama ile ya barabara, reli, ujenzi wa hospitali, madarasa na nyumba za walimu. Miradi yote hii inawatarajia ninyi makandarasi wadogo na wa kati."

Alisema serikali imeendelea kuimarisha na kusogeza karibu kwa wananchi huduma za jamii ikiwamo ukarabati wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu. "Katika kipindi cha Januari hadi Juni 2019, kwa shule za msingi, serikali imejenga madarasa 473, matundu ya vyoo 1,405, nyumba za walimu 24 na kukamilisha maboma ya madarasa 2,760. Kwa shule za sekondari, serikali ilijenga madarasa 465, matundu ya vyoo 736, nyumba za walimu 23 na kukamilisha maboma ya madarasa 2,392.

Alitoa wito kwa viongozi na watendaji wazingatie utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma kwa kutenga zabuni zenye thamani ya chini ya Sh. bilioni 10 kwa ajili ya wazabuni Watanzania ili kuwajengea uwezo na kushiriki katika zabuni. Alisema serikali kwa upande wake itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Alimpongeza Mkurugenzi Mkuu wa CRDB kwa kubuni programu hiyo ya tofauti ambayo imelenga kuwainua makandarasi wadogo na wa kati.

Mapema, akimkaribisha Waziri Mkuu kuzungumza na washiriki wa kongamano hilo, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, alisema hadi sasa jumla ya tani 67,000 za korosho zimeuzwa mkoani humo kupitia minada mitatu.

# Anyongwa kwa kamba ya viatu

INATOKA UK 2

mzazi wa mtoto aje na mwanazengo mmoja twende kituo cha polisi tutoe taarifa halafu tuongeze jitahada za kutafuta tukishirikiana na Jeshi la Polisi.

Saa 11 jioni walikuja tukaenda polisi, mwenyekiti wa kijiji na baba mtoto kwa mawazo ya haraka haraka ikabidi wakimbie machinjioni kwamba labda wale mbuzi wamepelekwa machinjioni kwenda kuuzwa.

"Tukiwa barabarani kwenda eneo ulipopatikana mwili wa mtoto, tulipata simu kuwa kuna watu wawili wamekutana na wapeleka maziwa Kanyama kwenye mteremko wanaswaga kundi la mbuzi na kondoo wanakimbia sana, pale pale ikabidi tufanye mawasiliano na askari kufuatilia lakini hatukufanikiwa," alisema Balele.

Balele alisema baada ya kuchukua mwili wa mtoto, waliupeleka kituo cha afya Kisesa ambako uchunguzi wa daktari ulionyesha kuwa mtoto alinyongwa kwa kutumia kamba ya viatu.

"Alinyongwa kabisa yaani koromeo lote lilikuwa limekatwa halafu sehemu ya uso hapa alikuwa amepigwa na kitu kizito alikuwa na majeraha damu zinavuja ndicho kitu kilichosababisha mtoto kufa," alisema.

Balele alisema jitihada zinazofanyika sasa ni kuwatafuta hao wahalifu waliofanya tukio la kinyama na kuchukua mifugo.

Diwani wa Bukandwe, Marco Minzi, akitoa neno katika mazishi ya mtoto huyo yaliyofanyika nyumbani kwa wazazi wake, aliwaomba wananchi kutoa ushirikiano kwa polisi ili kubaini waliofanya tukio hilo.

"Ndugu zangu haiwezekani mtu mgeni kutoka mbali akaja akafanya tukio kama hili bila mwenyeji. Haiwezekani hata siku moja, kama ni mtu ametoka Tarime au ametoka Shinyanga kuja kufanya tukio kama hili, alijuaje kuwa hao mbuzi anachunga mtoto mdogo na kaenda sehemu fulani. Lazima tuumie, tukiumia tukapata ujasiri wa kuwabaini watu waliofanya hivi," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Jumanne Muliro, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba taarifa hizo ziko kwenye mtandao wa kijamii wa polisi.


Distributed via

Mratibu wa mradi wa kuwajengea uwezo watu wenye ualbino wakiwamo wanawake ambao wamezaa watoto wenye ualbino kutoka Shirika la Under The Same Sun, Grace Wabanu, akitoa elimu kuhusu jamii kuacha kuwafanyia unyanyapaa, mkoani Shinyanga jana. **HAHARI UK. 24 PICHA: MARCO MADUHU**

# Mkapa ashtushwa na kasi ongezeko la watu

INATOKA UK 2

la Sahara na mawili ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Orodha ya mataifa hayo kwa nafasi zake nyuma ya India ni Nigeria, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Pakistan, Ethiopia; Tanzania; Marekani; Uganda na Indonesia.

Vilevile, ripoti inasema wakazi wa dunia wataongezeka kutoka bilioni 7.6 wa mwaka 2016 hadi bilioni 8.6 ifikapo mwaka 2030 ambao ni ukomo wa kipindi cha Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG).

**SENSA TANZANIA**

| Mwaka | Idadi ya watu | Tanzania Bara | Zanzibar |
|---|---|---|---|
| 1967 | 12,313,469 | 11,958,654 | 354,815 |
| 1978 | 17,512,610 | 17,512,610 | 476,111 |
| 1988 | 23,095,878 | 22,455,193 | 640,685 |
| 2002 | 34,569,232 | 33,584,607 | 984,625 |
| 2012 | 44,928,923 | 43,625,354 | 1,303,569 |

**Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)**

## Wajasiriamali wafunguliwa fursa China

**Na Beatrice Philemon**

ZIARA ya wajasiriamali waliokwenda China kujifunza teknolojia za aina mbalimbali na kutembelea viwanda, imezaa matunda baada ya kuingia mikataba ya makubaliano ya kuagiza mashine kutoka kwenye kampuni za China na kwa bei nafuu kuleta Tanzania.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi inayojishughulisha na masuala ya kuwawezesha wanawake na vijana kibiashara (TABWA), Moreen Mawala, ambaye aliambatana na wajasiriamali 18 kwenda China kujifunza teknolojia za kisasa zitakazowawezesha kuzalisha bidhaa zenye ubora nchini na kusaidia wajasiriamali kushindana katika masoko ya kimataifa na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Makubaliano hayo yalipatikana kupitia mkutano wa kibiashara uliofanyika kati ya wajasiriamali wa Tanzania na wafanyabiashara wa China.

Wajasiriamali wanaojihusisha na biashara ya urembo walipata fursa ya kukutana na wadau wa urembo na kwamba watawawezesha kurudi China Machi mwakani kwa ajili ya kuwapa mafunzo maalum ya urembo.

Alisema pia safari hiyo imekuwa na mafanikio makubwa kwani wameweza kuwashawishi wafanyabiashara na watu wengine kutoka China kuja Tanzania kujionea fursa za uwekezaji na kufanya utalii jambo ambalo litaiingizia nchi fedha za kigeni.

Mawala alisema kadhalika, taasisi hiyo iliwawezesha wajasiriamali hao 18 kwenda China kwenye maonyesho makubwa ya dunia ya biashara ya Canton Fair, ambapo wameweza kukutana na wazalishaji wa bidhaa za viwandani zikiwamo mashine za kusindika mazao na mashine za kusafishia maji.

Baadhi ya wafanyabiashara wameishukuru Taasisi ya Tabwa kwa kuwawezesha kuwatafutia fursa za kibiashara, ambapo mhandisi wa mitambo na mashine, Elvis Valentine, alisema wameweza kukutana na watengenezaji wa bidhaa hizo kutoka katika kampuni zao.

Maonyesho ya Canton ni maonyesho makubwa ya kimataifa yanayofanyika mara mbili kila mwaka Aprili na Oktoba katika jiji la kibiashara la Gounzouh yakiwa na lengo la kutoa fursa kwa wafanyabiashara kutoka duniani kujifunza na kununua bidhaa zikiwamo mashine.

**Alisema pia safari hiyo imekuwa na mafanikio makubwa kwani wameweza kuwashawishi wafanyabiashara na watu wengine kutoka China kuja Tanzania kujionea fursa za uwekezaji na kufanya utalii jambo ambalo litaiingizia nchi fedha za kigeni.**

# CCM yajivunia wagombea kujaza fomu kwa umakini

**Na Hamisi Nasiri, MASASI**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mtwara, kimewataka wananchi mkoani humo kuwa ifikapo Novembe 24, siku ya kupiga kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa wachague viongozi ambao ni sahihi kwenye maeneo yao ili kuwaletea maendeleo.

Wito huo ulitolewa jana wilayani Masasi na Katibu wa CCM Mkoa wa Mtwara, Alhaji Saidi Kusilawe, alipokuwa akihutubia mamia ya wanachama wa chama hicho kwenye sherehe za uzinduzi wa kampeni za uchaguzi huo.

Uzinduzi huo kwa ngazi ya Wilaya ya Masani ulifanyika Jimbo la Ndanda katika Kata ya Ndanda Mjini Masasi.

Alisema CCM mkoa inawapongeza wagombea wake wote katika mkoa wa Mtwara kwa kujitokeza kugombea ikiwamo kujaza fomu za kugombea kwa umakini na ufanisi.

Kusilawe alisema hatua ya wagombea hao kujaza fomu kwa umakini wa hali ya juu ni ishara tosha kuwa CCM imeteua wagombea wenye uwezo mkubwa.

Alisema uwezo huo waliouonyesha katika kujaza fomu kwa umakini kunaashiria kuwa pia iwapo watachaguliwa, basi wataionyesha katika kuwaletea maendeleo wananchi wao.

Kusilawe alisema Jumapili ambayo ni siku ya uchaguzi wananchi ndio watakaobeba dhamana ya kupiga kura na kuchagua viongozi kwenye maeneo yao na kwamba lazima wachague viongozi bora.

"CCM mkoa wa Mtwara inawataka wananchi kuchagua viongozi wenye uwezo wa kuleta maendeleo ili kila eneo baada ya uchaguzi tuone maendeleo yanapatikana kwa haraka," alisema Kusilawe.

Alisema wananchi wanapaswa kufahamu kuwa uchaguzi unagusa maisha ya binadamu, hivyo wasikubali kuacha kwenda kupiga kura kwani ni haki yao ya msingi ya kikatiba.

Naye Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Masasi, Edward Mmavele, alisema lengo la chama hicho kuzindua kampeni zake Ndanda, ni kutaka kuleta mageuzi Ndanda igeuke kuwa ya kijamii.

Alisema miradi mingi ya maendeleo imekuwa ikikwama katika Jimbo la Ndanda, kutokana na wananchi kuchagua mbunge wa upinzani na diwani wa upinzani wote kutoka Chadema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya TPB, Sabasaba Moshingi (katikati), akikabidhi moja kati ya meza 100 na viti 100 vyenye thamani ya Sh. milioni 4.8 kwa Mkuu wa Wilaya ya Mbinga, Cosmas Nshenye, kwa ajili ya shule mbili za Sekondari za Mbambi na Makita, zilizopo Halmashauri ya Mji wa Mbinga, mkoani Ruvuma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sababu Shinyanga kinara uharibifu miundombinu

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WANANCHI wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wametakiwa kuacha tabia ya kukata nyaya zilizoshikilia nguzo za nishati ya umeme kwa ajili ya kutengenezea mikokoteni ya kuvuti ng'ombe kwa kuwa kufanya hivyo ni kuihujumu miundombinu ya umeme.

Meneja Masoko wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) makao makuu, Mussa Chowo, aliyabainisha hayo wakati akizungumza na madiwani wa Halmashauri ya Ushetu, katika kikao cha Baraza la Madiwani, na kueleza kuwa serikali imekuwa ikipeleka huduma ya nishati ya umeme vijijini, lakini wengine wamekuwa wakiharibu miundombinu hiyo.

Alisema Mkoa wa Shinyanga unaongoza kwa uharibifu wa miundombinu ya nishati ya umeme ukilinganisha na mikoa mingine kwa kukata nyaya zinazoshikilia nguzo ya umeme na kwenda kutengenezea mikokoteni kwa ajili ya kukokota ng'ombe na punda.

Pia alisema wamekuwa wakichoma takataka jirani na nguzo hizo hasa wakati wa maandalizi ya kilimo kutokana na asilimia kubwa ya nguzo za umeme kupita porini na katikati ya mashamba ya wananchi.

"Shinyanga mnaongoza kwa uharibifu wa miundombinu ya umeme, mmekuwa mkikata nyaya zinazoshikilia nguzo za umeme na kwenda kutengenezea mikokoteni ambayo inavutwa na ng'ombe na punda...tena mnachoma nyasi jirani na nguzo jambo ambalo ni hatari," alisema Chowo.

# Wanufaika Tasaf watafutiwa masoko

**Na Elizabeth Zaya, MAKETE**

HALMASHAURI ya Makete imeanza mchakato wa kuwasaidia walengwa wa mpango wa kunusuru kaya maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) wanaojishughulisha na kilimo cha viazi kuwatafutia masoko ya kudumu.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Francis Namaumbo, alisema walengwa hao kwa sasa bado hawapati faida kutokana na bei ya viazi kuwa chini na kukosa soko la kudumu.

"Tunawapongeza sana Tasaf wamefanya kazi kubwa katika halmashauri yetu hii, tumeona badala ya kuwasaidia hela ya kujikimu, lakini wamewawezesha pia kuanzisha miradi mbalimbali, kwa mfano hapa kwetu wanajishughulisha na kilimo cha umwagiliaji," alisema Namaumbo na kuongeza:

"Wanalima sana viazi, tatizo kubwa lililopo hawana masoko kwa kuuzia, kwa hiyo wakati mwingine hawapati faida inayokuwa imetarajiwa, na ndiyo maana tunachojipanga kwa ajili ya kuwasaidia kuwatafutia au kuwaunganisha na fursa za masoko kwa kushirikiana na wadau mbalimbali."

Jambo jingine ambalo wanapambana kwa ajili ya kuwasaidia walengwa hao kunufaika na kilimo hicho alisema ni kukomesha tabia ya wanunuzi ambao wamekuwa wakiwanyonya kwa kutumia magunia ya lumbesa pamoja na kuangalia namna ya kuwawekea wanunuzi bei elekezi ambayo itakuwa rafiki kwa pande zote mbili.

"Tumeona kwamba hata hili suala la kuweka bei elekezi ni muhimu sana kwa sababu mpaka sasa gunia moja la viazi limeshuka hadi kufikia Sh.10,000 hii inakuwa inawaumiza na kama tunavyojua wafanyabiashara ni wajanja sana, pamoja na hiyo bei ya chini lakini unakuta wanaweka kwenye magunia ya lumbesa," alisema Namaumbo.

Alisema katika halmashauri hiyo, wametekeleza miradi ya Tasaf 39 ikiwamo ya kujiongezea kipato ambayo wananchi wanaiibua wenyewe, miradi ya kukuza uchumi na miradi ya ujenzi.

Pia alisema jumla ya wanafunzi 3,378 wanahudumiwa na mfuko huo, huku watoto 387 wakisaidiwa kupata matibabu.

**"Tumeona kwamba hata hili suala la kuweka bei elekezi ni muhimu sana kwa sababu mpaka sasa gunia moja la viazi limeshuka hadi kufikia Sh.10,000 hii inakuwa inawaumiza na kama tunavyojua wafanyabiashara ni wajanja sana, pamoja na hiyo bei ya chini lakini unakuta wanaweka kwenye magunia ya lumbesa," alisema Namaumbo.**

# Kigogo wa ZSTC kizimbani tuhuma kudhalilisha mtoto

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

MTENDAJI Mkuu Shirika la Biashara la Taifa la Zanzibar (ZSTC') Wilaya ya Mkoani, Seif Suleiman Kassim, mkazi wa Jiondeni Mkoani, amefikishwa katika Mahakama ya Mkoa 'A' Chakechake Pemba, akituhumiwa kwa makosa mawili, likiwamo la utoroshaji na ubakaji wa mtoto wa miaka 13.

Mwendesha Mashtaka kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Juma Mussa Omar, alimsomea tuhuma hizo, lakini alikana.

Hata hivyo hakimu wa mahakama hiyo, Abdul-razak Abdul-kdir Ali, alimpa dhamana kwa kosa la kwanza la utoroshaji na kumpeleka mahabusu hadi Novemba 21, mwaka huu kwa kosa la ubakaji ambalo halina dhamana.

Awali mwendesha mashtaka huyo, akiongozana na wakili mwenzake, Mohamed Ali Juama, alidai kuwa kosa la kwanza linalomkabilia mtuhumiwa huyo ni la utoroshaji.

Alidai siku na tarahe isiofahamika Aprili mwaka 2019, majira ya mchana eneo la Bandarini mkoani Pemba, bila ya halali na bila ya ridhaa ya wazazi wake, alimtorosha mtoto huyo (jina linahifadhiwa).

Alidai mtuhumiwa huyo alimtorosha mtoto huyo ambae ni mwanafunzi, alipokuwa anakwenda shuleni, kisha kumwingiza kwenye ofisi anayofanya kazi ya ZSCT Mkoani.

"Ulifanya kitendo hicho, wewe mtuhumiwa cha kumtorosha mtoto huyo, jambo ambalo ni kosa, kinyume cha kifungu cha 113 (1) (a) Sheria ya Adhabu namba 6 ya mwaka 2018," alidai.

Kosa la pili linalomkabili mtuhumiwa huyo ni la ubakaji kwa mtoto huyo huyo, ambapo kufanya hivyo ni kosa pia kinyume na kifungu cha 108 (1), (2) (e) na kifungu cha 109 (1) cha Sheria ya Adhabu namba 6 ya mwaka 2018, Sheria ya Zanzibar.

Kosa hilo, alituhumiwa pia kulifanya mwezi huo wa Aprili mwaka huu, majira ya saa 6:15 mchana ndani ya ofisi ya ZSTC zilizopo Bandarini, Wilaya ya Mkoani.

Baada ya mtuhumiwa huyo ambaye alikuwa akiongozwa na wakili wake, Abeid, alikana tuhuma hizo, na wakili wa mtuhumiwa, aliiomba mahakama hiyo kulipanga shauri hilo muda mfupi ujao.

"Muheshimiwa, naelewa kuwa kosa la pili la ubakaji halina dhamana, lakini kwa hili la pili la utoroshaji, naiomba mahakama yako, impe dhamana mteja wangu, na kisha kupanga tarehe ya karibu," aliomba.

Hakimu alilipanga kurudi tena mahakamani shauri hilo, Novemba 21, mwaka huu, huku mtuhumiwa akipelekwa rumande.

Kwa kosa la utoroshaji, mtuhumiwa huyo ametakiwa kuandikisha Sh. milioni 2 na mdhamini mmoja kwa kiwango kama hicho, na akitimiza masharti hayo atakuwa na dhamana.



Fahad Fuad, ambaye ni mwanzilishi wa Kampuni ya Unzip Tanzania inayolenga kukuza utalii wa ndani nchini, akiwajibika katika moja ya vivutio vya utalii nchini. **MPIGAPICHA WETU**

# Kigwangalla ataka vijana kuchangamkia fursa utalii

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, ameeleza kushangazwa na juhudi binafsi za kijana Fahad Fuad katika kutangaza utalii wa ndani na kutoa wito kwa vijana kuiga mfano huo kwa kuwa soko la sekta ya utalii limezidi kukua.

Dk. Kigwangalla ambaye hivi karibuni aliandaa kampeni ya 'Twenzetu kileleni' alisema Fuad ambaye ni mwanzilishi wa kampuni ya Unzip Tanzania amekuwa kinara katika kuhamasisha Watanzania kutembelea vivutio vya utalii vilivyo nchini.

Alisema sekta ya utalii ambayo sasa inaongoza kwa kuingiza fedha za kigeni kwa asilimia 25 ya fedha zote na kuchangia asilimia 17 ya pato la Taifa, inazidi kukua, hivyo ni muda mwafaka kwa vijana kuwekeza zaidi katika sekta hiyo nchini.

"Hii comment (maoni) imenifanya niandike ili kutambua 'passion' yake na wenzake, kabla hatujajuana na kufanya kazi pamoja nisingejua uwezo na passion yake, vilevile na yeye asingejua passion yangu na tabia zangu, hakika ni kijana aliyejitoa kindakindaki kutangaza utalii," aliandika Kigwangalla katika ukurasa wake wa Twitter na Instagram.

Akizungumza na gazeti hili , Fuad alisema tangu aanze kuwasafirisha Watanzania katika vivutio mbalimbali vya utalii, hadi sasa amewatembeza zaidi ya watalii 620.

"Kila kitu ni malengo kwa sababu nilianza kazi ya kupiga picha katika sherehe kama harusi, sendoff na birthday, lakini baada nilikodiwa kama kibarua na kampuni moja ya utalii kwenda kupiga picha za utalii mbugani Mikumi Morogoro.

"Huo ndio ulikuwa mwanzo wangu mpya kwani licha ya kuwa na taaluma ofisa mahusiano kwa umma, sasa nimejiajiri na sasa naifanya kazi hii kwa furaha na uhuru.

"Kwa hiyo lengo langu ni kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini na kuhamasisha Watanzania kutembelea vivutio hivyo hasa vile ambavyo hawavifahamu sana," alisema.

Alisema kwa kupitia mitandao yake ya kijamii ambayo ana wafuasi zaidi ya 80,000 hutumia kurasa zake kuweka picha na kutangaza vivutio hivyo jambo ambalo limeonekana kuhamasisha watu wengi kutembelea.

Aidha, Fahad alisema ndoto yake ilikuwa kutembelea vivutio vyote vilivyopo nchini ikiwamo Mlima Kilimanjaro kwa sababu hakua ameutembelea mlima huo kutokana na sababu za kiafya na kiuchumi.

"Kwa hiyo Waziri Kigwangalla alipoanzisha kampeni ya 'Twenzetu kileleni' niliona huu ndio muda muafaka wa kushiriki. Kwa bahati nzuri nilipata fursa ya kuwa moja ya watu niliochaguliwa kushiriki kampeni hiyo.

"Nilifurahi sana kwa sababu kwanza napanda mlima na waziri, pili kupanda Mlima Kilimanjaro ni ndoto yangu ya siku nyingi na tatu nimefanikiwa kutambulisha kazi yangu licha ya kufanya kazi kwa miaka mitatu bila ya kutambuliwa na waziri mwenye mamlaka husika," alisema.

0000

## CCM yaridhishwa utekelezaji wa Ilani

**Na Allan Isack, ARUSHA**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimesema kimeridhishwa na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Mkoa wa Arusha kwa zaidi ya asilimia 90.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kutoa tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2015 hadi 2019, Katibu Mwenezi wa CCM, Humphrey Polepole, alisema chama hicho kimeridhishwa na utekelezaji wa ilani kwa kipindi cha miaka minne.

Polepole alisema hayo jana katika kikao kazi cha siku mbili kilichofanyika mkoani hapa, alisema chama hicho kimefanya mambo makubwa ndani ya mkoa wa Arusha.

Alisema wakati chama kikifanya tathmini ya utekelezaji wa ilani, waliangalia zaidi utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta za afya, maji, elimu, mifugo, kilimo na ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Alisema mtaji mkubwa wa chama hicho kuelekea katika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ni kuisimamia serikali kutekeleza miradi ya maendeleo kwa vitendo na si maneno ya propaganda.

"Kazi ya chama ni kuisimamia serikali, kutoa maoni kwa serikali, kutoa maelekezo kwa serikali na hadi sasa maelekezo hayo yamefanyiwa kazi kwa zaidi ya asilimia 90," alisema Polepole.

Kuhusu baadhi ya vyama vya siasa kujitoa kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, Polepole alisema si kweli kwamba vimejitoa bali vimeona wananchi hawawezi kuvichagua kutokana na maendeleo yaliyofanywa na serikali kwa kipindi cha miaka minne.

"Vipo vyama vya siasa vinasema vimejitoa kwenye uchaguzi wakati hawana hata wanachama. Ukiangalia kwa Mkoa wa Arusha, vyama vilivyosema vimejitoa wagombea waliochukua fomu na kuzirudisha ni wachache mno na waliopitishwa kwa mujibu wa kanuni, sheria na taratibu hawazidi 10," alisema.

Polepole alisema chama hicho, katika uchaguzi wa serikali za mitaa kwenye vijiji na vitongoji, kimepita bila kupingwa kwenye baadhi ya maeneo ambayo uchaguzi utafanyika wamejipanga kushinda.

Alisema kwenye maeneo ambayo uchaguzi wa serikali za mitaa utafanyika watakwenda kuwaeleza wananchi mambo yaliyofanywa na serikali kwa kipindi cha miaka minne tangu kuingia madarakani.

Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, Mkoa wa Arusha ulifanya vibaya kwa kutoa kura nyingi kwa vyama vya upinzani, lakini bado serikali iliendelea kuwajali wananchi kwa kupelekea miradi mikubwa ya maendeleo, hivyo taswira ya awali imebadilika na wamekubali kuiunga mkono serikali.

# AG ataka mitaala ilenge soko la ajira

**Na Allan Isack, ARUSHA**

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali, Prof. Adelardus Kilangi, amevitaka vyuo vikuu nchini kuwaandaa vijana katika masomo kulingana na mahitaji ya soko la ajira ili kuondokana na tatizo la ajira wakati wanapohitimu masomo yao.

Kilango alisema hayo Jumamosi iliyopita katika mahafali ya nne ya Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino Tanzania (Saut) Tawi la Arusha. Katika mahafali hayo, wanafunzi 498 wa kozi mbalimbali walihitimu.

Alisema umefika wakati sasa vyuo vikuu kuwaandaa vijana kulingana na mahitaji ya soko ili kupata ajira kwa haraka pindi wanapohitimu.

"Naomba vyuo kuanza kujiuliza kwa nini vijana wanaomaliza mafunzo hawajiajiri wala kuajiriwa na kuzifuata fursa mbalimbali zilizopo nchini ikiwamo katika sekta ya kilimo," alisema.

Prof. Kilangi alisema wahitimu wanapaswa kuangalia ni kwa jinsi gani watatambua na kuzitumia fursa mbalimbali za kukuza maendeleo ya nchi kwa kutumia taaluma ili kuwa washindani katika soko la ajira kwa kujiajiri.

"Tumieni muda wenu na elimu mliyopata kuzitafuta fursa katika mitandao ya kijamii na kuacha kutumia mitandao hiyo kwa mambo yasiyofaa kwa kuwa soko kubwa lipo ndani ya mitandao hiyo," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro, kwa upande wake alivitaka vyuo hivyo kuandaa mitaala ya masomo kulingana na mahitaji ya soko la ajira la ndani na nje ya nchi.

Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Arusha, Isaack Amani, alisema kipindi hiki kuna tatizo kubwa la ajira kwa vijana, hivyo kuna umuhimu mkubwa kwa wahitimu kutanguliza weledi na nidhamu mbele ili kukabiliana na ushindani uliopo.

Aidha, aliwataka wahitimu kutumia taaluma zao na vipaji vyao kuleta maendeleo kwenye taifa na waendane na dhana ya uchumi wa viwanda.

Mkurugenzi wa Chuo hicho, Charles Rufyiliza, alisema kuna dhana imejengeka kuwa wanaosoma vyuo vya binafsi hawapati mikopo kutoka serikalini, jambo ambalo si kweli kwa kuwa wanafunzi walioomba mikopo mwaka huu, wamepatiwa kabla ya kufika chuoni hapo.



Distributed via ippmedia

Katibu Uenezi, Siasa na Itikadi wa CCM Taifa, Humphrey Polepole, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Arusha juzi, wakati wa kikao kazi cha siku tatu cha kufanya tathmini ya utekelezaji wa Ilani ya chama kwa mkoa huo, kwa kipindi cha miaka minne (2015/2019), **PICHA ALLAN ISACK**

# Wananchi 25,000 wanufaika elimu ya ujasiriamali

**Na Daniel Sabuni, ARUSHA**

WANAWAKE na vijana 25,000 kutoka nchi sita za Jumuiya ya Africa Mashariki (EAC) wamefaidika na miradi ya ujasiriamali kutoka Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Ujerumani (GIZ).

Joyce Kimaro, Mshauri Mkuu wa mpango huo, alisema hayo juzi jijini hapa wakati wa kikao kilichowakutanisha wadau waliofaidika na programu hiyo.

Kimaro alisema wananchi hao wamewezeshwa kubuni wazo la kibiashara linalogusa wananchi wa nchi wanachama wa EAC.

Alisema mawazo hayo yalipitishwa kwenye programu hiyo iliyoanza kutekelezwa mwaka 2016, lengo likiwa kutoa elimu ya biashara, masoko na jinsi ya kufanya biashara na kupata faida pamoja na kukuza mitaji.

"Tunapoona wazo la biashara limekidhi vigezo tunawapa elimu na mtaji kulingana na biashara wanayofanya. Pia tunawapatia Dola za Kimarekani 500 kwa kikundi," alisema Kimaro.

Baadhi ya wadau waliofaidika na programu hiyo kutoka Tanzania, walisema awali walikuwa na mitaji midogo, lakini kwa sasa mradi huo umewainua kiuchumi.

Mary Ngulupa, mfanyabiashara wa urembo alisema programu hiyo imewasaidia kupata elimu ya kukuza mtaji kwa wanawake na vijana katika biashara.

"Mwanzoni nilikuwa na mtaji mdogo lakini baada ya kuwezeshwa nimekuza mtaji na kumudu mahitaji ya familia yangu," alisema Ngulupa.

Alisema amesomesha watoto wanne shule za mchepuo wa Kiingereza na kumlipia kijana wake ada ya chuo kwa Sh. 30,000 za Kenya.

Programu hiyo imekuwa katika utekelezaji wa miradi 25 kuanzia mwaka 2016 na mradi huo ulizinduliwa na Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo, Balozi Liberat Mufumukeko.

# Ukatili kiuchumi tishio kwa wanawake, watoto

**Na Mwandishi Wetu, SIHA**

UKATILI wa kiuchumi unaoendelea kutukuzwa na baadhi ya koo katika Kata za Livishi, Sanya Juu na Nasai, Siha mkoani Kilimanjaro, unatajwa kutishia ustawi wa wanawake na watoto.

Baadhi ya walimu wa shule za msingi na sekondari, waliokuwa wakishiriki semina ya kuijengea jamii hamasa juu ya uwapo wa mpango kazi wa kitaifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya watoto wa kike katika wilaya hiyo, wameibua mjadala mpana na maswali yanayohitaji majibu.

Katika mjadala ulioanzishwa mwishoni mwa wiki na baadhi ya walimu walioko wilayani hapa, tatizo lililopo kwa sasa ni baadhi ya familia kutokuwa na sauti katika mali inayowahusu, wengine kufanyishwa kazi kwa malipo kidogo, kutomiliki mali inayowahusu na baadhi ya maeneo wanawake kutoruhusiwa hata kukata ndizi shambani.

Mmoja wa walimu hao, Modesta Massawe, alisema katika baadhi ya familia, watoto wa kike wanakosa amani kutokana na mila kandamizi. Mwanamke akipewa eneo la urithi na baba yake kwa ajili ya ujenzi wa makazi au kilimo, kaka yake hawezi kula ndizi inayotoka katika eneo hilo. Mwalimu Azan Kinyale alisema tatizo lingine linaloitesa Wilaya ya Siha ni kutelekezwa kwa watoto wanaosoma shule za msingi na baadhi ya shule za sekondari kutokana na ugumu wa maisha.

"Karibu asilimia 60 ya watoto waliopo katika wilaya hii wanaishi na bibi na babu zao na wazazi wenye watoto hao wamekimbilia katika miji mikubwa kutafuta maisha na hawawajibiki kutoa mahitaji yao ya lazima ya elimu kama sare za shule au madaftari," alisema Kinyale.

Mradi huo wa miezi minane unatekelezwa na mratibu wa mradi huo kutoka Kituo cha Haki za Binadamu na Jinsia mkoani Kilimanjaro (Kwieco) kwa ufadhili wa Foundation for Civil Society, utazihusisha shule 12 ambazo zitaundwa vilabu vya kupinga ukatili huo.

Mratibu wa mradi huo kutoka Kwieco, Peter Mashingia, akibadilishana uzoefu na walimu hao, alisema kazi wanayoendelea nayo hivi sasa ni kujaribu kupunguza au kutokomeza ukatili huo na kusukuma huduma za elimu ya sheria na haki za binadamu kwa wanakamati 48 wanaotoka kata za Sanya Juu, Nassai na Livishi zinazotishiwa na ukatili huo.

"Unajua tunachokifanya sasa hivi huku ni kujikita zaidi kupinga mila na desturi kandamizi na kuhamasisha usawa toka ngazi ya familia, hasa kuwajengea uwezo wazee wa ukoo kuhakikisha wanajikita katika ulinzi wa watoto hususani watoto wa kike. Ukatili wa kiuchumi katika maeneo haya ni suala linalopaswa kupigiwa kelele kwa nguvu zote," alisema Mashingia.

Walengwa wanaohusishwa katika mradi huo ni vikundi vya wanawake katika jamii (kiuchumi na kidini), wataalamu katika taasisi za elimu, Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Siha, maendeleo ya jamii, ustawi wa jamii, wajumbe wa baraza la madiwani, maofisa watendaji wa kata na maendeleo ya jamii kata.

Wengine ni wanafunzi wa shule 12 za msingi na sekondari, dawati la polisi, jinsia na watoto, wazazi na walezi, waathirika wa ukatili wa kijinsia na vyombo vya habari.



Distributed via ippmedia

Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Prof. Makame Mbarawa (wa pili kulia), akikabidhi vitendeakazi kwa Katibu wa Bodi mpya ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (MUWSA), Mhandisi Aron Joseph ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo, katika hafla ya uzinduzi wa bodi hiyo, uliofanyika mjini Moshi mkoani Kilimanjaro wikiendi. **PICHA: DIXON BUSAGAGA**

# Wenye ulemavu wapewa elimu

**Na Mary Mosha, MOSHI**

LICHA ya kuwapo kwa watu wenye ulemavu wa viungo, wenye uhitaji mkubwa wa viti mwendo ili kuwasaidia kusogea sehemu moja kwenda nyingine, bado wataalamu wanashauri kutopewa viti hivyo bila kupimwa kwa afya zao ili kutumika kama tiba.

Mtaalamu wa Tiba wa Vitendo kutoka CCBRT Moshi, Neofita Lukiringa, alisema hayo alipozungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki.

Aliitaka jamii inapotaka kuwasaidia watu wenye ulemavu hasa wa uti wa mgongo kuhakikisha wanawataalamu wanaofanya vipimo ili kupunguza madhara yanayotokana na matumizi mabaya ya viti mwendo.

"Tunaomba watu wanaotaka kutoa msaada wa viti mwendo ni vyema kuwasiliana na wataalamu wa afya na wahusika mwenyewe kwa ajili ya kufanyiwa vipimo kabla ya kununua viti hivyo ambavyo vinaweza kuwaletea madhara zaidi badala ya kuwasaidia kupata matibabu," alisema.

Jennifer Mushi, mwenye ulemavu wa uti wa mgongo wilayani Hai, alisema wagonjwa wengi wa ulemavu wa uti wa mgongo na ulemavu mwingine hujikuta wanapata shida zaidi baada ya kusaidiwa viti mwendo kutokana na uhitaji wao.

"Jamii yetu haina uelewa. Hata mimi mwenyewe sikuwa na uelewa mpaka nilipoelimishwa katika Hospitali ya KCMC, hivyo tunaiomba serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha wanatoa elimu kwa jamii ili kuwasaidia watu wenye ulemavu," alisema.

Samson Wilson, mkazi wa Moshi Mjini, alisema licha ya kukosekana kwa elimu ya baadhi ya mambo yanayowahusu watu wenye ulemavu kutokana na serikali kutotoa kipaumbele kwa jamii ya watu wenye ulemavu.

Alisema watu wenye ulemavu wamesahaulika na jamii hasa katika taasisi za serikali hawapewi huduma stahiki, ikiwamo kusikilizwa na ukalimani hasa pale wanapotaka kutoa ushahidi au kutolewa ushahidi, mara nyingi hukosa haki zao za msingi.

"Serikali kupitia mashirika yasiyo ya kiserikali ya kutetea haki za binadamu, ni muhimu kuanzisha vipindi maalumu katika vyombo vya habari vinavyotoa elimu mbalimbali na namna ya kumhudumia mtu mwenye ulemavu ili kusaidia kupata haki zao za msingi.

**"Tunaomba watu wanaotaka kutoa msaada wa viti mwendo ni vyema kuwasiliana na wataalamu wa afya na wahusika mwenyewe kwa ajili ya kufanyiwa vipimo kabla ya kununua viti hivyo ambavyo vinaweza kuwaletea madhara zaidi badala ya kuwasaidia kupata matibabu," alisema.**

# Huduma hafifu simu zamkera RC

**Na Mary Mosha, MOSHI**

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, ameitaka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kusogeza huduma ya mawasiliano kwa wananchi wa vijiji vya wilaya hasa za Same na Rombo vilivyoko maeneo ya mipakani.

Mghwira amesema ili kupata mawasiliano, wananchi hao hulazimika kusafiri kutoka kata moja kwenda nyingine.

Pia wananchi wa baadhi ya maeneo hayo wamekuwa wakipanda kwenye miti, ili kufanya mawasiliano hali ambayo inakwamisha fursa za maendeleo jambo ambalo halikubaliki na serikali ya awamu ya tano.

Mkuu huyo wa mkoa aliyasema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita mjini hapa, wakati akizungumza na watu wenye ulemavu wa kutosikia (viziwi) na wa kutoona waliokutanishwa na TCRA kwa lengo la kupatiwa elimu ya mawasiliano na usajili wa laini za simu za mikononi.

Alisema miongoni mwa maeneo ambayo yanatajwa kukosa mawasiliano ni pamoja na yaliyo kwenye jiografia ya milima ya Pare katika wilaya hizo. Wananchi wengi katika maeneo hayo simu zao husoma minara ya Kenya.


"Katika wilaya hizi za Same na Rombo yako maeneo ambayo wananchi hawapati mawasiliano kabisa mpaka wapande kwenye miti au wasafiri kutoka kata moja kwenda nyingine kwa ajili ya mawasiliano na hilo kwenye serikali ya awamu ya tano halikubaliki kwa wananchi kukosa fursa za maendeleo," alisema.

Ester Urassa, mkazi wa Tarakea alikiri kutokuwapo kwa mawasiliano na kuiomba TCRA kuangalia uwezekano wa kuzishauri kampuni za simu kuweka minara ili wapate mawasiliano zaidi.

"Mbali na mawasiliano ya simu hatuna hata redio na hazishiki huku, hivyo Mamlaka ya Mawasiliano waangalie uwezekano wa kufanya ili tupate mawasiliano kama Watanzania wenzetu," alisema Ester.

Jan Kaaya, mhandisi mwandamizi wa TCRA Kanda ya Kaskazini alisema tayari serikali imeanza hatua za kufanya tathmini katika maeneo hayo ili kupeleka minara ya mawasiliano kwa haraka.


Nipashe
# TESA
Jumanne Novemba 19, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


Ukurasa 15

**Wake wa viongozi watua kuikomboa shule wanayolelewa wenye Ualbino**

Ukurasa 18


Walionusurika kukeketwa Serengeti katika mahafali kuhitimu ujasiriamali


Ukurasa 18

## Mwarobaini wa mrundikano darasani unapatikana hapa


Distributed via ippmedia

# Tuzo mpya Walimu na Wanafunzi Bora yaanika siri ya ufanisi shuleni

Ukurasa 16

# ELIMU KUTOKA POLISI



Kamishna wa Operesheni na Mafunzo ya Jeshi la Polisi, CP Sabas, akisalimiana na wakazi wa Pasua Boma Mbuzi, wilayani Moshi, baada ya kumalizika kwa kikao chake na wananchi hao aliowapongeza kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama katika kupunguza uhalifu katika makazi yao. **PICHA ZOTE: JESHI LA POLISI**



Kamishna CP Sabas akifurahia jambo na wanafunzi wa shule za msingi waliokuja kumsalimia baada ya kumalizika kwa mkutano wake na wananchi. Zaidi amewapongeza kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama katika kupunguza uhalifu kwenye makazi yao.



Kamishna wa Operesheni na Mafunzo ya Jeshi la Polisi, CP Liberatus Sabas, amefanya mkutano wa kuwashukuru wananchi wa Pasua Boma Mbuzi wilayani Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro kwa kupunguza uhalifu.



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**

marobarnabas@yahoo.com

# Twajenga na kubomoa sawia

'JENGA' ni kitendo cha kutengeneza kitu kwa kutumia vifaa mbalimbali imarisha. Fanya kitu kikue au kiimarike.

'Bomoa' ni kitendo cha kuvunja kitu kama vile jengo; ni kuharibu mipango iliyowekwa; kitendo cha kushusha mtu hadhi.

Maana ya 'sawia' ni kwa wakati mmoja; kwa wakati uleule; kwa wakati huohuo. Nimeanza kwa ufafanuzi wa maneno 'jenga', 'bomoa' na 'sawia' ili wasomaji wangu waelewe maana sahihi ya maneno hayo kwani ni baadhi ya maneno yanayopotoshwa mara kwa mara na magazeti yetu ya Kiswahili.

Mara nyingi baadhi ya vyombo vya habari huandika au kutangaza, kwa mfano: 'Chama cha Chadema.' Kirefu cha 'Chadema' ni Chama cha Demokrasia na Maendeleo. Kuandika au kusema 'Chama cha Chadema' si sahihi. Kwa hiyo inapoandikwa au kusemwa 'Chadema' inakidhi haja (tosheleza). Ni kama kuandika au kusema 'CCM' yaani kifupisho cha 'Chama Cha Mapinduzi'. Hivyo kuandika au kusema. 'Chama cha CCM' ni kosa.

Distributed via ippmedia

Gazeti fulani liliandika kichwa cha habari kuwa "Chama cha NDL wamtaka Jafo ajiuzulu." Kwa usahihi (hali ya jambo au kazi kutokuwa na kasoro au kosa) kichwa kingeandikwa: "NDL chamtaka Jafo ajiuzulu;" au "Viongozi NDL wamtaka Jafo ajiuzulu." Msomaji fulani alinitumia ujumbe ufuatao: "Habari ticha. Mimi naitwa Hanif nakaa Mbagala. Nifafanulie maana 'sebu'. Kwa mfano 'nimekuwita njoo ww ukanijibu sebu je! Sitaki au sebu hapo katia viwi kipi Kiswahili fasaha cha kukataa niki." (0686 453 478).

Awali ya yote napenda kumfahamisha msomaji huyo kuwa mimi si mwalimu kama alivyoniita 'ticha' Nimelazimika kujifunza Kiswahili ili kuwasaidia watu wasiojua maana halisi ya maneno ya Kiswahili au wanaopenda kuchanganya Kiswahili na Kiingereza ingawa yapo maneno ya Kiswahili.

Pili, nimeshidwa kumwelewa, hasa neno 'sebu' hata baada ya kutafuta maana ya neno hilo kwenye kamusi tano tofauti nilizo nazo.

Soma uandishi wa siku hizi: "Maafande wa Tanzania Prisons kumbe wabishi buana! Kama hujui jamaa hao mpaka sasa ndio timu ambayo haijaonja kipigo katika Ligi Kuu Bara msimu huu, lakini jana pia waliwagomea vinara wa ligi kwenye Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam huku wakiwasapraizi Wanamsimbazi."

Nimeeleza mara nyingi kuwa 'buana' halimo kwenye lugha ya Kiswahili ingawa waandishi wanalitumia mara kwa mara badala 'bwana' ambalo ndilo neno sahihi.

'Habari' ni tamko la maamkizi. Kwa muktadha huu ni maelezo kuhusu jambo. Waandishi ndiwo waandikao matukio na kutangaza kwenye vyombo vya habari kama redio, runinga na magazeti.

Ni wajibu wa waandishi na watangazaji kuandika na kutangaza matukio yaliyotokea bila kutia chumvi. Kwa kuwa wao ni pua, masikio na macho ya wasomaji na wasikilizaji, hawapaswi kuandika / kutangaza kuwa "kama hujui …"

Ni kweli hawajui ndio sababu ya kuwa na vyombo vya utangazaji ili kuwajuza wasomaji na wasikilizaji. Kinachotakiwa ni waandishi na watangazaji kueleza matukio kama yalivyo/yalivyokuwa bila kuwauliza wasomaji/wasikilizaji maswali!

"… waliwagomea vinara wa ligi hiyo kwenye Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam huku wakiwasapraizi Wanamsimbazi. Prisons iliwasapraizi mashabiki wa Simba waliofurika uwanjani waliokuwa na imani kuwa chama lao…"

'Wakiwasapraizi' na 'iliwasapraizi' yanatokana na neno la Kiingereza, linaloandikwa'surprise'lenye maana ya mshangao, mastaajabu au mzimbao.

Kinachowafanya watangazaji, na hasa waandishi kutotumia maneno ya Kiswahili kama 'mshangao,' 'mastaajabu' au 'mzimbao' ni nini? Au wanawaonesha wasomaji na wasikilizaji kuwa wanaelewa zaidi Kiingereza kuliko Kiswahili!?

"Anayejidai mjanja ni mjinga." Maana yake mtu anayejidai kuwa mwerevu ni mjinga. Yawezekana akatokea mjanja kuliko yeye. Methali hii inatukanya dhidi ya kujidai kuwa wajuzi wa kila jambo.

"STARS FANTASTIC" ni kichwa cha habari katika gazeti maarufu la michezo nchini linalochapishwa kwa Kiswahili!

'Star' kwa Kiswahili ni nyota na wingi wake kwa Kiingereza ni 'Stars' ila kwa Kiswahili halina wingi kwani mamoja na wingi ni sawa, yaani 'nyota.' Si 'manyota!'

'Fantastic' pia ni neno la Kiingereza na maana yake kwa Kiswahili ni a kutisha; -a ajabu. Kama lina maana yake kwa Kiswahili kwa nini waandishi wa magazeti ya Kiswahili yatumie neno la Kiingereza? Ingeandikwa "Taifa Stars inatisha" au "Maajabu ya Taifa Stars" isingeeleweka?

Kichwa kingine kwenye gazeti hilohilo lenye waandishi 'waliobobea' (zamia katika jambo kwa uraibu mkubwa, kwa nguvu nyingi na kwa dhati; topea) kwa Kiingereza ingawa wanayatumikia magazeti ya Kiswahili kiliandikwa:

"Sheria kuamua ishu ya Mkwabi." Neno 'ishu' limetoholewa (kitendo cha mtu kubadilisha matamshi au tahajia* ya neno la lugha moja ili lilingane la matamshi au tahajia ya lugha nyingine) kutoka Kiingereza, yaani 'issue.' *Tahajia ni herufi zinazounda neno kulingana na mfumo wa lugha fulani.

**Methali: Umekuwa nanasi kutagia mibani?**

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Wake wa viongozi watua kuikomboa shule wanayolelewa wenye Ualbino

SHULE ya Msingi Buhangija, katika Manispaa ya Shinyanga, ilianzishwa mwaka 1960 na kusajiliwa rasmi mwaka 1974. Ilianza kufundisha wanafunzi wasioona na wasiosikia, waliojengewa kambi jirani na shule.

Mwaka 2009 kulipoibuka mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, serikali mkoani Shinyanga, ililazimika kuwapeleka watoto hao wahifadhiwe kwenye kambi hiyo ya watoto wenye mahitaji maalum ili wapatiwe ulinzi.

Baada ya kambi hiyo kuvuma kuhifadhi watoto hao wenye ualbino, wazazi wa mikoa mingine nao waliwapeleka watoto wao huko, huku baadhi wakiwatelekeza

Kadri miaka ilivyopita, kambi ilielemewa na watoto hao, huku shule nayo ikikabiliwa na changamoto ya upungufu wa madarasa, matundu ya choo, walimu na vifaa maalumu vya kusomea, vikiwamo vitabu vya nukta na nundu kwa wasioona.

MWALIMU MKUU

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Selemani Kipanya, anasema, awali kambi ilipaswa kuishi watoto 50 tu, lakini imezidiwa kufikia watoto 400, hali iliyofanya wadau wajitokeze kuwakomboa kwa kuwajengea mabweni.

Anasema, pia shule ilikabiliwa na upungufu wa madarasa, matundu ya choo, walimu, vifaa vya kusomea na miundombinu ya madarasa kutokuwa rafiki kwao.

""Wanafunzi wenye uhitaji maalumu ambao wapo shuleni hapa na wanaishi kambini wapo 230. Walemavu wa viungo wapo wawili, wasioona, wasiosikia na wenye ualbino131,"anaeleza Mwalimu Mkuu.

Anaendelea: "Walimu wenye taaluma ya elimu maalumu wapo nane tu na hakuna mliganyo wa kutoa elimu, ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi waliopo shuleni na kusababisha kuwepo mrundikano darasani."

**MAFANIKIO YALIVYO**

Mwalimu Kipanya anasema, baada ya wadau kujitokeza kusaidia shule hiyo, wakiwamo Umoja wa Wake wa Viongozi wa Taifa (New Millenium Women Group), hivi sasa shule imepunguziwa changamoto, ikibaki tatizo la upungufu wa walimu wa elimu maalumu.

Anasema awali mahitaji ya sasa, ofisi za walimu na madarasa shida ni moja kila upande; matundu ya vyoo yanahitaika mawili, na madawati shida ni 37.

Omtata Rose, ni mwalimu anayefundisha wanafunzi wasiosikia, anasema kutokana na uchache wao, inawapa wakati mgumu kufundisha, kwa mwalimu mmoja anafundisha wanafunzi 21, wakati alipaswa kufundisha wanafunzi wanane, ili



Watoto wenye ulemavu wanaosoma Shule ya Msingi Buhangija, Manispaa ya Shinyanga, wakiwa kwenye hafla ya kukabidhiwa madarasa manne, matundu ya choo 10 na vifaa vya kusomea, kutoka kwa Umoja wa Wake wa Viongozi Taifa. **PICHA: MARCO MADUHU.**

Distributed via ippmedia

"Kutokana na uchache wetu walimu, wengine wamekuwa wakishindwa kuelewa kwa haraka na kujikuta wakifanya vibaya mitihani.

kuwaelewesha vizuri.

Kwa mujibu wa Mwalimu Rose, mfano linganishi idadi ya sasa ilivyo na mahitaji ya zamani katika mabano:Ofisi za walimu moja (Nne); vyumba vya madarasa mahitaji ni moja (25); matundu ya vyoo 37 (2); madawati 383 (37).

Anafafanua zaidi:"Wanafunzi hawa wenye uhitaji maalumu hasa wasiosikia huwa wanakuja shuleni hapa hawajui kabisa lugha ya alama, hivyo wanahitaji kuwa nao karibu sana ili wapate kuielewa.

"Kutokana na uchache wetu walimu, wengine wamekuwa wakishindwa kuelewa kwa haraka na kujikuta wakifanya vibaya mitihani," anasema Mwalimu Rose.

"Mfano, kwenye matokeo ya mwaka huu ya kuhitimu darasa la saba, wanafunzi viziwi waliofanya mtihani ni wanane, lakini waliofaulu watano, tofauti na wenye ulemavu mwingine, wasioona na wenye ualbino ambao wote walifaulu kwenda kidato cha kwanza," anasema.

Aidha, anarejea matokeo ya mwaka jana ya kuhitimu darasa la saba, wanafunzi wenye ulemavu wa kutosikia, waliofaulu watatu; asiyeona mmoja na alifaulu; wenye ualbino walikuwa watano na wote walifaulu.

Katika matokeo ya darasa la saba mwaka huu, waliofanya mtihani walikuwa wanane na walifaulu watano; wasioona wanne wote walifaulu; wenye ualbino na wote walifaulu, ikisa mafanikio ya asilimia 93

Ni matokeo yaliyoipa shule Buhangija nafasi ya 13 kiwilaya, kati ya 48 za umma Shinyanga Mjini. Mwaka jana ilishika nafasi ya 18.

**SERIKALI SHINYANGA**

Ofisa Elimu Maalumu wa Manispaa ya Shinyanga, Edward Mdagata, anakiri shule hiyo inakabiliwa na upugufu wa walimu wa elimu maalumu na tayari wameshatuma maombi serikalini.

Mkuu wa Mkoa Shinyanga, Zainabu Telack, anaahidi seikali itatimiza ndoto za watoto hao kambini, wenye amani. Anafafanua:"Sisi kama serikali tupo bega kwa bega na watoto wetu hawa wenye ulemavu mbalimbali wakiwamo albino.

"Ndio maana tumekuwa tukijitahidi kutafuta wadau wa kuwasaidia kutatua changamoto zao na leo hapa tupo na wake wa viongozi kitaifa wakikabidhi madarasa, matundu ya choo na vifaa vya kusomea. Nawaomba wadau wengine waendelee kujitokeza ili kuwatatulia changamoto watoto hawa."

Katibu Tawala wa Mkoa Shinyanga, Albert Msovela, anasema baada ya kupokea fedha hizo, alizisimamia kuhakikisha madarasa yanajengwa na matundu ya choo 10, yaendane na thamani halisi.

Anafafanua bajeti yake, iliyotumika kujenga madarasa manne ni Sh. milioni 65.8; matundu ya choo Sh. milioni 21.1 na zimebaki zaidi ya Sh. milioni 40, fedha anazobainisha watazielekeza kwenye matumizi mengine.

**WAKE VIONGOZI**

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Viongozi Kitaifa, Tunu Pinda, anasema mwaka 2014 walipofika kutembelea shuleni Buhangija, kwenye kambi walikuta mlundikano wa watoto wakikabiliwa na changamoto na wakaamua kufanya harambee kuchangisha fedha, ili kuwasaidia.

"Sisi kama wake wa viongozi ikatubidi tujadiliane kufanya kitu cha kuwasaidia na kuamua kufanya Harambee jijini Dar es Salamu, huku mgeni rasmi alikuwa Waziri Mkuu Mizengo Pinda, ambaye kwa sasa ameshastaafu," anasema Tunu.

"Tulijiwekea kukusanya kiasi cha fedha Sh. milioni 400, lakini hatukuweza kufanikiwa kuzipata. Tulipata fedha taslimu Sh. milioni 65 na mara baada ya kukusanya michango yote na ahadi tukapata Sh. milioni 93, ambazo tukazileta hapa shuleni ili kutatua changamoto zilizopo," anasema.

Mary Majaliwa, mke wa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ndiye mlezi wa umoja huo, anasema fedha hizo zilijenga madarasa manne na matundu 10 ya vyoo na anaahidi kuongeza Sh. milioni 3.6 kumaliza kasoro zilizopo.

**WAZIRI NDALICHAKO**

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, anawapongeza wake wa viongozi kitaifa kusaidia kutatua shida katika elimu kwa watoto hao wenye ulemavu wa Buhangija.

"Wizara ya elimu, Sayansi na Teknolojia itaendelea kutatua changamoto za shule hii ya walemavu. Mwaka 2017 tulitoa pesa Sh.286,600,000 kupitia mpango wa 'Lipa Kulingana na Matokeo' (EP4R), kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili, vyumba vinne vya madarasa na matundu ya choo 18,"anasema Waziri Ndalichako.

"Fedha hizo pia zilikarabati vyumba saba vya madarasa na ofisi tatu za walimu na mwaka huu kupitia mpango huo huo wa "Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R)' tumetoa Sh. milioni 12.5 kwa ajili ya kukamilisha boma la darasa lililojengwa na wananchi," anaongeza.

Anasema ujenzi huo utasaidia kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto za shule hiyo.

ELIMU

NA BEATRICE MOSES

# Tuzo mpya walimu na wanafunzi Bora yaanika siri ya ufanisi shuleni

• Waliong'ara wafunguka mbinu zao • Jafo: Sekondari Kata zawasha taa • Alama rasmi kuwatambua hapa kazi'



Mwalimu Kalimbe Keyyu wa somo la Kemia, akipokea tuzo kutoka kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tamisemi), Selemani Jafo.



Distributed via ippmedia

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tamisemi), Selemani Jafo, akimkabidhi tuzo Mwalimu wa Kiswahili, Barnabas John, katika hafla iliyofanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: MIRAJI MSALA**

HISTORIA mpya imeandikwa katika sekta ya elimu, baada ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kuanzisha tuzo za elimu.

Ni tuzo inayotolewa kwa 'Wanafunzi Bora; Walimu Bora, halmashauri na mikoa iliyofanya vyema kwenye mitihani ya taifa ya kidato cha tano na darasa la saba.

Hatua hiyo ya Tamisemi, inatajwa dira ya kuchochea kwa kiwango cha elimu nchini, kwa kuwa itawezesha kuongezeka ushindani katika kujifunza, kufundisha, kusimamia na kuweka utekelezaji wa sera za sekta hiyo kwa ujumla.

Waziri mwenye dhamana Tamisemi, Selemani Jafo, alikuwa mgeni rasmi katika hafla ya tuzo hizo iliyofanyika jijini Dar es Salaam, kukabidhi tuzo kwa washindi wa nafasi mbalimbali.

Walimu wa shule za msingi waliotunukiwa tuzo hizo ni Sinyati Sioi kwa somo la Kiswahili wa Kemebos, Mkoa wa Kagera; Benard Makare (Sayansi), shule ya Paradise, Geita; John Matata(Hisabati), shule ya Granyaki, mkoa Mara; Alfred Gikaro(Kiingereza), shule ya Little Treasures, Shinyanga, Thomas Makonye( Maarifa ya Jamii) God's Bridge Mbeya .

Upande wa walimu wa sekondari waliotunukiwa tuzo za ni; Oliva Mwasenga, somo la Uchumi, Kibaha- Pwani; Laurenk Ndonje (Baiolojia ), Canossa, Dar es Salaam; Dotto Shirima (Uhasibu), St. Christina Girls, Tanga; Wilberd Mwekwa (Historia), Kisimiri, Arusha.

> Ufundishaji wa ushirikishaji majadiliano, kuwa na wanafunzi wenye nidhamu, ambao washiriki kujisomea kwa vikundi.



Mwalimu Meshack Twaiti, mahiri wa kufundisha somo la Hesabu, akipokea tuzo kutoka kwa Waziri Selemani Jafo.

Wapo; Jonas Bichwa (Jiografia), Mwilamvya, Kigoma; Ndemas Hassan (Biashara), Kibaha, Pwani; Barnabas John (Kiswahili), Kasulu, Kigoma; Julio Mario (Fizikia), Feza Boys, Dar es Salaam; Meshack Twaiti (Hesabu) St. Jude, Arusha; Samson Mlele (Kiingereza) na Kalimbe Keyyu wote wa Kisimiri, Arusha

## WASEMAVYO WASHINDI

Twaiti, aliyetangazwa mwalimu bora wa somo la Hesabu kidato cha sita, alibainisha siri yake ni kwamba, alihakikisha anajenga mazingira bora ya ushirikiano na wanafunzi wake.

"Ufaulu wa mwanafunzi unaonyesha jinsi alivyoelewa, lakini walikuwa na adabu nzuri. Pia, ina shule mazingira rafiki kwa wanafunzi, kuna maktaba yenye vitabu vyote muhimu , hivyo walikuwa wanakwenda kujisomea walipokwama waliniuliza," anasema Mwalimu Twaiti.

Anabainisha kuwa pia uongozi wa shule unawahudumia vyema wanafunzi na walimu kwa ujumla na kumshirikisha Mungu katika shughuli zao kwa ujumla.

" Siyo kazi rahisi mwaka 2016 nilishika nafasi ya 127, mwaka 2017 nikawa wa 44 kutoka hapo nikaongeza bidii zaidi hatimaye nimefanikiwa kushika namba 1, hakika namshukuru Mungu," anasema Mwalimu Twaiti.

Mwalimu John, mahiri katika ufundishaji lugha Kiswahili kidato cha sita mwaka huu, anaeleza ushindi aliyoupata umechangiwa na ushirikiano mzuri na wanafunzi, uliowasaidia saikolojia, ya kupenda somo hilo.

"Nilifundisha kwa kuwashirikisha mara kwa mara, huku nikiwashauri kujisomea kwa 'bidhaa' (marejea kama vitabu), kwa kuwa walikuwa na utii wamefanya vizuri hatimye kuleta matokeo mazuri," anasema.

Anabainisha, pia ushirikiano mzuri wa kikazi aliyopata kwa walimu wenzake, ulimjengea utulivu na kumfanya atumie muda mwingi kujipanga vizuri kuwafundisha wanafunzi.

Mwalimu Hassan wa somo la biashara alibainisha kuwa mbinu za ufundishaji alizotumia, ndizo walizofundishwa vyuoni.

"Ufundishaji wa ushirikishaji majadiliano, kuwa na wanafunzi wenye nidhamu, ambao wanashiriki kujisomea kwa vikundi. Pia, binafsi nilihakikisha nakamilisha mtaala kwa wakati unaotakiwa," anasema mwalimu Hassani.

Keyyu, aliyetangazwa mwalimu bora wa somo la Kemia, anabainisha mikakati na mbinu zake kwamba, aliwajengea ujasiri wanafunzi wake, kwa kuwaeleza somo hilo 'siyo gumu' hivyo waondoe woga.

"Baada ya kuwajenga kisaikolojia, wanafunzi wetu ambao walikuwa ni mseto, ingawa kuna wakati nililazimika kuzungumza na wasichana pekee, kwa kuwa mimi ni mwalimu wa kike, nilitamani kuwavutia ili wasiogope wajitume," anasema.

Anaeleza: "Pia nilikuwa nawahimiza kujisomea kurudia yale niliyowafundisha na mengine wasome kwenye vitabu maktaba, kisha nikawa na tabia ya kuwashtukiza kwa mitihani ya majaribio mara kwa mara."

Mwalimu Keyyu anaeleza imani yake kwamba, mitihani hiyo iliwajengea uwezo mzuri, kwa kuwa walilazimika kujisomea kwa bidii wakiamini mwalimu wao hatabiriki.

## WAZIRI JAFO

Waziri Jafo katika hotuba yake, anaeleza ni tuzo za kwanza kutolewa na serikali na awali kulikuwapo wadau wachache, ikiwamo Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, ambao walitoa tuzo hizo kwa namna tofauti.

Anabainisha kuwa tuzo hizo mpya zinazofungua historia mpya nchini na alama ambayo serikali hivi sasa inaweka kutambua juhudi za walimu na wanafunzi waliofanya vizuri.

" Serikali ya awamu ya tano imeamua kuwekeza kwa namna yake kwenye elimu, ilianza na elimu bure, ukarabati wa shule kongwe tayari mafanikio makubwa ya uwekezaji yanaonekana kwa kuwa kumekuwa na ongezeko la ufaulu kwa ngazi zote kuanzia darasa la saba hadi kidato cha sita," anasema Jafo.

Anabainisha kuwa katika matokeo ya mtihani wa mwaka jana, katika jumla ya shule bora 100, shule 64 zilikuwa za umma, kati ya hizo shule 52 zilikuwa za kata.

Jafo anaeleza kuwa wanajipanga vizuri ili kuongeze tuzo ya wanafunzi, mwanamichezo bora na msanii wa mwaka ili kutambua kukuza michezo kwa kuwa elimu ni pamoja na michezo.

HAKI, UWAJIBIKAJI & VITA YA RUSHWA

# Darasa Wiki Azaki, sura halisi kuwajibikia umma

• Zatamba ni 'mkoa bubu'



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akikata utepe kuashiria ufunguzi wa Maonyesho ya Wiki ya Azaki katika Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Niko Kasera**

KUMEKUWAPO mjadala mpana kuhusu Asasi za Kiraia au Azaki na nini hasa mchango wao kwenye jamii ya Watanzania.

Wiki zinaelekea mbili tangu Azaki chini ya uratibu wadau kama The Foundation for Civil Society na Policy Forum, kwa kile walichokiita 'Wiki ya Azaki Tanzania.'

Kongamano hilo lilitoa fursa kwa wadau hao kujadili kwa pamoja na kuonyesha ni kwa namna gani zimekuwa na mpango mpana kwenye taifa, ikiwamo suala mtambuka wa Uwazi na Uwajibikaji, pia kwenye maeneo mengine muhimu ikiwamo, afya, elimu bora na kilimo.

Kongamano hilo lilipata ugeni mzito sio tu wa mawaziri na wabunge, pia Msimamizi Mkuu wa Shughuli za Serikali, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ambaye alipofahamishwa mchango wa Azaki, alifurahishwa na kauli yao. Hapo ikaja dhana ya hitaji kushirikiana na kushirikishwa na serikali kuu pamoja na serikali za mitaa.

Wasilisho hilo lililotolewa na Azaki litabainisha pamoja na mambo mengine, zikisiositiza undugu na serikali na wabia wa maendeleo jamii ya Kitanzania.

Wadau hao walitumia fursa hiyo kufafanua baadhi ya tuhuma ambayo wamekuwa wakihusishwa nayo.

Wasilisho hilo linasema kati ya mwaka 2016 hadi mwaka jana, ripoti za fedha zilizokaguliwa kutoka Azaki 16 zinaonyesha kwamba zimeingiza fedha Sh. bilioni 236 kwenye uchumi wa Tanzania.

Kutokana na fedha hizo, Sh. bilioni 19 zimelipwa serikalini kwa njia ya kodi na ushuru, wakati Sh. bilioni 169 zimeelekezwa moja kwa moja kwa kutoa huduma kwa wanufaika. Waajiriwa wamepokea Sh. bilioni 45 kwa namna ya mishahara na posho.

Nini hasa umuhimu wa takwimu hizo za Azaki? Kimsingi, zinadhihirisha wazi kwamba Azaki hizi sio tu zina mchango mkubwa kwenye uchumi wa nchi, pia mchango wao unaweza kulinganishwa moja kwa moja na mapato ya mkoa mzima wa Mara kwa msimu wa mwaka 2018 hadi 2019, ambao ni pamoja na mbuga za kitalii na vyanzo vyote vingine. Hili sio la kubezwa.

Pia, kujitolea kwa Azaki kuweka wazi mapato yao na matumizi baada ya kufuata sheria na kuhakikisha kwamba vitabu vyao vinakaguliwa ni hatua muhimu ya kupongezwa, hatua ya uwajibikaji uliotukuka.

Ni kweli kwamba uamuzi wa kuwapo Wiki ya Azaki ulitoka na sio tu utashi wao Azaki, bali pia msukumo wa kutakiwa kuwa wazi zaidi pasipo shaka ambayo dalili ilionekana katika baadhi ya maeneo.

Wapo waliohoji uwajibikaji wake, ambayo baadhi yao walitolea majibu, kwamba zinasimama katika nafasi kuiunganishi na imekuwa na mchango mkubwa sio tu kuwakuleta wadau pamoja kujadili muhimu na magumu, bali hata mengi yanayoathiri, kama ufuatiliaji mapato ya umma namatumizi yake. Kote ni uwajibikaji binafsi kwa manufaa ya umma.

Kuna Azaki zimetoa mchango mkubwa kwenye sauti za wananchi kwa kuwapa fursa wenyewe kuzungumza hisia na maoni yao, ikiwamo maboresho kwenye sekta nyingi za umma. Vile vile, kuwapo utaratibu wa ufuatiliaji umesaidia kubainisha mapungufu ya kisekta na inaisaidia serikali kutafuta suluhisho la kudumu.

Ni muda sahihi kutafakari mtazamo wetu na mchango wa Azaki zinazotuzunguka.

**Kwa maoni na ushauri: samawatiarts@yahoo.com**

## JE, WAJUA?

## NA REUBENI LUMBAGALA

# Mwarobaini wa mrundikano darasani unapatikana hapa



Kwa kutumia utaratibu wa EP4R wanafunzi hawatarundikana darasani kama hivi. **PICHA: MTANDAO.**

KUTEKELEZA sera ya elimu bila malipo kumeleta mwamko mkubwa kwa wazazi na walezi kupeleka watoto wao shuleni. Kutokana na hali hiyo ongezeko kubwa la wanafunzi katika shule za msingi na sekondari kote nchini ni kubwa, hatua inayosababisha kuwapo na changamoto ya miundombinu ya kutosheleza mahitaji ya wanafunzi. Shule nyingi za msingi na sekondari zina uhitaji wa madarasa, madawati, meza, viti, ofisi za walimu, nyumba za walimu na vyoo ili kuweza kuhudumia kikamilifu wanafunzi waliopo shuleni.

Serikali ya Awamu ya Tano imetimiza mwaka wa nne tangu ilipoingia madarakani Novemba 2015. Katika kuadhimisha miaka minne ya serikali ya awamu hiyo sera ya elimu bila malipo nayo imetimiza mwaka wa nne tangu ilipoanza kutekelezwa Januari, 2016.

Kutokana na ongezeko kubwa la wanafunzi wanaojiunga na darasa la kwanza katika shule za msingi na wale wa kidato cha kwanza katika shule za sekondari, kumekuwa na uhitaji wa kuwa na mipango mikakati ya kuboresha na kujenga miundombinu ya shule ili kuwahudumia wanafunzi wanaosoma katika shule za msingi na sekondari zinazomilikiwa na serikali.

Miongoni mwa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika uboreshaji na ujenzi wa miundombinu ya shule hizo ni pamoja na mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R).

Mradi wa EP4R hushughulika na kufadhili ujenzi wa miundombinu ya shule ambapo kipaumbele ni kwenye halmashauri ambazo zimeshawishi, wazazi, walezi na wananchi kuchangia nguvukazi katika ujenzi wa maboma ya madarasa (majengo ya madarasa ambayo hayajaezekwa).

Baada ya wananchi kutoa nguvukazi zao, serikali husaidia kukamilisha maboma hayo. Hatua hiyo inafanikisha ujenzi wa madarasa mengi kwa fedha kidogo kutokana na wananchi kushiriki moja kwa moja katika shughuli za maendeleo ya elimu kupitia kuchangia nguvukazi zao na wakati mwingine rasilimali zikiwamo fedha.

Sh.bilioni 306 zimeshatumika katika awamu saba za mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo ambapo inaelezwa kwamba kumekuwa na mafanikio makubwa katika uboreshaji na ujenzi wa miundombinu ya shule na kufanikisha kwa kiasi kikubwa kupunguza changamoto ya mlundikano mkubwa wa wanafunzi madarasani.

Na sasa utekelezaji wa mradi wa EP4R upo kwenye awamu ya nane (Phase 8) ambapo serikali imetenga Sh. bilioni 201 ili kufanikisha uboreshaji na ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi na sekondari hapa nchini.

Akiwa wilayani Chato mkoani Geita, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa Joyce Ndalichako, alisema "ujenzi au uboreshaji wa miundombinu ni suala endelevu na ukiangalia katika kipindi cha uongozi wa Rais, John Magufuli, mpaka sasa kwenye mradi wa EP4R tumeshatumia bilioni 306 ambapo zimefanikisha kujenga madarasa katika awamu ya saba".

Aidha, Waziri Ndalichako anasema mgawo wa fedha za EP4R awamu ya nane, kipaumbele kitakuwa katika halmashauri ambazo zimefanya vyema kwenye matumizi ya fedha za EP4R katika awamu saba zilizotangulia.

Na kwa Halmashauri ambazo hazikufanya vyema zitapewa fedha baada ya kushughulikiwa wale wote waliokwamisha miradi hiyo.

Utengaji wa fedha za EP4R awamu ya nane utapunguza tatizo la msongamano wa wanafunzi madarasani ikizingatiwa kuwa katika matokeo ya darasa la saba yaliyotangazwa hivi karibuni, ufaulu wa wanafunzi uliongezeka.

Kupanda kwa ufaulu kunaleta moja kwa moja mahitaji ya vyumba vya madarasa, madawati, mabweni, maktaba na vyoo katika shule za sekondari.

Distributed via ipmedia

Aidha , kila mwaka kumekuwa na kundi kubwa la wanafunzi wanaoanza darasa la kwanza ambao nao wanahitaji mazingira bora ya kujifunza shuleni. Kwahiyo, bilioni 201 za awamu ya nane za ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya shule zitasaidia wanafunzi watakaojiunga na shule za msingi na sekondari kwa mwaka 2020.

Mathalani, Shule ya Msingi Miembeni ya wilayani Kongwa ni miongoni mwa shule ambazo wazazi wa wanafunzi pamoja na wananchi wamejitolea kuchimba msingi wa vyumba viwili vya madarasa, kusomba kokoto, mawe, mchanga, kutoa fedha za ununuzi wa saruji na vifaa vingine vya ujenzi ili kukamilisha maboma mawili ya madarasa kama njia ya kuiunga mkono serikali katika ujenzi miundombinu ya shule.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Miembeni, Gilbert Rwekaza, anasema: "Kutokana na jitihada za serikali za kuboresha miundombinu ya elimu, wananchi wameamua kushiriki shughuli za maendeleo ili kupunguza tatizo la msongamano wa wanafunzi darasani. Wito wangu ni jamii kuendelea kujitolea katika maendeleo kwani kwa kufanya hivyo tunajiletea maendeleo kwa haraka".

Kutokana na utaratibu wa serikali wa kutoa kipaumbele kwa maeneo ambayo wananchi wamechangia nguvukazi katika ujenzi wa miundombinu ya shule, mtazamo wa wananchi wa kuiachia serikali kufanya kila kitu katika ujenzi wa miundombinu ya shule unapaswa kubadilika. Ni vyema jamii ijione kuwa wao ni washirika wa moja kwa moja katika shughuli za kimaendeleo katika nyanja zote ikiwamo sekta muhimu ya elimu. Tafakari

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***
***Maoni:** (+255) 764 666349.*

RIPOTI

# Tiba mbadala ya saratani ni 'hatari zaidi kuliko faida'

WAGONJWA wa saratani wanapaswa kuwaambia madaktari wao kama wanatumia dawa za tiba asili kwa sababu baadhi ya dawa hizo zimetengenezwa na vitu vinavyoweza kusababisha kukoma kwa mchakato wa matibabu, mkutano wa wataalamu wa masuala ya maradhi ya saratani ulielezwa.

Vitunguu swaumu, tangawizi na vidonge vitokanavyo na majani ya 'ginkgo' kwa mfano, vinaweza kuchelewesha kupona majeraha ya ngozi ikiwa saratani ya titi itasambaa.

Daktari wa upasuaji Profesa Maria Joao Cardoso, anasema hakujawa na ushahidi kuwa tiba asili au krimu zilifanya kazi.

Kama kuna walakini, ni vyema kama dawa hizo hazitatumika, lakini ni vyema mgonjwa akalieleza.

"Madaktari wanapaswa kufanya ziada katika kuuliza wagonjwa wao kuhusu dawa nyingine wanazozitumia wakati wanapopatiwa matibabu," Profesa Cardoso aliiambia BBC.

Anasema ilikuwa muhimu kwa wagonjwa kutazamwa na madaktari wao kabla ya kuanza tiba mbadala kwa saratani iliyosambaa kwenye ngozi.

Hali hii hujitokeza kwa mtu mmoja kati ya watano wenye saratani ya matiti- na kwa kiasi kidogo kwa wagonjwa wenye saratani za aina nyingine.

Hatari ni kuwa bidhaa nyingi zinaweza kuingilia tiba za homoni au mionzi, na hizo huchelewesha mfumo wa damu kuganda- hali ambayo inaweza kusababisha vidonda kuchukua muda mrefu kupona.

Anadokeza baadhi ya bidhaa za dawa za asili kama mifano zinazoweza kuchelewesha kuganda kwa damu kuwa ni 'green chiretta'

'feverfew', vitunguu swaumu,'ginkgo',mizizi ya 'ginseng','hawthorn', 'horse chestnut' na ukwaju

Profesa Cardoso anasema haikushangaza kuwa wagonjwa na wanaowatunza kutafuta tiba za mitishamba au tiba mbadala ambazo pengine walihisi zingeleta matokeo tofauti.

Lakini anasema watu lazima wafahamu "wanaweza kuleta madhara zaidi badala ya matokeo chanya".

"Nia ya dawa ni muhimu kumbuka ni kutoleta madhara", alisema. **BBC**



Vidongetiba mbadala vya saratani. **PICHA: MTANDAO**

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Walionusurika kukeketwa Serengeti katika mahafali kuhitimu ujasiriamali

- Nyumbani kwao nako wawapa 'tano'

YAWEZEKANA mahafali haya hayajawahi kusikika kwa wengi, ingawa siku chache zijazo yatafanyika kwa mwaka wa pili na huenda yakatikisa zaidi kwa ajili ya maandalizi ya kipekee.

Ni mahafali ya wahitimu 'wajanja' waliokwepa kisu cha ngaribu ambao sasa wanahitimu mambo mbalimbali ukiwamo ujasiriamali.

Kuanzia sasa zimesalia siku 11 , kwani Novemba 29 mwaka huu, wahitimu 'wajanja' waliopiga chenga 'operesheni ukeketaji' watafanyiwa mahafali ya kuhitimu mafunzo ya mambo mengi yakiwamo ya ujasiriamali.

'Wajanja' hawa ni kundi la mabinti 13 walioibukia katika mbadala wa kupewa utaalam wa ujasiriamali, sasa wana hadhi rasmi ya wahitimu.

Mabinti hawa walikonga roho za wanakampeni wanaotetea ujanja wao, ni Shirika la Matumaini kwa Wanawake na Wasichana Tanzania wanakampeni hao, wanatekeleza mradi huo katika madarasa yaliyopo Mugumu Serengeti na Butiama mkoani Mara, ambayo yamepewa majina maalumu, ambayo ni nyumba salama.

Novemba 29 itakuwa hitimisho la mafunzo mbalimbali waliopewa mabinti hao 'wajanja' yakijumuisha uzalishaji, biashara na ujasiriamali.

Sherehe hizi zinafanywa kwa mara ya pili baada ya mwaka jana, mabinti nane kuhitimu mafunzo kama hayo na kukabidhiwa vyeti na vitendelea kazi, na sasa wanaendesha maisha yao kama kawaida.

Kupitia malezi ndani ya makazi hayo, wanakowekwa mabinti hao, shirika hilo limefanikiwa kuokoa wasichana na watoto zaidi ya 600, ambao baadhi yao wanasoma chekechea, shule za msingi, sekondari na vyuo.

Kwa mujibu wa mkurugenzi wa shirika hilo, Robi Samwel, baadhi yao walisharudi kwa wazazi wao baada ya wazazi na walezi hao kuelimisha kuhusu madhara ya ukeketaji, wakakubali kuachana na mila hizo potofu.

"Unaweza kuona idadi ya wasichana waliopo vituoni sasa ni ndogo, hii inatokana na kufanyika juhudi za kujenga uhusiano kati ya wazazi na watoto na kuwaruhusu warudi nyumbani," anasema Robi.

Anafafanua kuwa katika nyumba salama ya Mugumu kuna mabinti 55 wakiwamo pia watoto wadogo, huku nyumba ya Butiama ikiwa na mabinti 46 wakiwamo pia watoto wadogo.

Robi anasema, mabinti na watoto wanaendelea na shule wakiwamo wanaotarajia kuhitimu mafunzo, ambao wazazi wao wamekubali kuwapokea warudi nyumbani kuendelea na maisha bila kutishiwa kukeketwa.



Baadhi ya wasichana wanaotarajia kufanyiwa mahafali wakiwa kwenye mafunzo ya kusuka vikapu katika nyumba salama ya Mugumu. **PICHA: SABATO KASIKA**

### KURUDI NYUMBANI

Mkurugenzi huyo anasema, mabinti hao hawatarudi kwa wazazi wao kienyeji tu bali kuna utaratibu maalum uliowekwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanaishi bila kutishiwa kukeketwa.

"Shirika lilipokea wasichana na watoto waliokimbia kutoka nyumbani kwao kwa kukataa kukeketwa, hivyo hatuwezi kuruhusu warudi kwa wazazi wao kienyeji, ndiyo maana tumeweka utaratibu huo," anasema.

Anasema wameandaa fomu maalum zitakazosainiwa na shirika, ustawi wa jamii, dawati la jinsia na wazazi wenyewe, ambazo zinaelezea ukubali wao wa kuwapokea watoto na kuwalinda dhidi ya ukeketaji.

Anasema, wazazi wamekubali utaratibu huo na kuahidi kuuzingatia na kwamba ikitokea mmoja wao ameukiuka na kutaka kumkeketa binti yake, basi hatua za kisheria zitachukuliwa.

Hata hivyo, anasema katika wahitimu hao 13, mmoja ataendelea kuishi kwenye kituo cha shirika hilo, kwa vile wazazi wake wamekataa kumpokea wakidai kwamba aliwadhalilisha kwa kukataa kuketwa.

Anasema, Hope For Girls And Women Tanzania limepata mafanikio hayo yanayoambatana na utoaji wa elimu katika jamii, kwa kushirikiana na serikali na wadau wengine wanaopinga vitendo vya ukeketaji.

"Wapo baadhi ya wazazi waliokubali elimu hiyo na kuachana na mila hizo potofu ingawa wengine bado wanazing'ang'ania wakiwamo waliomkataa mtoto aliyetaka kurudi nyumbani baada ya kumaliza mafunzo," anasema.



Mkurugenzi wa Hope for Girls and Women Tanzania, Robi Samwel.

### WADAU NAO WANENA

Baadhi ya wadau wanaoshiriki katika vita hiyo ni ofisi ya Ofisa Maendeleo ya Jamii, Serengeti na Dawati la Jinsia, ambao wanasema ushirikiano wa jamii bado unahitajika kumaliza tatizo hilo.

Sijali Nyambuche ni Mkuu wa Kitengo cha Dawati la Jinsia na Watoto wa Kituo cha Polisi Mugumu, ambaye anasema vitendo vya ukeketaji kwa sasa vimepungua ukilinganishwa na kipindi cha nyuma.

> "Ukeketaji hufanyika kila mwaka unaogawanyika kwa mbili... mwaka huu inawezekana vitendo hivyo visifanyike kwa wingi hadi mwaka 2020, kwani ndiyo unaogawanyika kwa mbili.

Hata hivyo, anasema bado elimu zaidi inahitajika ili kusaidia kuibadili jamii ya Serengeti iachane na mila hizo zilizopitwa na wakati, ambazo zimekuwa zikisababisha madhara kwa watoto wa kike.

"Mabinti wamekuwa wakija kuomba hifadhi wakikimbia vitendo vya kukeketwa, bahati mbaya hatuna pa kuwaweka, badala yake tunawakabidhi Hope For Girls And Women Tanzania," anasema Nyambuche.

Anasema, wale ambao bado wanaendekeza ukeketaji hufanya vitendo hivyo usiku wa manane na tena porini, hali ambayo wakati mwingine husababisha iwe vigumu kuwakamata.

"Ukeketaji hufanyika kila mwaka unaogawanyika kwa mbili...mwaka huu inawezekana vitendo hivyo visifanyike kwa wingi hadi mwaka 2020, kwani ndiyo unaogawanyika kwa mbili," anasema.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Serengeti, Wambura Sunday, anasema katika kudhibiti vitendo hivyo, kila kijiji na kata kuna watu wao ambao wanatoa taarifa wanapoona kuna tukio la ukeketaji.

"Hatua hiyo imesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza vitendo hivyo ingawa vimekuwa vikifanyika kwa usiri mkubwa, lakini bahati nzuri tuna watu wetu kwenye jamii husika wanaotupa taarifa," anasema Sunday.

Sunday anasema, mchango wa wadau wote wanaopinga ukatili wa kijinsia ni mkubwa na kwamba hali ikiendelea kama ilivyo, kuna uwezekano wa kutokomeza mila potofu.



WADAU **SABATO KASIKA**

# Sauti za wadau

## Kujisomea ni njia mojawapo ya kujiongezea uelewa wa mambo mbalimbali, lakini wapo baadhi ya wanafunzi hawajisomei. Nini kifanyike waachane na mtindo huo? Wadau wanajadili.



### JAMES MUSYANGI (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

UZEMBE huu hauko kwa wanafunzi tu bali hata watu wazima, ambao ninaamini kwamba kinachosababisha ni hali hii ni ugumu wa maisha na kujikuta wakipoteza muda mwingi kwenye mihangaiko na kukosa nafasi hata ya kushika kitabu.


Kila kukicha wanawaza watakula nini watawasomesha watoto wao vipi. Yaani wana kila aina ya changamoto zinazowakabili katika maisha.

Mazingira haya ni tofauti ya miaka ya zamani ambayo watu wengi walikuwa wameajiriwa wana uhakika wa kupata pesa kila mwisho wa mwezi na hata waliojishughulisha na kilimo walikuwa na uhakika wa kupata mazao, lakini leo ni tofauti kabisa kutokana na hali halisi ikiwamo mabadiliko ya tabianchi, ambayo husababisha mvua zisinyeshe kwa wakati na hivyo kufanya mazao yakauke au kutoota kabisa.

Kwa hali kama hiyo ni vigumu watu kupata muda wa kupumzika na kujisomea.

Nikija kwa upande wa wanafunzi, ni kwamba kizazi cha sasa kimekuwa kigumu kuelewa, utandawazi umeharibu watoto wengi, wanapoteza muda kwa mambo yasiyofaa hali ambayo mimi ninaiona kuwa ndiyo inayochangia wasijisomee kabisa wakitegemea twisheni tu.

Niwakumbushe kwamba elimu ni muhimu na mafanikio katika elimu hayaji kirahisi, ni lazima wajishughulishe ikiwa ni pamoja na kujisomea vitabu mbalimbali kwa ajili ya kujijengea uelewa wa mambo mengi badala ya kubweteka tu na kuridhika kwa vitu ambavyo haviwezi kuwasaidia.



### CLAUDI COSMAS (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

TATIZO kubwa ninaloliona hapa la wanafunzi kutopenda kujisomea wenyewe nyumbani ni mazoea ya siku hizi ya twisheni.

Wanaamini kwamba wakishatoka twisheni inatosha, hawaoni kwanini wajisomee tena nyumbani. Mawazo kama haya ni potofu kabisa, hayafai kukaa kichwani mwa mwanafunzi anayejielewa na kutambua maana ya elimu.

Mwanafunzi anapotoka shule au twisheni, bado anatakiwa kutenga muda wa kujisomea nyumbani, lakini baadhi ya wanafunzi na hasa wa mijini wamekuwa wakihangaika na simu au televisheni kuangalia mambo ambayo wakati mwingine hayawahusu kabisa.

Ili kuwasaidia kurudi kwenye mstari, ni vyema wadau wote wa elimu wakiwamo wazazi wakafanya sehemu yao ya kuhimiza umuhimu wa elimu ili watoto wawe na moyo au watambue umuhimu wa kujisomea wawapo nyumbani. Maarifa na uelewa vinapatikana kwa njia ya kusoma au kujisomea, lakini wanafunzi wakifanya ujanjaujanja wajue kuwa huko mbele watakwama tu.

Na ikumbukwe kuwa mtindo huu wa kutojisomea na hata watu wazima kutojisomea vitabu ukiendelea, tutajikuta tukiwa na taifa lisilokuwa na watu wenye uelewa wa kutosha kuhusu mambo mbalimbali yakiwamo hata yale yanayotuzunguka wenyewe.

Kwa hiyo tutafakari, tubadilike kwa kuchukua hatua zinazostahili badala ya kung'ang'ania mtindo wa kwenda na wakati bila kujua huo wakati unatupeleka wapi. Wapo wanaodai kwamba wanakwenda na wakati kwa kupoteza muda kuangalia mambo mbalimbali katika simu na kuacha mengine ya msingi.



### ROBI SAMWEL (MKURUGENZI WA SHIRIKA LA HOPE FOR GIRLS AND WOMEN TANZANIA)

KITAALUMA mimi ni mwalimu ingawa sifundishi na pia kwenye hili swali lako, mimi nitazungumzia mazingira ya vijijini ambayo nina uzoefu nayo, kwamba kinachochangia wanafunzi kutojisomea, ni malezi na makuzi kutoka kwa wazazi na walezi.

Ukifuatilia maeneo mengi ya vijijini utabaini kwamba mtoto wa kike ni mtu wa kufanya kazi za nyumbani mara anapotoka shule, hapewi nafasi ya kujisomea, badala yake wanatumwa kuchota, kupika na shughuli nyingine zote za nyumbani, huku mtoto wa kiume akienda kuchunga ng'ombe au kucheza mpira.

Kwa hali kama hiyo hakuna mwenye nafasi ya kujisomea.

Nikufahamishe kuwa bahati mbaya sana wapo baadhi ya wazazi na walezi ambao hawakubahatika hata kusoma darasa la kwanza, watu wa aina hiyo hawana habari kabisa na elimu.

Umefika wakati sasa kuwapo na uhamasishaji kwenye jamii kuhusu umuhimu wa elimu ili hata wazazi ambao hawakubahatika kusoma, waelewe na kuwaacha watoto wawe muda wa kujisomea mara wanapotoka shuleni, badala ya kuwapa majukumu mengine na kusababisha wakose hata dakika chache za kupitia kile walichofundishwa shuleni.

Hakuna chochote kinachoweza kumkomboa katika maisha zaidi ya elimu.



### JOHN PIUS (MHITIMU CHUO KIKUU HURIA DAR ES SALAAM)

YAPO mambo mengi tu ambayo yamechangia kuwapo kwa hali hii, mojawapo likiwa ni uzembe wa wanafunzi wenyewe kwa kutopenda kujishughulisha, huku wakipoteza muda kwa mambo ya ovyo na kusahau kwamba elimu ndiyo ufunguo wa maisha.

Unajua inashangaza sana, kwani wakati ninakuwa, niliambiwa kuwa zamani wanafunzi hata wa darasa la nne walikuwa wanajisomea, lakini siku hizi hadi wa sekondari wanahimizwa kujisomea! Tunakwenda wapi na taifa hili litakuwa la wasomi wa aina gani hapo baadaye?

Unakuta hata mwanafunzi wa sekondari anahimizwa kujisomea kana kwamba hajui umuhimu wa elimu.

Ninadhani kuna kosa ambalo tunatakiwa kulitambua na kuwasaidia watoto wetu ili waweze kuelewa maana ya elimu na kutenga muda wa kujisomea kuliko kuwaacha wajifanyie wanavyotaka na mwisho wanakuwa hawana kitu kichwani.

Mwanafunzi anapofika sekondari, jamii inaamini kwamba angalau anajielewa na anaelewa maana ya elimu, lakini ninasikitika kusema kuwa watoto wa kizazi hiki baadhi yao hawajui hadi wasukumwe ndipo washike vitabu au daftari kujisomea wawapo nyumbani.

Wanaamini wakishatoka shule au twisheni hakuna haja ya kujisomea, wenye mawazo kama hayo wanajidanganya, wazazi na walezi wao wanatakiwa kuwakumbusha kuwa safari ya elimu ni ndefu inayohitaji mbinu nyingi.



### CONSOLATHA MVUNGI (MWALIMU BONGA S/M BABATI, MANYARA)

KWA hili ni lazima tukubali kwamba tumeacha njia na sasa tunakwenda tunakojua wenyewe, ingawa ni kweli kwamba kuna changamoto nyingi kwenye elimu, lakini nyingine ziko ndani ya uwezo wa wanafunzi wenyewe na wazazi wao.

Lakini bahati mbaya sana ni kwamba baadhi ya wazazi hawafuatilii maendeleo ya watoto wao shuleni na ndiyo hao ambao hata wakiwamo watoto wao wanapoteza muda kwa kuangalia televisheni, huwa hawawakatazi, wanaona ni jambo la kawaida mtoto kupoteza muda kuangalia televisheni badala ya kujisomea.

Wazazi wa aina hiyo na wanafunzi wao ndiyo wanaotegemea twisheni kama njia ya kumfanya mwanafunzi afaulu na kusahau kuwa pamoja na twisheni, bado kuna juhudi binafsi katika masomo, ambazo mwanafunzi anatakiwa kuonyesha, hasa kutenga muda wa kutosha kujisomea.

Wanafunzi kuamini kuwa twisheni pekee ndizo zinazoweza kuwasaidia katika masomo bila wao kujituma ni makosa ya kiufundi katika elimu.

Ninatambua kuwa ugumu wa maisha ni changamoto kwa baadhi ya watu na wamekuwa wakipoteza muda mwingi kutafuta chochote kwa ajili ya familia na kukosa nafasi ya kukagua au kujua maendeleo ya watoto wao.



# Polisi yaonya uchaguzi S/Mitaa

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limeonya kuwa halitamvumilia mtu au kikundi chochote ambacho kitajihusisha kuvuruga mchakato wa uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajia kufanyika nchini Novemba 24, mwaka huu.

Onyo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, wakati akizungumzia kuhusiana na hali ya ulinzi na usalama wakati wa kampeni hadi zitakapohitimishwa Novemba 23.

Alisema jeshi hilo limejipanga kuhakikisha uchaguzi huo unafanyika kwa amani na tayari limetayarisha askari wa kutosha kwa ajili ya kulinda mikutano ya kampeni inayoendelea hadi pale litakapohitishwa siku ya uchaguzi.

Alisema hakuna haja ya wananchi kuogopa kushiriki kwenye kampeni au kupiga kura kwani hali ya ulinzi na usalama imeimarika huku akiwataka kuripoti polisi haraka wakihisi kuna vitendo vinavyoweza kuhatarisha amani au kuathiri zoezi la mchakato wa uchaguzi.

Kwa mujibu wa Matei, kampeni zinaendelea katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Mbeya na kwamba katika maeneo hayo wameimarisha ulinzi na usalama.




Wafanyakazi wa kampuni ya ujenzi ya DJ Lwamlema Investment ya jijini Mbeya, wakiweka alama za usalama barabarani katika Barabara ya Mbeya – Chunya, eneo la Kawetere juzi, ili kupunguza matukio ya ajali za barabarani. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wahitimu kilimo vyuo vikuu washauriwa kulima kisasa

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WAHITIMU wa fani ya kilimo kutoka vyuo vikuu nchini, wameshauriwa kuitumia elimu yao kuisaidia jamii kulima kilimo cha kisasa kwa kuandaa mashamba darasa na shiriki kwenye kilimo badala ya kubaki na nadharia pekee.

Ushauri huo ulitolewa jana na wahitimu wa Shahada ya Kilimo kutoka katika Chuo cha Sokoine cha Kilimo (SUA) mkoani Morogoro ambao wameungana na kuanzisha kilimo cha nyanya na pilipili katika eneo la Sae jijini Mbeya.

Mwenyekiti wa kikundi hicho, Mdaila Dalidali, alisema kikundi hicho kina wanachama watano ambao wameamua kujiajiri kwenye sekta hiyo badala ya kusubiri kuajiriwa serikalini ama kwenye kampuni na taasisi binafsi.

Alisema wanazalisha mazao hayo kwa kutumia teknolojia ya umwagiliaji kwa njia ya matone na kwamba makundi mbalimbali ya wakulima wanaenda katika eneo hilo kwa ajili ya kujifunza mbinu wanazotumia kuzalisha ili na wao wakazitumie.

Alisema kutokana na tathmini waliyoifanya, wamebaini endapo wasomi wengine wataanzisha vikundi na kuanzisha mashamba darasa wakulima wengi watanufaika na elimu ya kilimo na kuongeza tija kwenye uzalishaji.

"Tunawashauri vijana wenzetu kufanya vitu kama tunavyofanya hapa, hii itasaidia kuondokana na dhana kwamba wasomi tunafanya kilimo cha kwenye makaratasi, sisi hapa tunafanya kitu ambacho ni uhalisia wa kile tulichojifunza," alisema Dalidali.

Alisema mbali na kilimo hicho kutumika kama mashamba darasa ya kufundishia wananchi wengine, lakini kinawakwamua kiuchumi kwa kuyauza mazao wanayozalisha na kuyatumia kwa ajili ya chakula.

Naye Lulendi Sabi, mmoja wa wanakikundi hao, alisema wanatumia mbegu bora kwenye uzalishaji ili kuwaonyesha wananchi kuwa wakitumia mbegu hizo zina tija zaidi kuliko zile za kienyeji.

Alisema wana mbegu za nyanya ambazo zinazaa mpaka tani 30 kwa ekari endapo mkulima ataunza vizuri shamba lake kulingana na maelekezo ya wataalamu.

Sabi alisema mazao hayo ni mengi hasa ikilinganishwa na mbegu za kienyeji zinazotumiwa na wananchi na hivyo akawashauri kutumia mbegu hizo.

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Adam Mhagama, aliwataka vijana kujiunga kwenye vikundi na kuomba mikopo inayotolewa na halmashauri kwa vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ili waitumie kwenye shughuli za uzalishaji.

**"Tunawashauri vijana wenzetu kufanya vitu kama tunavyofanya hapa, hii itasaidia kuondokana na dhana kwamba wasomi tunafanya kilimo cha kwenye makaratasi, sisi hapa tunafanya kitu ambacho ni uhalisia wa kile tulichojifunza," alisema Dalidali.**

# Wananchi ruksa kuchimba barabara hifadhini Kitulo

**Na Nebart Msokwa, BUSOKELO**

SERIKALI kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii imewaruhusu wananchi wa Bonde la Mwakaleli kuendelea kuchimba barabara kuunganisha mkoa wa Mbeya na Njombe kupitia Hifadhi ya Kitulo ambayo awali walisimamishwa kwa madai kuwa haipaswi kupita katikati ya hifadhi.

Aprili mwaka jana, wananchi wa Bonde la Mwakaleli kwa kushirikiana na Mbunge wao wa Busokelo, Atupele Mwakibete, walianza kuchimba barabara hiyo kwa ajili ya kuitumia kwa madai kuwa itawasaidia kupunguza umbali wa kufika kwa majirani zao wa Makete ambao kwa sasa wanalazimika kusafiri zaidi ya kilometa 150, lakini kwa kutumia barabara hiyo hivyo umbali huo utapungua na kubakia takribani kilometa 40.

Akizungumza kwenye mkutano wa hadhara wa ujirani mwema, katika kijiji cha Kandete, Mbunge huyo alisema baada ya kufanya mazungumzo na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (Tanapa) kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, serikali imeridhia barabara hiyo iendelee kuchimbwa ili isaidie kusukuma mbele maendeleo ya wananchi.

"Mwaka jana tulianza kufungua barabara kwa jembe la mkono kutoka hapa kwenda Makete, lakini tulisimamishwa kwa vile ilionekana kuwa barabara hiyo itapita ndani ya hifadhi kinyume na sheria, lakini baada ya serikali kuona umuhimu wake, imeturuhusu tuendelee kuilima na sasa ni ruksa kuiendeleza," alisema Mwakibete.

Alisema barabara hiyo ikikamilika itasaidia kuinua uchumi wa wananchi wa Jimbo zima la Busokelo kwa vile watakuwa na fursa nzuri ya kusafirisha kirahisi mazao yao kwenda kuuza kwa jirani zao wa Makete.

Mwakibete alisema barabara hiyo pia itawasaidia wananchi wanaokwenda kupata matibabu kwenye Hospitali ya Ikonda ambayo imekuwa ikihudumia wananchi wa eneo hilo.

Akizungumza kwenye mkutano, Kamishna Msaidizi wa Tanapa, ambaye ni Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Kitulo, Theodora Alloys, aliwataka wananchi kutumia barabara hiyo kwa manufaa yao na taifa kwa ujumla.

Alisema wananchi kwa kutumia barabara hiyo wawe sehemu ya ulinzi wa hifadhi ya Taifa Kitulo kwa kudhibiti matukio ya uchomaji moto misitu, ujangili na kuinga vitendo vyovyote vya uharibifu wa mazingira.


"Barabara hii ambayo mmeruhusiwa kuiendeleza mnapaswa kuitumia vizuri ili iendelee kuleta uhusiano mzuri baina yenu na hifadhi, kamwe msikubali baadhi ya watu kuitumia kwenda kufanya ujangili wa kuwinda wanyama ndani ya hifadhi, kuanzisha mioto au kukata miti ovyo," alisema Alloys.

Alloys alisema baada ya barabara hiyo kufunguliwa, itatumiwa pia na watalii kuingia ndani ya hifadhi, hivyo akawataka wananchi wa eneo hilo kujiandaa kunufaika kiuchumi kwa kuandaa bidhaa za asili ambazo zinapendwa na watalii.

Aliwashauri wananchi hao kuanza kutengeneza bidhaa za asili kama vile mikeka, vyungu na kuboresha ngoma za utamaduni wa asili ambazo huwa ni kivutio kikubwa cha watalii akidai kuwa bidhaa hizo zinaweza kuwaingizia uchumi mkubwa.

Baadhi ya wananchi wameiomba serikali kuwasaidia kujenga madaraja na makaravati kwenye maeneo korofi ya barabara hiyo ili kuhakikisha inaanza kupitika mapema.

Daniel Mwambega, mkazi wa Kata ya Luteba, alisema kuwa kutokana na uhitaji wa barabara hiyo, wananchi wako tayari kujitolea kuilima kwa jembe la mkono na watahakikisha inakamilika haraka iwezekanavyo.





# TLS yawaita waathirika ajali za barabarani

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

CHAMA cha Wanasheria Tanganyika (TLS), kimewataka waathirika wa ajali za barabarani kujitokeza ili kupata haki zao katika kampuni mbalimbali za bima ambazo gari husika limekatia bima.

Aidha, TLS imewasisitiza waathirika wa ajali hizo kutoa taarifa ya matatizo wanayopata wakati wa ufuatiliaji wa stahiki za malipo yao wanazotakiwa kulipwa baada ya kupata ajali.

Ofisa programu wa chama hiko na msimamizi wa mradi wa usalama barabarani, Markphason Buberwa, alisema TLS ipo kwa ajili ya kuwasaidia waathirika wa ajali za barabarani ambao wengi wamekuwa wakikata tamaa kutokana na usumbufu wanaopata katika ufuatiliaji wa malipo ya ajali walizopata.

"Tunaomba waathirika wajenge utaratibu wa kutoa taarifa katika ofisi za TLS, tutawasaidia jinsi ya kupata haki zao kupitia sheria," alisema Buberwa.

Alisema wamekuwa wakisikia changamoto nyingi, lakini bado hazijawafikia wao ili wazifanyie kazi kisheria na wahusika wapate haki zao za msingi.

Alifafanua lengo lao ni kuona kila mmoja anapata haki yake ya msingi kutokana na majeraha au ulemavu aliosababishiwa kupitia ajali za barabarani.

Alisema takwimu za kipolisi zinaonyesha jumla ya watu 18,000 ni waathirika wa barabarani, jambo ambalo halikubaliki na linahitaji kupingwa kwa kiasi kikubwa.

Akitoa ufafanuzi, CPL Martine Mangu, kutoka Ofisi ya Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani Dawati la Elimi kwa Umma, alisema asilimia 76, ya ajali za barabarani ni makosa ya kibinadamu, wakati asilimia 72, ni makosa ya madereva na asilimia nne zinachangiwa na watembea kwa miguu na nane husababishwa na ubovu wa miundombinu na asilimia 16, zinachangiwa na magari mabovu.

Kutokana na hali hiyo, alisema elimu ya usalama barabarani inapaswa kutolewa ili kupunguza ajali ikiwamo kuzitokomeza kabisa.

Alisema madereva wanapaswa kuwa makini ili kuokoa maisha ya raia wanaotembea kwa miguu.

Mmoja wa waathirika wa ajali, Kombo Jumbe, alisema ajali nyingi zinazotokea huchangia kwa kiasi kikubwa kupoteza ndoto za jamii kwa ujumla.

**"Tunaomba waathirika wajenge utaratibu wa kutoa taarifa katika ofisi za TLS, tutawasaidia jinsi ya kupata haki zao kupitia sheria," alisema Buberwa.**

# Wito kwa wadau wa petroli kuandaa programu endelevu

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

UMOJA wa Wahandisi wa Petroli Tanzania (SPE) umeitaka serikali kuwashirikisha wadau wote wanaohusika na masuala ya petroli ili kuandaa programu endelevu ambayo itasaidia kampuni za mafuta na gesi kuchukua wahitimu wa vyuo nchini kila mwaka na kuwajengea uwezo ili kukidhi soko la ajira la ndani na kimataifa.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Mwenyekiti wa umoja huo, Martha Kamuzora, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye ufunguzi wa kongamano la kujadili umuhimu wa sekta ya nishati katika kukuza ajira kwa vijana.

Kongamano hilo ambalo lilishirikisha wadau mbalimbali wakiwamo wanafunzi wa vyuo vikuu, ambavyo vinatoa shahada ya mafuta na gesi nchini kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo cha Madini na DIT.

Kamuzora alisema programu hiyo itasaidia chuo kujua wanafunzi wangapi wametoka, na kampuni kutambua kuna nafasi ngapi hali ambayo itasaidia wataalamu kutoka viwandani kwenda vyuoni na kuchukua wahitimu wa masomo ya mafuta na gesi. Alisema serikali ishirikiane na umoja huo, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), vyuo pamoja na wadau wengine ili kuanza mchakato wa kuangalia mitaala na namna ya ufundishaji kisha kupanga mfumo mzuri ambao utawezesha wanafunzi kupata ujuzi kwa vitendo katika kampuni husika.

"Kuwe na mfumo wa aina hiyo, ambao wenzetu nchi za nje wameweza kuwa na mkataba na sekta binafsi, yaani serikali, sekta binafsi pamoja na vyuo wamekuwa na maamuzi ya pamoja wanashirikishana kila kitu, lakini hapa kwetu chuo kipo chenyewe, serikali yenyewe, sekta binafsi yenyewe hakuna muunganiko wowote," alisema Kamuzora.

Akifungua kongamano hilo Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, alisema serikali inahakikisha wahitimu hao wanashiriki moja kwa moja katika ujenzi na ustawi wa Taifa kupitia ujuzi walioupata katika vyuo.

Alisema kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2014 za ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS ) zilizofanyiwa marejeo Juni 2019, Tanzania ina takribani ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi milioni 24.5 ambapo kati ya hao wenye ujuzi wa juu ni asilimia (3.6), ujuzi wa kati (16.5) na ujuzi wa chini ni asilimia (79.9).

Alisema ili nchi kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, kigezo cha kwanza ni kuwa na nguvu kazi yenye ujuzi wa juu asilimia (12), ujuzi wa kati asilimia 34, ujuzi wa chini asilimia 54, hivyo ni lazima serikali pamoja na wadau mbalimbali wajikite kuwaandaa wataalamu kupitia wahitimu wa vyuo pamoja na wale waliopo vyuoni.

"Takwimu zinaonyesha kuwa kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati asilimia 59, ya wahitimu wa Vyuo Vikuu wanakwenda kwenye soko la ajira wakiwa wameivishwa nusu, sasa serikali tumeamua kuchukua hatua za kuwaivisha wahitimu wa vyuo vyetu," alisema Mavunde.



Mwandishi mwandamizi wa taarifa rasmi za Bunge, kutoka Ofisi ya Bunge, Patson Sobha (kushoto), akitoa mafunzo kwa wajumbe wanaoshiriki katika Bunge la Vijana 2019, lililoanza katika ukumbi wa Msekwa, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: BUNGE**

# Mwinyi aeleza sababu kuwapo amani nchini

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

WAZIRI wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Husein Mwinyi, amesema amani iliyopo nchini haitokani na ukubwa wa majeshi au wingi wa askari, ila inatokana na utulivu wa wananchi wenyewe.

Kauli hiyo aliitoa juzi wakati wa sherehe za Maulidi zilizofanyika kwenye msikiti wa Dodoma Sunni Nunge, jijini humo.

"Wapo watu wanaodhani kuwa ukiwa na majeshi makubwa au ukiwa na polisi wengi ndipo utakapopata amani vyombo vya ulinzi na usalama havileti amani, wanaoleta amani ni wananchi wenyewe," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema yapo mataifa ambayo yalikuwa na amani na majeshi mengi, lakini walipoichezea wameingia kwenye vita na machafuko ambayo hayajulikani mwisho wake utakuwa lini.

Aliyataja baadhi ya mataifa yaliyoingia kwenye machafuko baada ya wananchi wake kuiondoa amani na sasa hawana amani ni Libya, Siria, Algeria, Sierra Leone, DRC, Yemen, Sudan na Sudan Kusini.

"Sasa sisi Mwenyezi Mungu ametujalia amani ndani ya nchi yetu, kwa hivyo tujitahidi kuilinda ili kufanya mambo yetu ya kimaendeleo, lakini na kufanya ibada kwa utulivu kama hivi," alisema.

Aidha, Waziri Mwinyi alisema ili amani inapatikane inahitaji malezi bora kuanzia kwa watoto, vijana na watu wengine ndipo utulivu unakuwapo.

Naye Imamu wa Msikiti wa Dodoma Sunni Jamaat Nunge, Shekhe Ahmed Zuberi, aliwataka wananchi kuitafuta elimu kwa sababu kuna hazina ya vitu vingi katika kujifunza.

Alisema elimu ina gharama kubwa, hivyo inapotokea kuikosa mtu ananafasi ya kujifunza basi ajiendeleze zaidi ili kupanua uelewa wa masomo na maisha.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdala Ulega, aliwaasa wananchi kupenda kufanya ibada kila mtu na dini yake ili kuwa na wananchi wenye hofu ya Mungu na upendo kwa wote.

Ulega alisema serikali inawataka wananchi wake kufanya kazi ili kujiletea mafanikio ya uchumi katika familia zao.



# SMZ yaaswa mikataba ya mafuta, gesi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), imeshauriwa kuwa makini inapoingia makubaliano ya kibiashara ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia kwa lengo la kunusuru athari za kimazingira hasa kipindi cha uzalishaji.

Akiwasilisha mada ya mgawanyo wa mapato ya mafuta katika mafunzo kuhusu mafuta na gesi asilia kwa wanasheria wa serikali, Mshauri Mwelekezi wa Mafuta na Gesi, Yona Killagane, alisema uchimbaji wa mafuta unatumia fedha nyingi, hivyo bila kuwa na uamuzi wenye maslahi ya taifa, unaweza kusababisha serikali kuingia hasara.

Killagana alisema nchi nyingi zinazoendelea zinaingia hasara kwa kukosa sera makini, hivyo kuwataka kufahamu majukumu yao katika kuhakikisha wanakuwa na mipango imara ya kulinda sekta hiyo.

"Sekta hii si ya kudumu, hivyo inahitaji umakini mkubwa wa kusimamiwa ili nchi ipate faida na ninyi wanasheria mnapaswa kufahamu mfumo wa makubaliano mtakapopata fursa ya kutoa uamuzi katika usimamizi na uendelezaji wa sekta hii,"alisema.

Pia aliishauri Mamlaka ya Udhibiti na Utafutaji Mafuta na Gesi Asilia (ZPDC) kuhakikisha watakapopata mikataba ya kutafuta na kuchimba mafuta, isiingie katika mfumo wa kukodi majengo au vifaa kwa kuwa watakapomaliza watashindwa kunufaika na gharama zinazoweza kutumiwa.

Naye Mhandisi Mshauri kutoka kampuni ya Environmental Bench Mark, Venant Rwenyagira, alisema ni vyema Zanzibar ikahakikisha inasimamia vyema misingi ya usimamizi wa mazingira katika shughuli hiyo hasa katika kukabiliana na athari zinazoweza kutokea kipidi cha utafutaji na uchimbaji wa mafuta.

Alisema taasisi za sheria na mamalaka za mazingira pia zinapaswa kushirikishana na wadau mbalimbali ili kupata uamuzi wa pamoja katika utungaji wa sera na usimamzi wa miradi.

"Ingawa bado masuala ya kimazingra hayajapewa kipaumbele sana ni muhimu kuwa na mitazamo hiyo kwa kuangalia nafasi za kila mdau wa sekta husika ili kurahisisha utekelezaji wa kazi hiyo na pia tathmini za kimazingira ziwapo wazi ili kila mdau afaidike," alisema.

Aliishauri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuzingatia sera na sheria za kimataifa ziende sambamba ili kuzuia uchafuzi wa mazingira na kuwasimamia vyema makandarasi kuheshimu na kuchukua tahadhari na taratibu zote za mikataba na sheria za nchi.

Mkurugenzi wa Huduma za Ushauri, Usimamaizi wa Mikataba, Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa, Fatma Saleh, alisema utafiti mbalimbali umeshafanyika kwa ajili kutafuta gesi na mafuta.



Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Hassan Khatib (kushoto), akisalimiana na wakuu wa vikosi vya ulinzi na usalama vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, baada ya kumaliza kikao na watendaji pamoja na wafanyabiashara wa Baraza la Manispaa la Mji wa Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mashamba 1,350 ya serikali yatambuliwa

**Na Rahma Suleiman,ZANZIBAR**

MASHAMBA 1,356 ya serikali yametambuliwa katika wilaya nne za Pemba ambayo awali yalikuwa yakishikiliwa kinyume cha sheria na watu binafsi.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Hemed Suleiman, alisema hayo jana wakati akiwasilisha taarifa ya awali ya ripoti ya kamati ya kitaifa ya kuhakiki na kutambuwa mashamba ya serikali ambayo yamefichwa na wananchi na kuyamiliki kinyume cha sheria.

Alisema awali kamati hiyo ilipewa jukumu la kuyatambuwa mashamba 1,510 huku mengine 154 yakitafutwa.

"Kamati yetu ya kuhakiki na kutambua mali za serikali imeyatambua mashamba 1,356. Kwa sasa yako mashamba 154 hatujayatambuwa na tunayatafuta," alisema.

Suleiman alisema mashamba yaliyokuwa yakitafutwa ni yale ambayo awali umiliki wake ulikuwa chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ).

Alisema mashamba hayo yalichukuliwa kinyume cha sheria na baadhi ya wananchi na kuanza kujimilikisha na kuvuna mali mbalimbali.

Hata hivyo, Suleiman alikiri kwamba kamati hiyo chini ya mawaziri waandamizi ilipata changamoto mbalimbali katika kuyatafuta mashamba hayo na kuyahakiki.

Alisema baadhi ya watendaji wa serikali walionesha dharau na kushindwa kutoa ushirikiano katika kuyatambua mashamba hayo.

Sambamba na hilo, alisema kamati hiyo imefanikiwa kuyatambua baadhi ya mashamba baada ya kuzipata nyaraka zinazoonesha nani mmiliki halali.

"Tunashukuru nyaraka za mashamba zimetusaidia kwa kiasi kikubwa kuyatambua mashamba ya serikali yaliyofichwa na watu binafsi na tumeyatambua," alisema.

Naye Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, aliipongeza kamati hiyo kwa kufanya kazi ya kizalendo na hatimaye mali za serikali zimepatikana.

Alizitaka Wizara husika kuhakikisha mali zote za serikali zinaorodheshwa na kuhakikiwa kwa ajili ya kuepuka matukio yanayoweza kusababisha upotevu.

"Tunazo taasisi zilizopewa jukumu la kuhakiki mali za serikali huu ndio wakati wao wa kuyatambua mashamba hayo na kuyaingiza katika kumbukumbu halisi,' alisema.

Kwa upande wake Waziri Asiye na Wizara Maalum, Juma Ali Khatib, aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kuhakikisha mashamba ya serikali yaliyofichwa yanapatikana na kurudi katika umiliki wa serikali.

# Ataka utaratibu ukusanyaji kodi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Hassan Khatib Hassan, ameutaka uongozi wa manispaa ya Mjini Unguja kuandaa utaratibu maalum wa ukusanyaji wa kodi ili kupunguza mwanya wa upotevu wa mapato.

Hassan aliyasema hayo jana katika mkutano maalum na wafanyabiashara wa vyakula wa Manispaa ulioshirikisha viongonzi wa manispaa hiyo ulifanyika katika ofisi ya mamlaka hiyo.

Alisema wakati umefika kwa uongozi wa manispaa hiyo kuona umuhimu kwa wafanyabiashara kutumia taasisi za kibenki kulingana na biashara zao kwa watendaji na wafanyabiashara hao na pengine kukosa mapato.

"Tuandae utaratibu maalum kwa wafanyabiashara wetu wakalipe benki au hata hapo ofisini kwenu kwa kutumia mashine maalum," alisema Hassan.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara wa vyakula kuimarisha usafi wa mazingira katika maeneo ya kazi ili kuepusha mlipuko wa kipindupindu.

"Biashara zetu haziko vizuri kwanza sisi wenyewe wengi wetu hatuko wasafi lakini pia mazingira yanayotuzunguka si safi. Tujitahidi bado hatuko salama sana na maradhi ya kipindupindu," .alisema.

Hata hivyo, alisema serikali ya mkoa itaendelea kuwa karibu na wafanyabiashara wadogo kwa kuwaandalia mazingira mazuri ili kukuza kipato chao na kujiimarisha kiuchumi.

Naye Mkurugenzi wa Manispaa, Said Juma Ahmada, alisema uongozi wa manispaa hiyo umeshaanza utaratibu wa malipo kwa kutumia taasisi za kibenki licha ya changamoto wanazozipata kutoka kwa wafanyabiashara hao.

Alisema wataendelea kuzitumia kanuni zilizopo kwa kutoa adhabu ya papo kwa papo na kwamba wananchi waendelee kuzingatia taratibu na sheria za kuimarisha usafi na kupunguza kufanya makosa ili kuendelea kuweka mji katika mazingira mazuri.

**"Biashara zetu haziko vizuri kwanza sisi wenyewe wengi wetu hatuko wasafi lakini pia mazingira yanayotuzunguka si safi. Tujitahidi bado hatuko salama sana na maradhi ya kipindupindu," .alisema.**

# Mpango kupunguza vifo mama na mtoto

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

WIZARA ya Afya imezindua mradi wa huduma za uzazi wa mpango kisiwani Pemba, wenye lengo la kupunguza vifo na mama na mtoto pamoja na kuboresha afya.

Mradi huo unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Uingereza, utatekelezwa kwa miaka mitano.

Akizindua mradi huo Gombani Chakechake, Mkurugenzi wa Kinga na Elimu ya Afya Zanzibar, Fadhil Mohamed Abdalla, alisema huduma za uzazi wa mpango zitatolewa katika vituo vyote vya afya vilivyopo Unguja na Pemba.

Alisema uzazi wa mpango pekee unapunguza vifo kwa asilimia 30, hivyo ipo haja kwa jamii kushirikiana pamoja katika kuhakikisha kinamama wanatumia huduma ya uzazi wa mpango, ili kuepusha vifo na kuboresha afya ya mama na mtoto.

"Hali ya matumizi ya uzazi wa mpango sio nzuri kwa Zanzibar, hivyo sio rahisi kupunguza vifo vya mama na mtoto, huduma hii ni muhimu sana, kwa hiyo kinamama tumieni uzazi wa mpango ili tupunguze vifo," alisema mkurugenzi huyo.

Alieleza kwa upande wa Unguja ni asilimia 14 tu ya kinamama wanaotumia huduma ya uzazi wa mpango na kwa Pemba ni asilimia 7 tu, jambo ambalo limesababisha kutokea vifo 191 kwa kila vizazi hai laki moja kwa mwaka.

Aliitaka jamii kuondoa dhana potofu ya kwamba kutumia njia za uzazi wa mpango ni madhara, ambapo alisema kuwa huduma hizo ni salama.

"Huduma ya kutumia uzazi wa mpango ni salama, haina madhara yoyote kwa kinamama hawa, hivyo tuondoe shaka hiyo, tuwahamasishe kinamama watumie ili wawe na afya bora pamoja na mtoto," alisema.

Aidha, alieleza kuwa serikali imeimarisha miundombinu katika vituo vya afya Unguja na Pemba kwa lengo la kuwapatia huduma bora kinamama wajawazito, hivyo ni vyema wakatumia fursa hiyo kwa ajili ya kujipatia huduma.

Mkurugenzi wa mradi huo, Moke Magom, alisema una lengo la kuboresha afya ya mama na mtoto ambao utafanyika vituo vyote vya Zanzibar.

"Tunataka afya ya mama iwe bora wakati wa ujauzito, kujifungua na kuhakikisha mtoto anapata makuzi bora zaidi, ili awe na afya njema," alisema.

Mapema Ofisa Mdhamini Wizara ya Afya, Shadya Shaaban Seif, alisema huduma hizo zinatolewa bila ya malipo katika vituo vyote vya afya na kuwataka kinamama kwenda kupata huduma ya ya uzazi wa mpango, ili kujenga afya bora.

Akitoa maelezo baada ya kusoma Qur-an Sheikh Said Abdalla Nassor kutoka Samael, alisema suala la uzazi wa mpango limeelezwa katika Qur-an tukufu ili kulinda afya ya mama.

# Wenye ualbino wahofia uchaguzi

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

WATU wenye ualbino mkoani Shinyanga, wameeleza kuingiwa na hofu ya kudhuriwa kuelekea kwenye uchaguzi mkuu mwakani, wakidai kila uchaguzi unapofika ndipo wimbi la mauaji dhidi yao hutekelezwa.

Walibainisha hayo jana kwenye mafunzo ya kuwajengea uwezo watu wenye ualbino pamoja na wazazi ambao wamezaa watoto wa aina hiyo, ili kwenda kutoa elimu kwa jamii kuondoa unyanyapaa dhidi yao. Mafunzo ambayo yametolewa na Shirika la Under The Same Sun ambalo linatetea haki za watu wenye ualbino nchini.

Walisema kinapofika kipindi cha uchaguzi hasa uchaguzi mkuu ndipo mauaji ya watu wenye ualbino huanza kutokea na kuiomba serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani kuimarisha ulinzi dhidi yao.

Yunis Manumbu, alisema wameanza kuingiwa na hofu kwenye kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu mwakani, na kuiomba serikali idhibiti mauaji hayo pamoja na waganga wa kienyeji kuacha kupiga ramli chonganishi.

Naye mzazi ambaye amezaa mtoto mwenye ualbino, Leokadia Bulugu, mkazi wa Ndala Shinyanga Mjini, alisema jamii imeshaanza kumtisha na kumwambia kipindi cha uchaguzi kimefika, hivyo atafute mahali pa kumpeleka kumficha mtoto wake na asipofanya hivyo atauawa.

"Naiomba serikali iimarishe ulinzi wa kutosha kwa watu wenye ualbino kuelekea kwenye kipindi cha uchaguzi mkuu mwakani, sababu hofu imeanza kutanda nikiwamo na mimi kuhofia mtoto wangu kuuawa, ambapo jamii imeshaanza kuniambia nikamfiche ili asiuawe," alisema Bulugu.

Naye mgeni rasmi kwenye ufunguzi wa mafunzo hayo, Ofisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Shinyanga, Lilian Kiyenze, aliyemwakilisha Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Shinyanga, Lydia Kwesigabo, aliitaka jamii kuacha kunyanyapaa watu wenye ualbino, bali wawaone wapo sawa kama binadamu wengine.

Ofisa mradi wa kujengea uelewa watu wenye ualbino juu ya kwenda kutoa elimu kwa jamii kuacha kuwanyanyapaa, Grace Wabanu kutoka Under The Same Sun, alisema mradi huo utatekelezwa mkoani Mwanza na Shinyanga ili kutokomeza kabisa ukatili dhidi yao.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NIC Tanzania Limited, Margaret Karume (kushoto), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 4.7 kwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Loyola jijini Dar es Salaam, Father Ubwanda Meyo, katika sherehe ya mahafali ya kidato cha nne shuleni hapo, ikiwa ni mchango wa kununulia magodoro 100 kwa ajili ya mabweni ya wasichana jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vyuo vya maendeleo ya jamii vyapewa somo ajira

**Na Idda Mushi, MOROGORO**

KATIBU Mkuu Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, ameitaka vyuo na taasisi za maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii kutoa elimu itakayowasaidia wahitimu kuleta mabadiliko katika jamii zao na kujiajiri na kuajiri watu wengine kuliko kutegemea kuajiriwa.

Dk. Jingu ameyasema haya jana mkoani Morogoro wakati akifungua kikao kazi cha wakuu wa Vyuo na Taasisi za Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii nchini kilicholenga kubadilishana uzoefu kwa wakuu hao wa vyuo katika utendaji kazi na kujengeana uwezo ili taasisi na vyuo viweze kufanikisha malengo ya Taifa.

Alisema taaluma ya maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii lazima iwe nyenzo ya kutatua changamoto zilizopo katika jamii ikiwamo tatizo la ajira kwa vijana kwa kutoa taaluma itakayowapa fursa wahitimu kujiajiri kutokana na taaluma waliyopata.

"Umefika wakati sasa taasisi na vyuo kuja na mpango mkakati wa namna ya kutekeleza dhana ya kujiajiri kwa lengo la kuzalisha wahitimu mahiri," alisema Dk. Jingu.

Ameongeza kuwa vyuo vya maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii vimetoa mchango mkubwa sana katika kutatua changamoto za jamii, hivyo jamii kuthamini uwapo wa vyuo katika jamii na mafanikio yaliyoonekana kwa vyuo hivyo yaonekane kwa kila chuo.

Alivitaka vyuo hivyo kuanzisha vituo vya kielektroniki vya ubunifu na maarifa ambao utarahisisha upatikanaji wa maarifa na ujuzi kwa haraka zaidi kuliko kusoma vitabu na itatoa fursa ya kupata maarifa katika muda mfupi.

Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii nchini, Patrick Golwike, alisema ili kujipambanua katika jamii umuhimu wa kada ya maendeleo ya jamii inatakiwa kuwa na mbinu ya namna ambayo vyuo vya maendeleo ya jamii vitatoa wataalamu wakaosaidia kuleta mabadiliko kwa jamii.

Naye Kamishna wa Ustawi wa Jamii nchini, Dk. Naftali Ng'ondi, alisema kada ya ustawi wa jamii ni moja kati

## HABARI KIMATAIFA

### Rais awakemea polisi kuwashambulia waandamanaji

**SANTIAGO,** Chile

KWA mara ya kwanza tangu kuanza kwa maandamano ya kiraia mwezi uliopita nchini Chile, Rais Sebastian Piñera amelaani vurugu zilizosababishwa na Jeshi la Polisi dhidi ya waandamanaji.

"Kulikuwa na matumizi ya nguvu, dhuluma au makosa yalifanywa na haki za wote hazikuheshimiwa," Rais Piñera amekiri katika hotuba iliyorushwa kwenye televisheni kutoka Ikulu ya Rais ya La Moneda.

Mgogoro huo ambao bado unaendelea kuikumba nchi hiyo ya Amerika Kusini tangu Oktoba 18 umeua watu 22, wengi wao katika mikasa ya moto wakati wa uporaji na watano kutokana na matumizi ya nguvu ya vikosi vya usalama, na zaidi ya watu 2,000 wamejeruhiwa.

Kwa mujibu wa Shirika la Kitaifa la Haki za Binadamu (INDH), karibu watu 200 wamepigwa risasi za mpira kwenye macho wakati polisi ilikuwa ikijaribu kutawanya waandamanaji.

Rais Piñera alihakikisha kuwa hakutakuwa na adhabu yoyote, kwa wale ambao walifanya vitendo vya ukatili, akimaanisha uharibifu na uporaji uliotekelezwa na waandamanaji wenye msimamo mkali, pamoja na wale ambao wamefanya dhuluma na uhalifu mwingine, akimaanisha polisi na wanajeshi.

Vitendo vya udhalilishaji, unyanyasaji wa kijinsia, mateso, mashtaka na malalamiko ya ukiukwaji wa haki za binadamu vinavyofanywa na maofisa wa polisi yameongezeka tangu kuanza kwa maandamano, na kusababisha Umoja wa Mataifa (UN) kutuma ujumbe wa uchunguzi kuhusu uhalifu uliotokea nchini humo.

Siku ya Ijumaa, katika maandamano mapya katika mji wa Santiago, katika eneo la Plaza Italia, Jeshi la Polisi ilishtumiwa na mashirika kadhaa ya haki za binadamu kwamba walichelewesha kumsafirisha kijana mmoja hospitali aliyepatwa na mshtuko wa moyo, baada ya kurusha gesi ya machozi dhidi ya wauguzi. **RFI**

# Senegal, Ufaransa kupiga vita uhamiaji haramu

**DAKAR,** Senegal

WAZIRI Mkuu wa Ufaransa, Édouard Philippe yuko mjini Dakar Senegal kwa ziara rasmi ya siku mbili, akiandamana na ujumbe mkubwa wa viongozi wa serikali, wabunge, viongozi wa kampuni, na wawakilishi wa ulimwengu wa utamaduni na michezo.

Ziara hiyo imelenga zaidi usalama katika mkutano unaofunguliwa jijini Dakar mwanzoni mwa wiki na ambao unaonyesha, uhusiano maalumu kati ya Senegal na Ufaransa.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu wa Ufaransa, semina ya kati ya serikali ni zana muhimu.

**Senegal ndio nchi pekee katika ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara ambapo mkutano wa aina hiyo unafanyika.**

Mkutano huo unaofanyika Dakar unafuatia ule uliofanyika jijini Paris Oktoba 2017.

Senegal ndio nchi pekee katika ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara ambapo mkutano wa aina hiyo unafanyika. Hii inaonyesha kwa nchi zote mbili mfano na nguvu ya ushirikiano wao.

Katika nyanja ya uchumi, Ufaransa inasalia kuwa mshirika mkubwa zaidi wa biashara wa Senegal.

Katika masuala ya ulinzi, Senegal, inayochukuliwa kama nchi yenye usalama wa kutosha katika ukanda huo, ambayo imeshirikishwa katika kikosi cha Umoja wa Mataifa nchini Mali licha ya kuwa siyo mwanachama wa G5 Sahel, ina jukumu muhimu kwa kusimamia amani kwa mujibu wa Paris, ambayo inasisitiza kuhusu kutolea mafunzo vikosi vyake vya ulinzi na usalama.

Kwa ziara hiyo ya Édouard Philippe, Senegal na Ufaransa zimetia saini mikataba saba, ikiwa ni pamoja na kuthibitishiwa mkopo wa sera ya umma kutoka kwa Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) wa Euro milioni 50 kuhusu utawala wa kifedha.

Mwingine ni mkataba wa kupewa manuari tatu za doria kwa kikosi cha wanamaji cha Senegal. **RFI**


Distributed via ippmedia

Waandamanaji mjini Hong Kong wakiwa wamevalia viziba sura wakati wakipambana na polisi. **PICHA: REUTERS**

# Waandamanaji Hong Kong washinda kesi

**HONG KONG,** China

MAHAKAMA mjini Hong Kong jana iliamua kuwa amri tata ya kutofunika nyuso kwa kutumia barakoa wakati wa maandamano ni kinyume na katiba.

Uamuzi huo wa mahakama unakuja baada ya makabiliano makali kati ya Jeshi la Polisi na waandamanaji mwishoni mwa juma.

Kulingana na vyombo vya habari, ikiwa ni pamoja na kituo cha radio cha Hong Kong, Mahakama ya mji huo imebaini marufuku hiyo iliyotangazwa chini ya sheria za dharura inakiuka sheria ya msingi na inazuia haki za raia bila sababu ya msingi.

Majaji wawili, Godfrey Lam na Anderson Chow, walisema utekelezaji wa marufuku hiyo unashindwa kuweka uzani kati ya haki za raia zinazopigiwa upatu na hatua zinazochukuliwa kuzuia haki hizo.

Marufuku dhidi ya kufunika nyuso ilitangazwa mwezi Oktoba na kiongozi wa Hong Kong, Carrie Lam, ambaye alianisha lengo lake kuwa ni kusaidia kukabiliana na maandamano ya vurgu yanayoukumba mji huo kwa muda wa miezi kadhaa sasa.

Barakoa au vifunika nyuso vimekuwa vikivaliwa na waandamanaji ili kuzuia kutambuliwa pamoja na sababu za kiusalama kutokana na polisi kutumia kila wakati mabomu ya kutoa machozi na maji ya kuwasha ili kuwatawanya waandamanaji.

Amri hiyo ilihuishwa kutoka sheria ya hali ya hatari wakati wa utawala wa kikoloni wa Uingereza na waandamanaji wengi walikaidi kuitekeleza.

Mwanaharakati mashuhuri wa demokrasia mjini Hong Kong, Joshua Wong ameutaja uamuzi wa mahakama kuwa ushindi wa nadra wa kisheria kwa waandamanaji.

Kuondolewa kwa marufuku ya kufunika nyuso kunakuja baada ya makabiliano makali kati ya waandamanaji na polisi mwishoni mwa juma.

Wakati huo huo, Polisi mjini Hong Kong jana walikivamia Chuo Kikuu kilichokuwa kikidhibitiwa na waandamanaji baada ya kushindwa kuingia kwenye eneo hilo.

Miale ya moto iliyotokana na mfululizo wa milipuko ilionekana kutoka ndani ya majengo pindi maofisa wa polisi wa kutuliza fujo walipoingia kwenye viunga vya chuo hicho jana alfajiri.

Usiku wa manane, polisi walifyatua mara kadhaa mabomu ya kutoa machozi pamoja na kuwarushia waandamanaji maji ya kuwasha nje ya majengo ya chuo kikuu hicho.

Kwa siku kadhaa waandamanaji wanaoipinga serikali walijifungia ndani ya chuo kikuu cha masuala ya ufundi mjini Hong Kong wakipambana kwa kutumia mabomu ya kutengenezwa kwa mafuta pamoja na silaha za jadi.

Kwa mujibu wa polisi waandamanaji walivurumisha mabomu ya kutengenezwa kienyeji na kuchoma moto miundombinu kadhaa.

Machafuko yameongezeka mjini Hong Kong katika wiki za karibuni baada ya waandamanaji kuwatolea wito kufanya vurugu za kiwango cha juu.

Maandamano ya umma mjini Hong Kong ya kudai demokrasia yalianza dhidi ya sheria tata ya kupeleka wahalifu upande wa China Bara na tangu wakati huo maandamano hayo yamegeuka kuwa madai ya kufanyika mageuzi ya kidemokrasia na uchunguzi huru kuhusu unyanyasaji wa polisi. **DW**

# Tancoal yampongeza JPM kuleta mapinduzi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya kuzalisha makaa ya mawe (Tancoal) imempongeza Rais John Magufuli kwa kuleta mapinduzi chanya kwenye sekta ya madini nchini katika kipindi cha miaka minne ya utawala wake.

Taarifa iliyotolewa jana na kampuni hiyo ilieleza kuwa katika kipindi cha miaka minne imeongeza uzalishaji wa makaa ya mawe nchini.

"Tancoal imeuza tani 237,735.93 za makaa ya mawe katika kipindi cha Julai 2014 hadi Juni 2015, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa Julai, 2018 hadi Juni 2019 Tancoal imeuza tani 788,702 za makaa ya mawe. Hili ni ongezeko la zaidi ya asilimia 300 katika kipindi cha miaka minne iliyopita," ilieleza taarifa hiyo.

Kadhalika, ilieleza kuwa katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Oktoba 31, mwaka huu, Tancoal imeshauza tani 225,616 za makaa ya mawe na kwamba mauzo hayo siyo ya ndani tu bali soko la mauzo nje ya nchi yameongezeka kwa wastani wa asilimia 30 ya mauzo yote, na kuiingizia serikali mapato ya kigeni.

Ilieleza kuwa Tancoal inatarajia kuongeza mauzo ya makaa ya mawe nchi za nje kupitia Bandari ya Mtwara nchi za Uturuki, Madagasca na Ethiopia, ambazo zimeonyesha nia ya kununua.

"Tancoal itaendelea kuunga mkono uendelezaji wa viwanda vya ndani kwa kuwasambazia makaa ya mawe yaliyo bora na kwa bei rahisi ambayo yanatumia katika uzalishaji na kuendeleza viwanda, Tancoal tunasambaza makaa ya mawe katika viwanda vyote vya saruji nchini kwa bei nzuri," ilieleza taarifa hiyo.

Ilieleza kuwa Tancoal inaipongeza serikali ya awamu ya tano kwa uongozi mzuri uliosababisha kuleta mafanikio hayo chanya katika kampuni.

## Jalada anayedaiwa kuua mke lipo kwenye hatua ya kuchapishwa

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya mauaji ya Naomi Marijani, inayomkabili Hamisi Luwongo, umedai mahakamani jalada la kesi hiyo bado lipo kwenye hatua ya kuchapishwa baada ya upelelezi kukamilika.

Kesi hiyo ilitajwa jana mbele ya Hakimu Mwandamizi, Salum Ally.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba jalada la kesi hiyo bado lipo kwenye hatua ya kuchapwa.

"Mheshimiwa hakimu jalada la kesi hii bado linaendelea kuchapwa na halijakamilika bado na likikamilika litapelekwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) kwa ajili ya kusomwa na maelekezo zaidi," alidai Wankyo.

Hakimu Ally alisema kesi hiyo itatajwa Desemba 2, mwaka huu na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Katika kesi ya msingi, mfanyabiashara huyo anakabiliwa na kesi ya kumuua mke wake, Naomi Marijani, Mei 15, mwaka huu, katika eneo la Gezaulole Kigamboni, jijini Dar es Salaam.



**Mfanyabiashara huyo anakabiliwa na kesi ya kumuua mke wake, Naomi Marijani, Mei 15, mwaka huu, katika eneo la Gezaulole Kigamboni, jijini Dar es Salaam.**



Mwanasheria Mwandamizi wa Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Wakili Manchare Heche Suguta (kushoto), akijadiliana jambo na wahitimu wenzake, baada ya kutunukiwa Shahada ya Pili ya Umahiri wa Sheria za Kimataifa za Mazingira, katika Mahafali ya 49 ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) juzi. Wa pili kulia ni Wakili Albert Msando. **PICHA: MARY GEOFREY**

## Wenye ulemavu watakiwa kujikubali

**Na Mary Geofrey**

WATU wenye ulemavu nchini, wametakiwa kujikubali kwa upungufu walionao, kutokata tamaa na kutumia vipaji walivyonavyo ili kujikwamua kiuchumi.

Wito huo ulitolewa na Balozi wa Tuzo za 'I Can', zinazotolewa na Taasisi ya Dk. Reginald Mengi, inayojihusisha na watu wenye ulemavu, Wakonta Kapunda, wakati akizungumza na washiriki wa semina ya kutambua kipaji ijulikanayo kama Thamani ya Kipaji iliyofanyika mwishoni mwa wiki, jijini Dar es Salaam.

Alisema vijana wengi na watu wenye ulemavu wanashindwa kufikia malengo yao na kutambua vipaji vyao kwa sababu hawajajikubali na kuamua kuchukua hatua.

"Mimi tangu nilipopata ajali na kutambua kuwa viungo vyangu haviwezi kufanya tena kazi zaidi ya kichwa, niliamua kujikubali na kufanya jitihada za kutambua kipaji changu hivyo kuanzia hapo nimekuwa nafanya mambo makubwa licha ya kuwa na ulemavu huu," alisema Wakonta.

Wakonta ambaye alishinda Tuzo ya Mafanikio katika ujuzi wa kipekee, mwezi Machi mwaka huu, iliyotolewa na Taasisi ya Dk. Mengi, alipata ajali akiwa na miaka 19 iliyomsababishia ulemavu unaomfanya atumie ulimi wake kuandika muswada wa filamu ili kujipatia fedha.

"Nimefanikiwa kuendeleleza ndoto yangu ya uandishi wa filamu kwa kutumia ulimi wangu, ambao ndio pia ninaotumia kujibu simu na kuandika ujumbe mfupi wa simu ya mkononi," alisema Wakonta.

Naye Mwanzilishi wa Taasisi isiyo ya Kiserikali ya 'The Dreamers Development Organization', iliyoendesha semina hiyo, Grace Meena, alisema watu wengi hususani vijana hawatimizi malengo yao kwa sababu hawajataka kufuatilia ndoto zao na kuanza kuziishi na badala yake wanafanya kazi na kuishi ndoto za wengine.

"Watanzania wengi hawaishi kwenye ndoto zao, wanaishi ndoto za wengine ndio sababu wanasuasua katika kufikia malengo yako, hivyo kama taasisi tunatoa elimu ya kujitambua na kufahamu kipaji chako na kukisimamia kikue," alisema Rose.

Alisema wanatoa elimu kwa jamii kupitia vikundi kuhusu namna ya kutambua vipaji vyao na kuwafanya watimize ndoto zao.

Alisema pia wamekuwa wakitoa elimu ikiwamo ya ujasiriamali, usimamizi wa fedha na masuala mengine ambayo yatarahisisha mtu kutumia kipaji chake katika kuleta mafanikio katika jamii.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MASHINE INAUZWA** DE-OILING MACHINE. Mashine ya kukausha mafuta kutoka katika vyakula vilivyokaangwa na mafuta kwa mfano Crisps, karanga, korosho nk. Kwa mawasiliano: 0764 127 853 / 0762 222 407 / 0628 883 003.

**MASHINE INAUZWA,** SEASONING MACHINE. Mashine ya kuchanganya chumvi au pilipili nk. Kwenye vyakula kama karanga, korosho, crisps nk. Kwa mawasiliano piga simu namba: 0764 127 853 / 0762 222 407 / 0628 883 003.

**MASHINE INAUZWA,** PACKING MACHINE. Mashine ya kupaki karanga, korosho, crisps nk. Kwa mawasiliano piga simu namba: 0764 127 853 / 0762 222 407 / 0628 883 003.

**2 ACRE YARD FOR RENT**

Facing New Julius Nyerere International Airport. Call: +255 754 375 967. Email: **gold@goldtz.net**

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila*

## KUPOTEA KWA VYETI



**ATHUMANI MOHAMED** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1216/0046** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la taifa mwaka 2004 katika shule ya Sekondari Merriwa, Cheti cha Ualimu chenye index namba **E.511/0128** kilichotolewa na Chuo cha Ualimu Bustani mwaka 2006. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochcote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DOD/DOD/RB/456684/2013**

115523002

## KUPOTEA KWA VYETI



**TUMAINI DAUD PHILIPO** MKAZI WA USANDA HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA. ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHAKE CHA SHULE KIDATO CHA NNE AMBACHO KILIPOTEA MAENEO YA NYEGEZI MKOANI MWANZA MWAKA HUU NAMBA YA SHULE S 1239 SAMUYE SECONDARY SCHOOL NAMBA YAKE YA **MTIHANI 0081/ 2007** KWA YEYOTE ATAKAE KIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA TUMAINI DAUD PHILIPO KWA SIMU NAMBA 0767372040 **MWA/NY/RB/371658/2019 CONTROL NAMBA 9910810246552.**

215523102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;222/2019**

**Ombi la MAGDALENA MUSTAFA MPANUKA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MUSSA HAMILI LUTALAGO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 18/11/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/11/2019

215523502

## KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**PAULINA P MUNISH**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota Paso **T 145 CZN** yenye Chassis namba **KGCI0-0058121** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Polisi Taafifa: **MOSH/TR/RB/2344/2019**

215523402

**THE COMPANIES ACT NO.12 OF 2002**

**NGANA FINANCE LIMITED**


**TAARIFA KWA UMMA**

Tunapenda kutoa tangazo kwa umma kuwa Kampuni ya Ngana Finance Limited yenye usajili **Na.134502** iloyo na ofisi zake maeneo ya Jiji la Dar es Salaam inafungwa kwa hiyari ya wanahisa wenyewe.

Hivyo tunaomba kama kuna taasisi au mtu yeyote ana madai awasiliane na sisi kupitia anwani ifuatayo, ndani ya siku 14 tangu tarehe ya kutolewa tangazo hili.

**Auditax International**
**PPF Tower, 7TH Floor**
**P.O BOX 77949**
**Dar Es Salaam.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ADAM G. MAJOLLO** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo cheti cha kidato cha nnae chenye index namba **S.3561/0133** kilichotolewa na Baraza la taifa mwaka 2012 katika shule ya Sekondari Salma Kikwete. Na cheti kingine cha kidato cha nne chenye index namba **P.1445/0136** kilichotolewa na Baraza la taifa mwaka 2015 katika shule ya Sekondari Kenton Mwenge Centre. Yeyote atakaevion ataoe taarifa kituo chcohcote cha Polisi. Polisi Taarifa: **WMB/RB/3985/2019**

115522102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Katika Mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**
**wilaya ya DODOMA**

**MADAI NAMBARI 274/2019**

**MDAI.................................MARTIN KHAN MAGUCHI**

**MDAIWA........................DICKSON BENSON NYAMRIBA**

**KWA DICKSON BENSON NYAMRIBA**
**JKT MAKUTOPORA 834**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba **MADAI YA TSH.4,472,000/=**

Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Jumatatu tarehe 25/11/2019 saa 2.00 asubuhi kwa kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo, ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Na kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama itathibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 6/11/2019.

215522702

**ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPLIES T. LTD &COURT BROKER**

Distributed via ippmedia

## MNADA WA HADHARA

UTAFANYIKA TAREHE 17/12/2019 SAA 4: ASUBUHI, KWA IDHINI YA MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA DODOMA MJINI TUTAUZA NYUMBA ILIYOKO NZUGUNI B KWA KUFIDIA DENI ANALODAIWA NA MWITA JOSEPH MSIMBETA .

**MAWASILIANO PIGA NO. 0713913150.**

215522902

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MURTAZA FIDAHUSEIN ESSAJEE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 629 DPL TOYOTA IST** YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI TAARIFA YA POLISI: **DAR/CHA/RB/477578/2019**

215523302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;231/2019**

**Ombi la TABU JUMA NDEHERE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SELEMAN SHOMARI KIPWASA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 26/11/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 13/11/201

215523602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Katika Mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**
**wilaya ya DODOMA**

**MADAI NAMBARI 273/2019**

**MDAI...........................MARTIN KHAN MAGUCHI**

**MDAIWA...........................RAJABU JUMA RAJABU**

**KWA RAJABU JUMA RAJABU**
**JKT MAKUTOPORA 834**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba **MADAI YA TSH.3,499,000/=**

Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Jumatatu tarehe 25/11/2019 saa 2.00 asubuhi kwa kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo, ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Na kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama itathibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 6/11/2019.

215522702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Katika Mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**
**wilaya ya DODOMA**

**MADAI NAMBARI 274/2019**

**MDAI..........................MARTIN KHAN MAGUCHI**

**MDAIWA............................................DAUD DAUD**

**KWA DAUD DAUD**
**JKT MAKUTOPORA 834**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba **MADAI YA TSH.4,299,000/=**

Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Jumatatu tarehe 25/11/2019 saa 2.00 asubuhi kwa kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo, ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Na kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama itathibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 6/11/2019.

215522702

**IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL**
**FOR MWANZA AT MWANZA**

**APPLICATION No 265 OF 2019**

**ESTER CHARLES ALEXANDER.....................APPLICANT**

**VERSUS**

**BRAYNA COMMUNICATION & ANOTHER.........RESPONDENT**

**SUMMONS / NOTICE**

**TO: BRAYNA COMMUNICATION CO.**
**c/o PROCESS SERVER**

Take notice that the above matter is coming for mention on 10th day of October 2019 at 9:00 A.M, Before Hon. Masao E, Chairman of the Tribunal.

You are hereby commanded to appear in person or by an advocate or by authorized agent to this Tribunal on the fixed date without fail.

A copy of application is attached herewith.
Given under my Hand and Seal of this Tribunal this 8th day of October 2019.

215522501

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Charles Katebi Buluba** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya Suzuki Carry yenye usajili wa namba **T 886 DEB.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi taarifa:/ **DAR/RB/480038/2019**

215522002

*Uza, Chenye Thamani Kubwa*

*Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa*

*Tupigie 0767 223311*

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# MAN UNITED YATAJA NANE INAOWATAKA

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imetaja majina ya nyota nane inayowataka katika usajili wa majira ya kiangazi.

Wachezaji ambao wanawindwa na Man United ni Callum Wilson (Bournemouth), John McGinn, Jack Grealish (Aston Villa), Erling Braut Haaland (pichani) anayeichezea Red Bull Salzburg.

Pia wamo winga wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, Declan Rise (West Ham United), James Maddison (Leicester City) na Moussa Dembele wa Lyon. Kocha Ole Gunnar Solskjaer ameanza uchunguzi wa ubora wa wachezaji hao akitaka kusajili katika dirisha dogo Januari, mwakani au majira ya kiangazi.

Pi anawinda kwa nguvu saini ya mshambuliaji wa Juventus, Mario Mandzukic ambaye ameonyesha nia ya kujiunga na klabu hiyo ya Old Trafford. Man United inataka washambuliaji wazoefu kuziba pengo la Romelu Lukaku na Alexis Sanchez waliojiunga na Inter Milan ya Italia.

Distributed via ippmedia

# Benzema atangaza kisichowezekana Fifa

**PARIS,** Ufaransa

KARIM Benzema amesema kwamba anataka kuhamia timu nyingine ya taifa baada ya kutoswa moja kwa moja na Ufaransa.

Licha ya kuwa mmoja kati ya washambuliaji bora duniani kwa muda mrefu, Benzema hajaitwa katika kikosi cha Ufaransa kwa muda mrefu kutokana na kesi iliyomkabili dhidi ya nyota mwenzake wa zamani wa kikosi cha Ufaransa, Mathieu Valbuena.

Ilidaiwa Benzema pamoja na kundi la marafiki zake wasiokuwa wanasoka walimwambia Valbuena awape fedha ili wasiusambaze mkanda wa ngono wa nyota huyo. Benzema alikosa michuano ya Euro 2016 iliyofanyika Ufaransa, lakini akakosa katika michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2018 ambapo Ufaransa ilitwaa taji hilo.

Na sasa ametumia mtandao wake wa kijamii kudai anafikiria kwenda kucheza taifa jingine ikiwa ni jibu lake baada ya kukerwa na kauli iliyotolewa na Rais wa Shirikisho la Soka la Ufaransa, Noel Le Graet hivi karibuni.

"Noel, nilidhani haufanyi kazi ya kuingilia maamuzi ya makocha. Nataka ujue ni mimi mwenyewe tu ndiye ambaye ninaweza kumaliza maisha yangu ya soka la kimataifa. Kama unadhani nimeisha acha nicheze katika moja kati ya nchi ambazo naruhusiwa kuchezea na tutaona," aliandika Benzema.

Benzema ambaye wazazi wake wana asili ya Algeria hataweza kuwakilisha taifa jingine kutokana na sheria za Fifa kutomruhusu mchezaji aliyelichezea taifa jingine mechi za kimashindano kwenda kuhamia timu nyingine ya taifa.





# Ronaldo anyemelea rekodi mabao kimataifa

**LISBON,** Ureno

CRISTIANO Ronaldo amefikisha mabao 99 akiwa na timu ya Taifa ya Ureno alipofunga wakati wakiibuka na ushindi dhidi ya Luxembourg.

Hiyo ina maana kuwa Ronaldo kwa sasa anaisaka rekodi ya nyota wa zamani wa Iran, Ali Daei mwenye mabao 109. Ronaldo juzi alifunga bao na kuchangia ushindi wa mabao 2-0 iliyopata Ureno dhidi ya Luxembourg katika mechi ya kufuzu fainali za Kombe la Ulaya.

Ronaldo yuko nyuma mabao 10 dhidi ya nguli wa Iran, Ali Daei mwenye mabao 109 kwenye timu ya taifa.

"Rekodi zimewekwa ili zivunjwe na nitaivunja," alisema nyota huyo wa Juventus. Bruno Fernandes alitangulia kufunga bao kabla ya Ronaldo kuongeza jingine dakika sita kabla ya mpira kumalizika.Licha ya kufunga bao, nguli huyo alisema hakuwa fiti katika mechi mbili zilizopita akiwa na Juventus.

"Sikuwa fiti kwa asilimia 100 kwa takriban wiki tatu zilizopita, nilicheza kwa kiwango cha chini kuhofia majeraha zaidi," alisema Ronaldo.

## HABARI MICHEZO

# Southgate asifia kikosi Sterling akirejea England

**LONDON,** England

GARETH Southgate amedai kwamba, England ilikuwa imara zaidi baada ya kufanyia kazi ugomvi wa Raheem Sterling na Joe Gomez na walimaliza kampeni yao ya kufuzu michuano ya Euro 2020 kwa ushindi mnono.

Baada ya kuachwa kwenye kikosi cha England kilichoibuka na ushindi wa mabao 7-0 dhidi ya Montenegro baada ya kukwaruzana na Gomez, Sterling alirudi kwenye kikosi cha Southgate ambacho kiliibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Kosovo na yeye alihusika na mabao ya Harry Kane na Marcus Rashford.

Southgate aliwasifia wachezaji wake kwa kuweza kuwa na umoja na kushinda mchezo huo.

"Unatakiwa kufanya kazi kwa kupitia nyakati ngumu," alisema Southgate akiiambia ITV.

"Kundi lote lilifanya vizuri na kwa uhakika kabisa walicheza kwa kujituma na walikuwa imara zaidi.

"Wachezaji walicheza kwa kujituma na kwa uhakika tumemaliza kampeni ya kufuzu Euro 2020 kwa mafanikio makubwa kabisa.

"Naamini nitakuwa na kikosi imara zaidi kwenye michuano ya Euro, na hasa kutokana na kiwango bora kilichoonyeshwa na wachezaji wangu."

Akizungumzia ugomvi wa Sterling na Gomez, Southgate alisema walifanyia kazi uhusiano wao na kwamba, kwa sasa hakuna lolote baya kati yao.

"Tulizungumza nao na kila mmoja alionyesha heshima kwa mwenzake, hivyo hakuna jambo baya kwa sasa."






# SANCHEZ KUREJEA DIMBANI MAPEMA

**MILAN,** Italia

ALEXIS Sanchez anaweza kurudi uwanjani kwa mechi zinazokuja za Inter Milan mapema zaidi baada ya kuwa nje ya dimba kwa muda kutokana na kuumia 'enka'.

Sanchez aliumia enka wakati akiichezea Chile dhidi ya Colombia Oktoba mwaka huu.

Alifanyiwa operesheni ambayo ilibainishwa kuwa atakaa nje ya dimba kwa kipindi cha miezi mitatu.

Mkuu wa matibabu wa Inter, Piero Volpi ameiambia La Cuarta kwamba, maendeleo ya Sanchez yanaonyesha kwamba anapona kwa haraka na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, anaweza kurudi uwanjani haraka.

"Aliumia vibaya, lakini anapona kwa haraka, na anaweza kurudi uwanjani haraka zaidi," alisema.

"Katikati ya Januari anaweza kurudi uwanjani, lakini tunaona. Alexis anaweza kurudi haraka zaidi.

"Bado hajaanza mazoezi, lakini tuna matumaini atarudi uwanjani haraka inavyowezekana."

Sanchez alifunga bao pekee kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, wakati Inter ikiibuka na ushindi wa 3-1 dhidi ya Sampdoria ambapo baadaye alitolewa nje kwa kadi nyekundu.

# *Abidal: Neymar bado ni chaguo la Barca*

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA mara zote itataka kumsajili Neymar, lakini ugumu wa kifedha ndiyo utakaosababisha zoezi hilo kushindikana, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Soka wa klabu hiyo, Eric Abidal.

Neymar alikaribia kusajiliwa tena pale Camp Nou kipindi cha majira ya joto yaliyopita, ikiwa ni miaka miwili tangu aondoke na kujiunga na Paris Saint-Germain kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Barca walifanya mazungumzo na PSG, lakini walishindwa kufika bei iliyokuwa ikitakiwa na mabingwa hao wa Ligue 1. Lionel Messi alibainisha kwamba baadhi ya watu hapo Catalunya hawataki kuona Neymar akirudi.

"Mchezaji mkubwa ambaye ana falsafa ya Barca na ana kiwango kizuri mara zote atakuwa chaguo la kwanza kwa Barcelona," alisema Abidal akiliambia Gazeti la Mundo Deportivo.

"Tunaweza kufanya maamuzi ya kwenye idara yetu, lakini mambo ya fedha yanaweza kuwa magumu.

"Siwezi kusema kwamba yeye anabakia kuwa chaguo la kwanza, kwa sababu msimu ni mrefu, lakini kwa uhakika kabisa yeye ni chaguo letu."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GRIEZMANN: BARCA PAGUMU KUCHEZA

Si sehemu rahisi, ni timu mpya, klabu tofauti, mbinu mpya, nafasi mpya na jukumu kwangu, lakini...

**BARCELONA,** Hispania

ANTOINE Griezmann amekiri kuunganishwa kwake kwenye maisha ya Barcelona haikuwa rahisi lakini licha ya kuwa pagumu kwake, bado anashawishika kwamba atafanikiwa hapo Camp Nou.

**Baada ya mwaka mmoja wa tetesi na uvumi wa uhamisho, hatimaye Barca ilifanikiwa kunasa saini ya Griezmann akitokea Atletico Madrid, kwa kulipa euro milioni 120 zilizohitajika kuvunja mkataba wake.**

Wakati akiwa na mabao manne na pasi tatu za mwisho kwenye mechi 11 za LaLiga, kiwango cha Griezmann kwa ujumla kimeshindwa kuhamasisha msisimko mwingi kwa mashabiki na kuwaacha wakiwa na wasiwasi.

Ilidhaniwa kutua kwake kungeweza kuleta presha kwa nyota wa klabu hiyo, Lionel Messi, lakini Muargentina huyo anaendelea kubeba majukumu makubwa ya ubunifu begani mwake.

Baada ya Kocha wa Barca, Ernesto Valverde hivi karibuni kudai Mfaransa huyo bado anahitaji kuzoea staili ya uchezaji ya timu hiyo, Griezmann anaamini atajizatiti kwa wakati na wala hajutii kuhusu uamuzi wa kujiunga na Barca.

"Barcelona si sehemu rahisi [ya kucheza]," alisema katika mahojiano na Telefoot. "Ni timu mpya, klabu tofauti, mbinu mpya na nafasi mpya na jukumu kwangu. Lakini ni nini, na ni wakati wa kufanya kazi.

"Ninajisikia fahari kwa uamuzi na wapi nilipo, na itakuwa kazi ambayo itatatua kila kitu. Niamini na kila kitu kitakuwa kizuri.

"Kusudi langu sasa ni kuwa mchezaji muhimu katika klabu, kupata dakika zaidi, kufunga mabao mengi, kutoa pasi nzuri, kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa na kuwa kwenye ligi, kuwa tayari kwa timu ya Taifa [ya Ufaransa] Machi na pia kwa Euro 2020.

"Mimi ni mchezaji ambaye nafikiri kuhusu timu. Ninaweza kufunga mabao mengi, lakini hilo si lengo langu kuu. Lengo langu ni kuisaidia timu kwa namna yoyote niwezavyo."

## ZISIKUPITE

### EMERY APEWA MWEZI ARSENAL

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery amepewa mwezi mmoja kuokoa kibarua chake. ***(Sun)***

### RONALDO AKANA BIFU NA SARRI

MSHAMBULIAJI wa Juventus na Ureno Cristiano Ronaldo, 34, amesema hana tatizo na kocha wa timu hiyo, Maurizio Sarri kufuatia kufanyiwa mabadiliko 'sub' hivi karibuni. ***(Corriere dello Sport)***

### MARTINEZ KUMRITHI SUAREZ

MKURUGENZI wa Soka wa Barcelona, Eric Abidal amethibitisha klabu hiyo inavutiwa kumsajili mshambuliaji wa Inter Milan na Argentina, Lautaro Martinez, 22, kama mbadala wa straika wa kimataifa wa Uruguay, Luis Suarez, 32. ***(Mundo Deportivo)***

### BATSHUAYI KUBAKI CHELSEA

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Mbelgiji Michy Batshuayi, 26, anataka kubaki katika klabu hiyo na kupigania namba kuliko kuondoka dirisha la Januari. ***(Sun)***

### UPAMECANO AWINDWA CITY

MANCHESTER City inazingatia kutoa ofa dirisha la Januari kwa beki wa RB Leipzig, Dayot Upamecano, 21. ***(90 Min)***

### BARCA YAMBANIA RAKITIC EPL

BARCELONA imekataa hofa kutoka klabu za Ligi Kuu England zinazohitaji huduma ya kiungo Mcroatia Ivan Rakitic kwa pauni takriban milioni 13, ambazo ni pungufu ya pauni milioni 17 ya bei anayodhaminishwa nayo mchezaji huyo wa zamani wa Sevilla mwenye umri wa miaka 31. ***(Sport)***

### XHAKA CHAMBO YA ZAKARIA

ARSENAL itamtoa ofa kiungo Mswisi Granit Xhaka, 27, kwa Borussia Monchengladbach kama sehemu ya kukamilisha dili lao la kwanza lililokataliwa la kumsajili kiungo Denis Zakaria, ambaye ni raia wa Uswisi. ***(Mirror)***

### UTD KUKOMAA KWA HAALAND

MANCHESTER United inaweza kujaribu kumsajili Erling Braut Haaland, 19, kutoka Red Bull Salzburg katika dirisha la Januari na kisha kumtoa kwa mkopo kwa klabu hiyo ya Austria kwa kipindi chote cha msimu kilichobaki. ***(ESPN)***

### PALACE KUMFUATA EDOUARD

CRYSTAL Palace itatoa ofa ya pauni milioni 20 kwa straika wa Celtic, Mfaransa Odsonne Edouard, 21. ***(Sun)***

### MADRID, BARCA KWA SKRINIAR

REAL Madrid na Barcelona zinaweza kuingia katika mbio moja ya kuwania saini ya beki wa Inter Milan, Mslovakia Milan Skriniar, 24, ambaye amekuwa akiwindwa na Manchester United. ***(Corriere dello Sport)***

### YOUNG LULU UTD, ARSENAL

MANCHESTER United na Arsenal zinamfuatilia kipa kinda wa Hartlepool, Brad Young, 17. ***(Sun)***

### BERGE AISIKILIZIA LIVERPOOL

KIUNGO wa Genk na Norway, Sander Berge, 21, ambaye amekuwa akihusishwa na Liverpool na Napoli, amekiri kucheza Anfield kutakuwa ni "ndoto". ***(Mirror)***